# KUCHUNGUZA USANAA WA LUGHA KATIKA KUJENGA DHIMA ZA NYIMBO ZA HARUSI KATIKA JAMII YA WAASU

**ELIHAKI YONAZI**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

## MSIMAMIZI

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kwamba amesoma tasinifu hii yenye mada: ñ***Kuchunguza Usanaa wa Lugha katika Kujenga Dhima za Nyimbo za Harusi Katika Jamii ya Waasu”*** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili (M.A. Kiswahili) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

é é é é é é é é é é é é é é ..

Dkt. Omary Mohamed Maguo

(Msimamizi)

é é é é é é é é é é é é é é .

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ile ya tasinifu hii, kwa njia yoyote kama vile kielektroniki, kurudufu nakala au kurekodi bila ya idhini ya mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## TAMKO

Mimi, **Elihaki Yonazi,** ninakiri rasmi kwamba, tasinifu hii inayohusu **'Kuchunguza Usanaa wa Lugha katika Kujenga Dhima za Nyimbo za Harusi katika Jamii ya Waasu,** ni kazi yangu mwenyewe. Haitatolewa na haijatolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya Uzamili au shahada nyingine yoyote katika Chuo Kikuu kingine chochote.

é é é é é é é é é é é é é é ..

Saini

é é é é é é é é é é é é é é

Tarehe

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa bibi Santiel Saghuri kwa juhudi zake kubwa za kunilea. Mungu ampe pumziko la milele. Amen.

## SHUKRANI

Awali ya yote, ninapenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kitaaluma, na zaidi sana kuniwezesha kuikamilisha kazi hii. Jina lake lihimidiwe milele na milele. Aidha, ninatoa shukurani za pekee kwa msimamizi wangu, Dkt Omary Mohamed Maguo, kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti. Kwa hakika hakusita wala kuchoka katika kunishauri na kunirekebishia kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika.

Kwa upande mwingine, shukurani zangu za dhati ziende kwa wazazi na walezi wangu, hasa mama yangu mzazi Elidia Yonafika. Aidha, ninawashukuru sana wahadhiri wangu wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kuniwezesha kufikia hatua hii. Baadhi yao ni Prof. E. Mmbogo, Dkt Hilda Pembe na Dkt Zelda. Wengine ni ndugu na rafiki zangu wote, akiwamo mwalimu G. Mwangosi.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu kuchunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Ili kutimiza lengo hilo tulikuwa na malengo mahsusi mawili; kuchunguza dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu; na kujadili usanaa wa lugha unaotumika katika ujenzi wa dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Data za utafiti zilikusanywa kwa mbinu za hojaji, ushiriki, usaili na ile ya kinyaraka. Mjadala wa data ulioongozwa na nadharia za Uhalisia na Simiotiki. Nadharia hizo zilikuwa muafaka katika uchambuzi na mjadala wa vipengele vilivyolengwa katika utafiti huu. Kipekee, nadharia hizi ziliteuliwa kwa misingi ya kutegemeana na kukamilishana ili kukidhi malengo mahsusi ya utafiti. Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zina dhima nyingi. Baadhi yake ni kudumisha upendo, kudumisha heshima, kupongeza na kuwasifu maharusi, kuhimiza ukarimu na ushirikiano, kurekebisha tabia, kuonesha masikitiko na uvumilivu na kuonya. Kimsingi, nyimbo hizo hutazamwa kama kiungo thabiti cha kijadi kinachohakiki na kujenga misingi ya kuifunza jamii na kuielewa historia, mila na desturi, pamoja na mazingira yao kwa kuzingatia maendeleo ya kijamii. Vipengele vya kisanaa vilivyochunguzwa ni; taswira na ishara, jazanda/mafumbo, chuku, tashibiha na takriri. Vipengele vingine ni dhihaka na methali. Usanaa wa katika vipengele hivyo umeonesha mchango mkubwa, unaoongeza nguvu na kujenga mvuto wa kipekee unaolenga kuihamasisha jamii kupata undani wa jambo lililolengwa.

# YALIYOMO

**MSIMAMIZI** ..... **ii**

**HAKIMILIKI** ..... **iii**

**TAMKO** ..... **iv**

**TABARUKU** ..... **v**

**SHUKRANI** ..... **vi**

**IKISIRI** ..... **vii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **xiii**

**ORODHA YA VIFUPISHO** ..... **xiv**

**SURA YA KWANZA** ..... **1**

**UTANGULIZI** ..... **1**

1.1 Utangulizi wa Jumla ..... 1

1.2 Usuli wa Tatizo ..... 1

1.3 Tatizo la Utafiti ..... 4

1.4 Lengo la Utafiti ..... 6

1.4.1 Malengo Mahsusi ..... 6

1.4.2 Maswali ya Utafiti ..... 6

1.5 Umuhimu wa Utafiti ..... 6

1.6 Mawanda ya Utafiti ..... 7

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake ..... 8

1.8 Mpangilio wa Tasnifu ..... 8

**SURA YA PILI** .......... **9**

**MAPITIO YA MAANDIKO NA MKABALA WA KINADHARIA** .......... **9**

2.1 Utangulizi .......... 9

2.2 Dhana ya Nyimbo .......... 10

2.3 Chimbuko la Nyimbo .......... 12

2.4 Dhima za Nyimbo kwa Ujumla .......... 14

2.5 Tafiti Tangulizi Kuhusu Nyimbo .......... 18

2.6 Pengo la Utafiti .......... 22

2.7 Kiunzi cha Nadharia .......... 22

2.7.1 Nadharia ya Uhalisia .......... 23

2.7.2 Nadharia ya Simiotiki .......... 26

2.8 Hitimisho .......... 30

**SURA YA TATU** .......... **32**

**MBINU ZA UTAFITI** .......... **32**

3.1 Utangulizi .......... 32

3.2 Eneo la Utafiti .......... 32

3.3 Usanifu wa Utafiti .......... 33

3.5 Populesheni Lengwa ya Utafiti .......... 34

3.6 Sampuli na Usampulishaji .......... 34

3.6.1 Sampuli .......... 34

3.6.2 Usampulishaji .......... 35

3.7 Vyanzo vya Data .......... 37

3.7.1 Data za Msingi ........................................................................ 37

3.7.2 Data za Upili ........................................................................ 38

3.8 Ukusanyaji wa Data ........................................................................ 38

3.8.1 Mbinu ya Hojaji ........................................................................ 39

3.8.2 Mbinu ya Usaili ........................................................................ 39

3.8.3 Mbinu ya Ushiriki ........................................................................ 40

3.8.4 Upitiaji wa Nyaraka ........................................................................ 41

3.9 Uchambuzi wa Data ........................................................................ 41

3.10 Itikeli ya Utafiti ........................................................................ 42

3.11 Usahihi wa Data ........................................................................ 43

3.12 Hitimisho ........................................................................ 44

**SURA YA NNE ........................................................................ 45**

**UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ... 45**

4.1 Utangulizi ........................................................................ 45

4.2 Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasu ........................................................................ 45

4.3 Uchambuzi wa Dhima za Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasu ................ 47

4.3.1 Kudumisha Upendo ........................................................................ 48

4.2.2 Kudumisha Heshima ........................................................................ 51

4.2.3 Kuwapongeza na Kuwasifia Maharusi ........................................................................ 55

4.2.4 Kusisitiza Ukarimu na Ushirikiano ........................................................................ 59

4.2.5 Kurekebisha Tabia ........................................................................ 63

4.2.6 Kuonesha Masikitiko na Uvumilivu ........................................................................ 65

4.2.7 Kuonya ........................................................................ 69

4.3 Hitimisho ........................................................................ 72

**SURA YA TANO ..... 73**

**USANAA WA LUGHA KATIKA KUJENGA DHIMA ZA NYIMBO ZA HARUSI ZA JAMII YA WAASU ..... 73**

5.1 Utangulizi ..... 73

5.2 Usanaa wa Lugha katika Kujenga Dhima za Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasu ..... 73

5.2.1 Jazanda ..... 74

5.2.2 Ishara ..... 79

5.2.3 Takriri ..... 81

5.2.4 Tashibiha ..... 85

5.2.5 Chuku ..... 88

5.2.6 Dhihaka ..... 91

5.2.7 Methali ..... 95

5.3 Hitimisho ..... 98

**SURA YA SITA ..... 99**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... 99**

6.1 Utangulizi ..... 99

6.2 Muhtasari wa Tasinifu ..... 99

6.3 Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika ..... 100

6.4 Matokeo ya Utafiti ..... 100

6.4.1 Lengo la Kwanza ..... 100

6.4.2 Lengo la Pili ..... 101

6.5 Mchango wa Utafiti ..... 102

6.6 Mapendekezo ..... 102

6.6.1 Mapendekezo ya Kitaaluma ........ 102
6.6.2 Mapendekezo kwa Serikali ........ 103
6.6.3 Mapendekezo kwa Jamii ........ 103
**MARELEJEO ........ 104**
**VIAMBATANISHO ........ 114**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Sampuli ya Utafiti.......................................................................37

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Dkt | Daktari |
| DUP | Dar es Salaam University Press |
| Jr | Juniour |
| Kiambt. | Kiambatanisho |
| Ltd | Limited |
| M.A | Master of Arts |
| OUT | Open University of Tanzania |
| Prof. | Profesa |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| Taz. | Tazama |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| Wah | Wahariri |
| Wenz. | Wenzake |
| Ke | Wanawake |
| Me | Wanaume |
| Kesht. | Keshatajwa |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi wa Jumla

Utafiti huu umechunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu kama kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi. Sura hii imeeleza masuala muhimu ya kiutangulizi kama vile usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia, umeeleza kuhusu umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na mpangilio wa utafiti.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

Utafiti huu umechunguza dhima na usanaa wa lugha katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Kijiografia, Waasu wanapatikana Kaskazini Mashariki mwa Tanzania katika wilaya za Same na Mwanga mkoani Kilimanjaro, lugha yao hujulikana kama Chasu au Kiathu/Kiasu (Mreta, 2008). Aidha Mreta (kesht.) anasema Waasu kwa jina lingine hufahamika kama Wapare na lugha yao kwa jina lingine hufahamika kama Kipare. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, wilaya ya Same ina jumla ya wakazi 269, 807; wanawake wakiwa 138, 292 na wanaume 131, 515. Kiutawala, wilaya ya Same imegawanyika katika tarafa sita, ambazo ni Same, Mwembembaga, Chomesuji, Mambavunta, Ndugu na Gonja. Aidha, wilaya ya Same inapakana na wilaya ya Mwanga kwa upande wa kaskazini. Kaskazini Mashariki inapakana na nchi ya Kenya, Kusini Mashariki inapakana na mkoa wa Tanga na upande wa Magharibi inapakana na mkoa wa Manyara (Taarifa kutoka Ofisi ya

Takwimu ï Same, 2018). Tasinifu hii imefanyika wilayani Same katika tarafa za Same na Mwembembaga.

Waasu wana utamaduni wao ambao umejikita zaidi katika fasihi simulizi na vipengele vyake kama vile nyimbo za harusi na ngoma, methali, vitendawili, ngano, majigambo na hadithi ambazo ni asasi muhimu za jamii hiyo katika maisha yao (Kimambo, 1967). Asasi hizo ni vyombo muhimu vinavyotumiwa na jamii hiyo katika kufikisha yale yaliyokusudiwa kuifikia jamii. Shughuli kuu za kiuchumi katika jamii ya Waasu ni kilimo cha mazao ya chakula kama vile ndizi, mahindi, viazi na matunda ya aina mbalimbali, pamoja na ufugaji.

Jamii za Kiafrika, zikiwamo za Tanzania zimekuwa zikitumia vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi kama vile methali, nyimbo, vitendawili na majigambo kama asasi mahususi za kijamii na vyombo vya mawasiliano huku vikiakisi harakati na mahitaji ya jamii kwa lengo la kuikosoa, kuielimisha, kuionya, kuiburudisha, kuiadibu na kutunza amali za jamii inayohusika (Sengo, 1973). Kimsingi jamii ya Waasu ni miongoni mwa jamii za Kitanzania na Afrika kwa ujumla, hivyo basi maelezo ya mtaalamu huyo yanajumuisha jamii ya Waasu na kuichunguza juu ya nyimbo zake za harusi kama mojawapo ya vipengele vyake vya fasihi simulizi.

Samara (1992) anaeleza kwamba nyimbo hutazamwa kama hazina ya urithi wa jamii inayohusika iliyosheheni taarifa na maarifa mengi. Hii ni kwa sababu nyimbo ni mojawapo ya nyanja katika maisha ya jamii ambayo huchangia sana katika kuiendeleza na kuidumisha historia ya jamii inayohusika. Aidha, nyimbo ni chombo kinachoihakiki jamii namna ilivyo na inavyoweza kujieleza kupitia kazi za kisanaa;

na hutumiwa kuukuza na kuuendeleza ufahamu mpana wa masuala na maarifa ya jamii. Umuhimu unaodokezwa ulimfanya mtafiti kuziteua nyimbo za harusi za jamii ya Waasu na kuzitumia kama mada kamili katika utafiti huu.

Fasihi ilitumika kama nyenzo ya kuyamudu mazingira na kujenga maadili na mwenendo kwa wanajamii wote. Fasihi ilitumika kikamilifu kama chombo mahsusi kilichotumiwa na wanajamii wote katika shughuli za kila siku za maisha yao (Mlacha na Hurskainen, 1995).

Kwa mantiki hiyo, jamii iliweza kuelimishwa kupitia tanzu za nyimbo, methali, misemo na vitendawili. Tanzu hizo ziliweza kubeba ujumbe ulioakisi hali na matukio mbalimbali yaliyojiri katika jamii inayohusika. Aidha, katika historia ya maendeleo ya binadamu duniani, fasihi ilianza zamani sana, tangu binadamu alipoanza kutumia lugha kama chombo kikuu cha mawasiliano (Ranger, 1996).

Aidha, katika jamii za Tanzania vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi, zikiwamo nyimbo za kijamii, zimekuwa zikitumika kama asasi mahsusi za kijamii na kimawasiliano. Kwa kawaida, nyimbo hizo zimekuwa zikiakisi mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika jamii ili kukidhi harakati za kijamii inayohusika. Mojawapo ya misingi yake ni kukuza na kuendeleza amali za kijamii kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo katika jamii inayohusika (Ndungo na Mwai, 1996). Pia, zimekuwa zikifanya kazi ya kusawiri maisha na kushughulikia mambo yanayomhusu binadamu, pamoja na jinsi anavyoingiliana na mazingira yake. Hoja ya mtaalamu huyu imesaidia kusukuma mbele utafiti wetu, kwani Waasu ni miongoni

mwa jamii za Tanzania, hivyo yaelezwayo katika jamii za Tanzania na jamii ya Waasu huwa ni miongoni mwayo.

Ulimwenguni kote, nyimbo za jamii mbalimbali hutazamwa kama nyenzo ya kuhifadhia tunu na amali zilizomo katika jamii inayohusika. Huu ndio msingi wa hoja ya Njogu na Chimerah (1999) kwamba, kabla ya kuwapo kwa taaluma ya uchapishaji katika jamii za Kiafrika, nyimbo za kiasili zilitumika kama magazeti na vitabu vilivyokuwa hazina ya kuhifadhia utamaduni, falsafa, historia na maendeleo ya jamii inayohusika. Kwa mujibu wa Alembi (2000), mambo yanayohusu taaluma zote za mwanadamu kama vile historia, dini, sheria, utamaduni, jiografia, siasa, uchumi na sayansi huhifadhiwa katika nyimbo. Kipekee, hali hiyo huzifanya nyimbo kutazamwa kama ghala ya rasilimali na amali za Uafrika.

Hivyo basi, Waasu nao kama miongoni mwa jamii za Kiafrika, masuala yao mbalimbali huelezewa kupitia nyimbo, zikiwamo nyimbo za harusi. Hivyo basi, jamii ya Waasu kama mojawapo ya jamii ya Tanzania na Afrika wa ujumla inayo nyimbo zake za harusi. Nyimbo hizi zinmekuwa zikitumika katika sherehe za harusi tangu zamani zikiwa zinatumia usanaa wa lugha wa aina mbalimbali. Utafiti huu umechunguza dhima ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu na usanaa wa lugha unaotumika katika kujenga nyimbo hizo.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Nyimbo za harusi za kijamii ni sehemu ya utamaduni wa kiasili uliozoeleka kwa muda mrefu katika jamii nyingi hapa nchini na barani Afrika (Okpewho, 1979 na

Mulokozi, 2011), lakini bado hazijapewa uzito wa kiutafiti unaostahiki katika taaluma ya fasihi. Aidha, dhima ya nyimbo za harusi huweza kutofautiana kwa kiasi fulani kutoka jamii moja kwenda nyingine. Hii ni kutegemeana na utamaduni wa jamii husika (Wamitila, 2004). Kwa upande mwingine usanaa wa lugha katika nyimbo za harusi nao huweza kutofautiana kutoka jamii moja kwenda nyingine, hii ni kutokana na jamii kutofautiana katika masuala ya; kiutamaduni, mazingira, falsafa, historia, na uchumi.

Baadhi ya watafiti kama vile; Perpetua (2011), Kauti (2013), Pembe (2013), Abdulla (2016) na Mlambia (2017), wamefanya utafiti katika vipengele mbalimbali vya nyimbo, zikiwemo nyimbo za harusi. Hata hivyo kipengele cha dhima za nyimbo za harusi na usanaa wa lugha katika ujenzi wa nyimbo hizo, hakijamakinikiwa na wataalamu hawa. Aidha, suala la dhima za nyimbo za harusi na usanaa wa lugha katika ujenzi wa nyimbo hizo ni suala ambalo halijafanyiwa utafiti bado katika jamii ya Waasu. Jambo hilo lilimpa mtafiti ari ya kutaka kujua, je, kuna dhima zipi, na usanaa upi wa lugha katika ujenzi wa dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu? Msukumo wa utafiti huu ni kutokana na ukweli kwamba dhima ni kipengele nyeti kwa kila utanzu wa fasihi, na kwamba nyimbo za harusi ni taasisi nyeti sana katika kuadili vijana, ambayo kwa kawaida kila mtu alipaswa kuipitia. Nyimbo huhusishwa na jukumu/kazi (dhima) fulani katika jamii (Mulokozi, 1996, Pembe, 2013, Samwel na wenzake 2013). Kwa hiyo, utafiti huu umefanywa ili kuchunguza dhima ya nyimbo za harusi za jamii ya Waasu na usanaa wa lugha utumikao katika ujenzi wa dhima hizo. Hivyo utafiti huu umekusudia kuziba pengo hilo la amaarifa.

## 1.4 Lengo la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu.

### 1.4.1 Malengo Mahsusi

Utafiti huu una malengo mahsusi mawili:

(i) Kubainisha dhima ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu.

(ii) Kujadili usanaa wa lugha unaotumika katika ujenzi wa dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu.

### 1.4.2 Maswali ya Utafiti

(i) Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zina dhima gani?

(ii) Ni usanaa upi wa lugha unaotumika katika ujenzi wa dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kitaaluma, tasinifu hii imetoa taarifa kuntu kuhusu dhima za nyimbo za harusi za Waasu. Kwa hiyo, utatumika kama nyaraka na marejeleo mahususi katika utafiti wa kazi za kifasihi. Wasomaji na wachambuzi watapanua mawanda yao ya uelewa kuhusu nafasi pana ya nyimbo za harusi za kijamii zinavyosaidia kujenga misingi ya kuielewa historia, falsafa, utamaduni na maendeleo yao kupitia kazi za kisanaa.

Kisera, utafiti huu utawafaa watunga sera katika kuainisha mambo ambayo yanastahili kuingizwa katika sera za kudumu za taifa ili kuimarisha mipango ya utekelezaji wa kazi za kisanaa kwa manufaa endelevu ya vizazi vilivyopo na vijavyo. Kwa msingi huo, watunga sera hawana budi kuunda sera zitakazolenga kuziimarisha nyimbo za kijamii kama sehemu mahsusi ya utamaduni wa taifa, kwa kuziingiza katika mifumo ya kitaaluma ya kitaifa kwa kuwa ni utanzu wenye nguvu katika harakati za kuiadilisha kijamii.

Kwa ujumla, utafiti huu utasaidia kuibua mjadala juu ya nafasi ya nyimbo za harusi za kijamii katika kuunda falsafa  za kijamii na kitaifa kwa kuzingatia muktadha mpana wa kimwingilianomatini unaovuka mipaka ya kijiografia na kihistoria. Aidha, utafiti huu utatumika kama kitambulisho cha nafasi ya nyimbo za kijamii katika masuala ya kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa, na jinsi fasihi inavyotazamwa kama chombo cha kiwakati na kiharakati kinachosawiri hali halisi iliyopo katika jamii.

## 1.6 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu kuchunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu waishio wilayani Same mkoani Kilimanjaro. Jumla zimeteuliwa nyimbo 30 tu zilizowasilishwa katika mjadala wa data zilizolengwa. Jamii ya Waasu imeteuliwa kwa kuwa ndiko zilikotamalaki nyimbo za harusi zilizolengwa ili kukamilisha malengo mahsusi yaliyobainishwa katika utafiti. Uchambuzi na mjadala wa data umeongozwa na nadharia za Uhalisia na Semiotiki.

### 1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Watafitiwa katika jamii ya Waasu waliihusisha kazi ya utafiti wa nyimbo za harusi za jamii hiyo na masuala ya kibiashara, ambapo baadhi yao waliamini kuwa mtafiti alikusudia kuzikusanya nyimbo zao kwa maslahi binafsi ya kibiashara. Kwa msingi huo, wengi hawakuwa tayari kufanya mahojiano na kutoa ushirikiano wa kutosha ili kupata data zilizolengwa. Hata hivyo, watafitiwa walilazimika kutoa ushirikiano baada ya mtafiti kwa kushirikiana na wasaidizi wake, pamoja na baadhi ya viongozi wa maeneo husika kuwaelimisha kwa kina kuhusu madhumuni ya utafiti wa kitaaluma.

### 1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Tasinifu hii imechunguza dhima na usanaa wa nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Aidha, tasinifu hii imegawanywa katika sura sita. Sura ya kwanza imeelezea vipengele vya usuli na tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake pamoja na mpangilio wa tasinifu. Sura ya pili imeelezea mapitio ya kazi tangulizi na nadharia za utafiti. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Sura ya nne na ya tano zimewasilisha uchambuzi wa data za utafiti. Sura ya mwisho ya utafiti huu ni sura ya sita ambayo imetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi yana umuhimu sana kwa mtafiti na utafiti. Kufanya mapitio ya kazi tangulizi humpa mtafiti msingi wa kinadharia, kanuni za utafiti wake kwa kuangalia nadharia walizotumia watafiti waliotangulia (Kumar, 2010). Pia, kazi tangulizi humpa mtafiti fursa ya kujenga mlingano wa utafiti ambao anataka kuufanya na tafiti ziliotangulia. Mapitio haya yatajenga uelewa wa mtafiti kujua au kufahamu taaluma iliyofikiwa kwenye eneo la utafiti wake. Hivyo, mtafiti anatakiwa kujiuliza ni kwa kiasi gani utafiti wake utaongeza taaluma katika eneo hilo.

Katika sehemu hii tumejadili kuhusu kazi tangulizi zinazohusiana na mada yetu ya utafiti ili kuona watafiti waliotangulia wametafiti nini kuhusiana na lengo ambalo sisi tumelikusudia katika utafiti huu. Kwa hiyo, sura hii imegawanyika katika vipengele vya dhana, chimbuko na dhima za nyimbo za kijamii. Pia, kuna watafiti tangulizi wa nyimbo, pengo la maarifa, nadharia za uchambuzi wa data, pamoja na hitimisho.

## 2.2 Dhana ya Nyimbo

Nyimbo ni mojawapo ya tanzu kongwe za fasihi simulizi. Baadhi yake, zimeandikwa, lakini idadi kubwa zaidi iko katika fasihi simulizi. Jambo la msingi ni kwamba, kila wimbo huwa na maana yake na hujihusisha na hali halisi ya maisha ya wanadamu (Nkwera, 2002). Kipekee, nyimbo ni mojawapo ya vyombo muhimu vya kijamii kwa kuwa ni sehemu ya mila na desturi za jamii zote hapa duniani.

Nyimbo ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalum iliyozingira kwa wakati huo, kwa mfano; furaha, hofu ama uchungu (Freuchen, 1962). Mtaalamu huyu anaendelea kueleza kwamba, binadamu anapokuwa na mawazo mengi hujikuta akijiwa na maneno yanayounda wimbo bila hiari yake. Mawazo hayo yanatolewa kwa njia isiyo ya mazungumzo ya kawaida na kuleta athari iliyokusudiwa. Ufafanuzi wa Freuchen umetoa mwelekeo unaotofautisha kati ya nyimbo na kazi nyingine za kifasihi. Vilevile mawazo haya yanatoa mchango mkubwa katika kazi yetu, kwamba ni kwa nini jamii ya Waasu iimbe nyimbo fulani katika sherehe za harusi, ni nguvu gani inayowasukuma kufanya hivyo?

Kwa upande mwingine, Wamitila (2004) anafasiri nyimbo kuwa ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka, huundwa na lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Anafafanua zaidi kwamba, nyimbo huchukua sehemu kubwa ya miviga (sherehe) ya jamii mbalimbali. Hoja ya nyimbo kuhusishwa na sherehe, Oates na Oneil (1991), Taphlin (2000) na Swift (2010) wakinukuliwa na Mutembei (2012) wanashadidia kwamba, jamii za Wayunani wa kale walikuwa na

sherehe zao kuanzia karne ya tano zilizoambatana na mivigha iliyoitwa ôDithirambuô na kwamba ziliambatana na nyimbo.

Hivyo, ni dhahiri nyimbo katika jamii ikiwemo jamii ya Waasu zina dhima kubwa sana katika maeneo mbalimbali ya maisha ya kila siku na zina historia kongwe sana. Mawazo ya Wamitla (2004 na Mutembei 2012) yana mashiko, kwamba kila sherehe lazima iambatane na nyimbo. Hoja hii imesaidia kusukuma utafiti wetu mbele kwa mantiki kwamba nyimbo ni mojawapo ya kitu cha lazima katika sherehe za kijamii ikiwemo harusi.

Kulingana na Maganga (1996), nyimbo ni ushairi ambao hutumia namna inayovuta hisia kutokana na mpangilio maalum wa maneno yaliyoteuliwa yenye kauli za mkato, picha na tamathali inayowasilishwa kwa hadhira. Pia, anaeleza kwamba, maneno yanayoimbwa yanafungamana na muktadha wa jamii iliyomkuza na kumlea msanii. Kwa mfano, nyimbo zinazoimbwa kwenye sherehe za harusi, jando na unyago na kampeni za kisiasa, zinaimbwa kwa kuzingatia muktadha wa sherehe zinazohusika. Maelezo haya yanasisitiza kwamba, nyimbo ni mawazo yanayoimbwa kutokana na msukumo wa nguvu maalum zinazotegemea sana muktadha wa uimbaji wake. Ni dhahiri hata katika sherehe za harusi za Waasu nyimbo huimbwa kwa kutegemea muktadha, hivyo mawazo ya mtaalamu huyu yamechangia kuaminika zaidi kwa utafiti wetu.

Kwa hiyo, wimbo ni mawazo yanayoimbwa na watu ambayo huvuta hisia kutokana na mpangilio maalum wa maneno yaliyoteuliwa; na ni kielezeo cha fikira zinazotolewa kutegemeana na muktadha wa uimbaji. Maneno na uimbaji ni mambo

mawili katika wimbo wowote. Sauti za ala na miondoko au kucheza vyaweza kuwepo au kukosekana, lakini wimbo ukabaki wimbo (Mulokozi, 1989). Kwa msingi huo, nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, mapigo, mwendo na muwala na zinaweza kuimbwa na kuchezwa muziki au bila muziki kwa kuzingatia muktadha wake wa uimbaji.

Ni dhahiri hata katika sherehe za harusi za Waasu, nyimbo za harusi huweza kuambatana na muziki kama vile ngoma au usiwepo. Hivyo mawazo ya mtaalamu huyu juu ya dhana ya nyimbo tunayakubali, yana mashiko na yamesaidia kutuongezea maarifa katika utafiti wetu.

## 2.3 Chimbuko la Nyimbo

Kulingana na Finnegan (1977), inasemekana kwamba nyimbo zilianza pale tu binadamu alipoanza kupambana dhidi ya mazingira yake. Kwa msingi huo, inachukuliwa kuwa sanaa ya uimbaji ilianza kupata mashiko katika jamii kati ya miaka 30,000 na 60,000 iliyopita. Wanaendelea kueleza kwamba, kipindi hicho kinakadiriwa kuwa ndipo binadamu walipoanza kuzika wafu. Kimsingi ufafanuzi wa Finnegan unayatazama mazingira ya binadamu kuwa ndio chimbuko la sanaa.

Kwa upande mwingine, fasihi ya mwanzo ilizuka baada ya kuzuka kwa lugha (Senkoro, 1988). Pia, anaeleza kwamba, inasemekana lugha ilitokana na kazi alizofanya mtu katika kupambana na mazingira yake. Hoja hii inapewa uzito na Nkwera (1978) kwamba, lugha ilianza kama njia ya mawasiliano na baadaye ikawa chombo cha kisanaa katika jamii ya wanadamu. Hali hiyo ilimfanya binadamu aanze kutunga maneno na sauti zilizofuata mapigo ya zana zake za kazi. Kimsingi tunakubaliana na mawazo ya wataalamu hawa, ni dhahiri nyimbo zikiwemo nyimbo

za harusi katika jamii ya Waasu zilianza zamani sana, mara tu baada ya kuzuka kwa lugha. Hivyo basi, mawazo ya wataalamu hawa yamesaidia kutuongezea maarifa katika utafiti wetu, kwa kusaidia kuangazia uzito wa nyimbo zikiwemo zile za harusi katika jamii, kwamba zimeanza zamani sana lakini hadi leo bado zipo.

Kimsingi, shughuli za binadamu na mazingira yake hutazamwa kama ndilo chimbuko la kazi za kisanaa (Jann, 1961). Kwa msingi huo, nyimbo zilikuwapo tangu kuwapo kwa binadamu ulimwenguni na zilijipambanua katika nyanja mbalimbali za kijamii kama vile fasihi, dini, utamaduni, historia, falsafa na sayansi. Mawazo ya mtaalamu huyu yana mashiko makubwa. Ni dhahiri kwamba nyimbo za kijamii zikiwemo nyimbo za harusi za Waasu zilianza zamani sana, na kwamba zinapokezwana kizazi hadi kizazi. Mawazo haya yalitusaidia sana katika kuunganisha na kuyapa uzito maarifa yetu juu ya nyimbo za harusi za Waasu, ambazo tangu kale zipo na kwa kiwango kikubwa hazijabadilika.

Senkoro (1988) anaeleza kwamba, fasihi simulizi ya kale kabisa ni wimbo wa kazi. Anasema pale tu binadamu alipopata urazini alianza kufanya kazi, na katika kufanya kazi aliimba nyimbo. Anaelezea madhumuni ya nyimbo hizo kwamba yalikuwa ni kumpunguzia machovu ya kazi. Hivyo, chimbuko la nyimbo katika jamii ni shughuli mbalimbali za kijamii kama vile kazi, na kwamba kadri siku zilivyoenda nyimbo zilipewa majukumu mengine katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile sherehe, zikiwa na dhima maalumu. Tunakubaliana na mawazo ya mtaalamu huyu, kwamba nyimbo zina dhima kubwa katika jamii na kwamba hutofautiana kutokana na shughuli husika. Aidha yametusaidia kutupa mwanzo mzuri wa utafiti wetu, kwa

kutueleza kwamba nyimbo za sherehe zina dhima mbalimbali na kwamba ni tofauti na nyimbo nyingine. Dhima hizo ndizo tumezichunguza katika sherehe za harusi za Waasu.

Naye, Wamitila (2004) anafafanua juu ya chimbuko la nyimbo. Anasema kwamba nyimbo zina historia ndefu katika jamii ya mwanadamu. Anaeleza kwamba nyimbo zilianza tu mara binadamu alipopata lugha na kuweza kuzieleza hisia zake. Hoja hii inadhihirisha kwamba nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu kama zilivyo jamii nyinginezo zimekuwepo tangu zamani. Hata hivyo mtaalamu huyu haelezi ni lini hasa nyimbo za sherehe katika jamii zilianza. Kimsingi ni kwamba wimbo wa awali kabisa ulikuwa ówimbo wa kaziô na nyimbo nyingine kama vile za sherehe zilifuata baadaye kulingana na maendeleo mbalimbali ya binadamu na ya jamii husika.

Kwa ujumla, hapana shaka kwamba nyimbo ni utungo wa zamani kabisa katika taaluma ya fasihi simulizi ambao ulitumiwa na wanajamii kwa madhumuni mbalimbali katika kila jamii inayohusika. Kipekee, chimbuko la nyimbo haliwezi kutenganishwa na muktadha wa historia ya jamii iliyomkuza na kumlea mtunzi wa wimbo unaohusika (Okpewho, 1990). Hoja hii tunaikubali, hii ni kwa kuwa mazingira ni malighafi ya kazi yoyote ya kifasihi. Kimsingi ufafanuzi huu ulitusaidia katika kuchunguza dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu zilizolengwa katika utafiti huu, hivyo kutusaidia kuongeza maarifa katika mada yetu ya utafiti.

## 2.4 Dhima za Nyimbo kwa Ujumla

Nyimbo hutumika kama hazina ya kutunza historia na maendeleo ya jamii kwa kuwa katika jamii ambazo hazikuwa na maandishi hadi karne kadhaa tu zilizopita, nyimbo

ndizo zilizokuwa zinatumika kama vitabu na magazeti ya wanajamii (Njogu na Chimerah, 1999). Pia, mambo yahusuyo taaluma zote za mwanadamu yalikuwa yakihifadhiwa katika nyimbo. Kwa hiyo, tunaweza kuyajua mambo yanayotendeka na yanayowaathiri watu wa jamii fulani kupitia nyimbo za jamii inayohusika. Maelezo haya yalipewa uzito katika uchunguzi wa dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu, ambapo uchambuzi wa nyimbo nyingi unaonesha kutunza na kudumisha historia ya Waasu katika maeneo mbalimbali.

Aidha, nyimbo ni tiba kwa binadamu kwa sababu zinaweza kupunguza maradhi na kuondoa msongo wa mawazo unaotokana na uchungu wa matatizo ya kimaisha kwa kuwa zinamwezesha binadamu kuzitakasa hisia zake zinazoambatana na chuki ama huzuni (McNiff, 1992). Mtaalamu huyu anazidi kueleza kwamba, nyimbo ni mbinu mojawapo ya vyombo vya kueleza hisia na maono; na ni namna pekee ya kujieleza ambayo kila mtu huweza kuitumia wakati wowote bila gharama yoyote. Kwa mtazamo huo, nyimbo ni tiba muhimu ambayo kila mtu anaweza kuimudu kwa urahisi. Ni dhahiri kwamba nyimbo ni njia nzuri zaidi ya kueleza hisia, na kwamba hisia zielezwazo kwa njia hii huwa na athari kubwa. Mawazo ya mtaalamu huyu ni sahihi, na yametusaidia kuongeza maarifa juu ya mada yetu ya utafiti. Hisia nyingi, kwa mfano, uchungu wa mama kwa bintiye huelezewa kupitia nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu.

Kwa upande mwingine, McGilhrist (1982) anafafanua kwamba, nyimbo ni chombo kilichovuka mipaka ya kuburudisha kwa kuwa hutumika kama zana ya kuongeza siku za kuishi. Hii ni kwa sababu nyimbo ni chombo kinachotumika kutolea hisia na mihemuko inayomsibu binadamu. Hata hivyo, Senkoro (1988) anaongeza kwamba,

wasanii wanatumia nyimbo ili kueleza matatizo yao, fikra zao na  matarajio yao, na pia ni sehemu ya ajira yao. Mtazamo huo umo katika muziki wa kizazi kipya, ambapo vijana wamejiingiza katika mkondo huo ili kujipatia riziki zao. Hata hivyo, nyimbo zao zimejengewa msingi katika kuakisi matokeo na changamoto za binadamu katika kuutambua ukweli wa maisha. Mawazo ya wataalamu hawa yametusaidia kuwa na uelewa zaidi, kwamba nyimbo zina dhima nyingi sana na hutumika kutolea hisia. Hata hivyo, wao yamejikita katika nyimbo kwa ujumla. Kimsingi, dhima za nyimbo hutofautiana kutokana na aina zake.. Katika utafiti wetu tulijikita katika nyimbo za harusi pekee za jamii ya Waasu.

Naye, Luhanga (1988) anaeleza kwamba, nyimbo ni chombo cha jamii kinachohakiki tabia za watu na chenye uwezo wa kutoa mwelekeo na kuirekebisha jamii juu ya maisha yao, pamoja na kuweza kuyatambua na kuyatawala kwa urahisi. Pia, anaeleza kwamba, nyimbo zina maudhui ambayo huonesha maisha yaliyomo katika jamii; na ni chombo muhimu katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Hivyo, wanafasihi wanatumia nyimbo katika kulinda na kuendeleza falsafa na maadili ya jamii, pamoja na kuifanya jamii kuyatambua mazingira na harakati zake za kila siku. Kimsingi mawazo ya Luhanga (1988) yana mashiko makubwa na tunayakubali. Kwa mujibu wa data yetu, zipo nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zinazohakiki tabia zisizofaa kwa nia ya kuzirekebisha. Hoja katika nyimbo kama hizi zimepewa nguvu na mawazo ya mtaalamu huyu.

Nyimbo ni chombo cha mahusiano kinachoeleza na kufafanua shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi (Ngure, 2010). Pia, anaeleza kwamba, shughuli zote za furaha na

zile za huzuni katika jamii za Kiafrika lazima ziambatane na nyimbo; na kwamba, nyimbo ni utanzu maarufu kwa kuwa ni shughuli chache zisizoambatana nazo. Kwa mfano, anasema, hebu tufikiri, hali ingekuwaje bila nyimbo katika sherehe, kuabudu, harusi, jando na unyago? Kwa hiyo, nyimbo ni chombo thabiti kinachohakiki shughuli zifanywazo na jamii kwa kuzingatia muktadha na viashiria vya ujitokezaji wa mambo kwa kuzingatia mahitaji ya jamii kisanaa na kiwakati. Mawazo ya mtaalamu huyu tunayakubali, na yalitusaidia kuanzia hatua za awali za utafiti huu, kwa kutueleza kwamba sherehe zote za kijamii huambatana na nyimbo kwa kuzingatia muktadha. Hivyo basi, hata katika sherehe za harusi za jamii ya Waasu nyimbo ni jambo la lazima, huimbwa kwa kuzingatia muktadha na tukio husika.

Kwa upande wake Mulokozi (1996), nyimbo katika jamii yoyote ile zina dhima kubwa sana katika; kuendeleza, kudumisha, na kuhifadhi mila na desturi za jamii. Anatoa mfano wa nyimbo za jando na unyago kuwa wajibu wake ni kufunza na kuadili vijana kwa ajili ya kuandaliwa kuingia katika utu uzima. Anazidi kueleza dhima nyingine za nyimbo kuwa ni kuchapusha kazi, kuonya jamii na kusisitiza suala la umoja na mshikamano katika jamii. Hoja hii inasaidia katika kusukuma utafiti wetu mbele, kwani jamii ya Waasu ni mojawapo ya jamii anazozibainisha mataalamu huyu. Aidha, nyimbo zake kwa mfano zile zenye dhima ya kuheshimu wazazi hunuia kuendeleza utamaduni wa heshima katika jamii. Hivyo uchambuzi wa data yetu ulichangiwa kupewa nguvu na hoja ya mtaalamu huyu.

Kwa hiyo, nyimbo ni kipera muhimu inayotumika kama dira na mwelekeo wa maisha ya kila siku; na zimejengwa katika uwanja mpana wa kuendeleza falsafa, maadili na kurithisha mila na desturi za jamii kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa

kawaida, nyimbo hujengwa katika misingi ya kijadi yenye wajibu wa kuilewa jamii katika nyanja zake zote kwa kuzingatia mila na desturi zinazohusika. Katika utafiti huu, nyimbo za harusi za jamii ya Waasu zimepewa uzito wa kiutafiti katika uchunguzi wa dhima zake.

## 2.5 Tafiti Tangulizi Kuhusu Nyimbo

Mutembei (2012) akiwanukuu Oates na Oneil (1991), Taphlin (2000) na Swift (2010) anaeleza kwamba, nyimbo ni kipengele muhimu sana katika sherehe mbalimbali za kijamii. Pia, anaelezea kwamba, kuanzia karne ya tano hadi ya nane jamii ya Wayunani ilikuwa inatumia nyimbo katika sherehe za miviga iliyoitwa ôDithirambuô. Kwa msingi huo, nyimbo zilikuwa sehemu ya miviga hiyo kwa mungu wao aliyeitwa Dionizi; na kwamba, nyimbo hizo ziliimbwa na wanawake huku wanaume wakiendelea kutambika. Mawazo ya Mutembei (kesht.) yamesaidia kutubainishia nyimbo zipi huibwa na watu au jinsia gani. Katika jamii ya Waasu kwa mujibu wa data yetu nyimbo nyingi za harusi huimbwa na wanawake. Kwa hakika mawazo haya yalitupa maarifa zaidi katika utafiti wetu kwa kutuwezesha kuhusianisha nyimbo za harusi na dhima zake katika Jamii ya Waasu.

Mbogo (2008) alichunguza kipengele cha mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za harusi za Waembu nchini Kenya. Anaeleza kwamba nyimbo hizo hubadilika, mabadiliko hayo hutokana na maendeleo ya jamii kama vile uchumi, siasa, sayansi na teknolojia na miingilio ya utamaduni wa jamii za ndani na nje ya nchi. Anaeleza maudhui ya nyimbo za Waembu baada ya Ukoloni yana dhima ya; maadili mema katika misingi ya dini, usawa wa kijinsia na thamani ya uchumi wa pesa katika jamii. Pia, nyimbo hizo huisaidia jamii kwenda na wakati, pamoja na kupambana na

harakati mbalimbali za kijamii, yakiwamo magonjwa hasa UKIMWI, uchafuzi wa mazingira, na mabadiliko ya kisiasa. Utafiti wa mtaalamu huyu unaupa nguvu utafiti wetu kwa kuonesha kwamba dhima za nyimbo za harusi ni taasisi imara ya maadili kwa kila jamii. Hata hivyo mtaalamu huyu aliendа mbali kwa kuangazia mabadiliko ya nyimbo za harusi katika jamii yake. Utafiti wetu haukujikita huko, bali kuchunguza dhima na usanaa wa nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu.

Pembe (2013) yeye alichunguza nyimbo za ngoma ya Msewe kutoka Zanzibar. Pembe anaeleza kwamba, nyimbo hizo zina dhima mbalimbali kama vile kuwafunza wanawake jinsi ya kuwa wake bora katika ndoa zao, pamoja na namna ya kumudu majukumu yao kulingana na mazingira, mila na desturi zao. Aidha, anaendelea kueleza zaidi kwamba nyimbo hizo zimepata mabadiliko ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Hoja ya mtaalamu huyu huthibitisha kwamba, nyimbo kama kipengele cha fasihi simulizi si tuli, bali huweza kupata mabadiliko kutokana na mabadiliko ya kijamii. Mabadiliko hayo huakisi dhima mpya kulingana na wakati. Tunakubaliana na mawazo ya mtaalamu huyu. Aidha mawazo yake yametusaidia katika kazi yetu kwa kutuonesha kwamba suala la dhima la nyimbo za harusi lipo kwa kila jamii. Hivyo mawazo hayo yameipa kazi yetu nguvu ya kitaaluma. Hata hivyo sisi hatukuangazia mabadiliko ya nyimbo tulizozichunguza.

Naye Kauti (2013) alichunguza mabadiliko ya dhamira katika nyimbo za mwanamke wa Kiyao. Kimsingi, anaonesha kuwapo kwa tofauti kubwa katika dhamira za nyimbo za Kiyao kutokana na mabadiliko ya kimwili ayapatayo mwanamke. Anafafanua kwamba, kila hatua ya mabadiliko ya mwanamke nyimbo zake hubadilika kutokana na hatua inayohusika. Kwa mfano, kutoka kuvunja ungo, ndoa

na ujauzito, na kadhalika. Aidha, anaelezea athari za nyimbo za makuzi ya mwanamke katika jamii ya Kiyao kuwa ni kutukuzwa kwa mwanaume, mwanamke kuandaliwa tangu mwanzo kuwa kiumbe cha kuendeleza uzazi kwa kuzaa, kulea na kuwa tegemezi kwa mwanaume. Kwa upande mwingine, anaelezea kuwa, athari chanya za nyimbo hizo ni kuimarisha malezi ya mwanamke na kutoa elimu ya uzazi. Kazi ya mtaalamu huyu alitusaidia kuangazia muktadha unavyoleta utofauti wa nyimbo. Kwa kuzingatia mawazo haya tuliweza kubaini kwamba nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu hutofautiana hapa na pale kufuatana na muktadha na tukio.

Aidha, Abdulla (2016) baada ya kuchunguza athari za kiitikadi katika nyimbo za harusi za Zanzibar, aliziainisha nyimbo hizo katika makundi mbalimbali, zikiwamo za kumtoa bibi harusi nje. Pia, Mulokozi (1996) anaeleza kwamba, nyimbo za harusi zimebeba maudhui tofauti tofauti, na kwamba, kila wimbo huimbwa katika tukio fulani kutegemeana na maudhui yake yaliyolengwa kufikia watu. Mulokozi (ksht.) anashabihina na Mlambia (2017), yeye alichunguza nyimbo za asili za watoto za jamii ya Wahehe. Anaeleza kwamba, nyimbo hizo zina dhima mbalimbali kama vile kuhamasisha maadili mema, kuionya jamii, kudumisha heshima na kuagana na wazazi wakati wa kwenda kulala. Pia zinatunza mila na desturi za jamii yao.

Mawazo ya Abdulla (2016) yalitusaidia katika hatua za awali za utafiti wetu, kuziweka nyimbo za harusi za Waasu katika makundi anuai. Aidha, Mlambia (2017) na Mulokozi (1996) mawazo yao yalituongoza katika kuangaza dhima ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Hivyo basi, mawazo ya wataalamu hawa yana mashiko makubwa.

Waziri (2016) yeye alichunguza dhima ya nyimbo za *singo* katika kijiji cha Uzini Zanzibar. Anaelezea kwamba, singo ni sherehe muhimu sana inayofanywa ndani ya jamii ya Waswahili hasa katika visiwa vya Unguja na Pemba. Huelezea dhima ya nyimbo hizi kuwa ni pamoja na; kumfunza mwanamke mambo ya kufanya ili ndoa idumu, kwa kuweka mbinu anuai kwa mfano kutandika kitanda vizuri, kushirikiana katika ndoa, wanandoa kuwa makini katika ndoa yao nakadhalika. Ufafanuzi huo unadhihirisha kwamba, nyimbo huimbwa kulingana na muktadha wa jamii inayohusika na zina dhima kuntu. Maelezo haya yana msaada katika utafiti wetu kwani kila jamii ya binadamu ina miongozo ya kimaadili inayofanana kwa kiasi kikubwa.

Ndungo na Wafula (1993) wamehakiki taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi ya Kiafrika kwa kuzingatia methali katika jamii za wakikuyu na Waswahili. Katika utafiti huo dhamira mbalimbali zimeshughulikiwa ikiwamo inayohusu taswira ya mwanamake katika fasihi simulizi. Utafiti wa wataalamu hawa umesaidia kutupa uelewa zaidi katika mada yetu ya utafiti, kwani nao wameangaza dhamira mbalimbali katika fasihi simulizi kipengele cha methali kwa kumwangazia mwanamke, ambaye hata katika nyimbo za harusi za Waasu ndiye anayeongelewa zaidi. Hata hivyo, utafiti huu kwa upande wake umeshughulikia dhima za nyimbo za harusi katika jamii wa Waasu.

Kimsingi, suala la nyimbo za kijamii na fasihi simulizi kwa ujumla limeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali kwa namna tofauti tofauti kutokana na misukumo na mitazamo yao. Baadhi ya watafiti na wachambuzi huzitazama nyimbo hizo kama taasisi pana yenye tanzu nyingi ndani yake. Hali hii inatokana na kuwapo

mitindo mbalimbali ya uimbaji na uwasilishaji inayotumika kama kigezo kimojawapo cha uainishaji wa nyimbo za kijamii. Nyimbo za harusi za jamii ya Waasu ni miongoni mwa utanzu uliopewa msisitizo mdogo kiuchunguzi na kiuchambuzi. Kwa msingi huo, nyimbo zake zimeteuliwa na kutumika katika utafiti huu ili kuongeza maarifa ya nyimbo hizi kiuchunguzi. Vilevile ili kuangazia umahususi wa dhima za nyimbo hizi katika jamii ya Waasu pamoja na usanaa wa lugha utumikao katika ujenzi wake.

## 2.6 Pengo la Utafiti

Kupitia mapitio ya wataalmu mbalimbli kama vile Wamitila (2004), Mbogo (2008), Mulokozi (2011), na Pembe (2013), ni dhahiri kuwa wamefanya uchunguzi kuhusu nyimbo za kijamii katika vipengele vya fani na maudhui yake kwa misukumo na mitazamo tofauti tofauti. Hata hivyo, uchunguzi kuhusu usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu waishio katika wilaya ya Same mkoa wa Kilimanjaro, kwa kadri ya ufahamu wetu, bado haujafanyika. Utafiti huu ulikusudia kuziba pengo hilo la maarifa kwa kuchunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi za jamii ya Waasu wanaoishi katika wilaya ya Same.

## 2.7 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia kama zilivyo amali nyingine za kijamii ni zao la utamaduni na historia ya jamii inayohusika. Kulingana na Sengo (2009), nadharia ni mwongozo unaosaidia kupata ukweli na kuthibitisha jambo kwa lengo maalumu. Kwa kawaida, nadharia hufungamana na masuala ya kihistoria yaliyoizalisha kazi inayohusika. Hali hiyo, huzifanya nadharia kutazamwa kama mwongozo unaosaidia kutoa maelezo juu ya

namna jambo fulani linavyopaswa kufanyika ili kutoa matokeo yasiyoweza kutiwa shaka ya kitaaluma. Nadharia ni sehemu mahsusi ya hali halisi iliyopo katika jamii; na baadhi yake zinaweza kutumiwa katika miktadha tofauti tofauti.

Uchambuzi na mjadala wa data katika tasinifu hii uliongozwa na nadharia za Uhalisia na Semiotiki. Nadharia hizo ziliteuliwa kwa kuwa uchambuzi na mjadala wa data uliwekewa mkazo katika uchunguzi wa vipengele vya dhima na lugha katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Nadharia hizi zilikuwa muafaka katika uchunguzi na mjadala wa vipengele vilivyolengwa. Uteuzi wa nadharia hizi ulizingatia misingi ya kutegemeana na kukamilishana kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti.

### 2.7.1 Nadharia ya Uhalisia

Nadharia ya Uhalisia iliasisiwa nchini Ufaransa mnamo karne ya kumi na tisa (19) kwa ajili ya kupinga matamanio ya Kilimbwende yaliyokuwa ya kinjonzi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu (Snow, 1968). Nadharia hii inaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Katika upana wake, uhalisia humaanisha uwakilishi wa hali na uhalisi wa mambo ya kijamii yanavyojidhihirisha katika fasihi. Uhalisia unaelezea namna kazi ya fasihi inavyouwakilisha ulimwengu wa maisha ya jamii na hali halisi iliyomo (Moore, 1976).

Nadharia ya Uhalisia inaonesha uwezo wa wazi wazi wa kusawiri hali za kijamii kwa kuzingatia uyakinifu wa mazingira yanayomzunguka binadamu, ambayo ndiyo dira inayomwongoza mtu katika uteuzi wa mada ya kuongea na msamiati unaopaswa

kutumika (Fried, 1987). Uhalisia wa muktadha wa kazi ya fasihi umejikita katika kweli zote ziihusuyo kazi hiyo. Aidha, uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, matukio mahsusi, na matokeo yanaweza kuthibitika. Wafula na Njogu (2007) wanashadidia hoja hii kuwa uhalisia hutumiwa kama njia ya kutathmini hali halisi ya maisha katika jamii.

Spurlin & Fischer (1985) wanaeleza kwamba, uhalisi wa maisha katika jamii huelezwa jinsi ulivyo katika fasihi; na unaichukulia fasihi kama zao halisi la jamii. Nadharia hii humaanisha uwakilishi wa hali na uhalisi wa mambo katika fasihi, ambapo, mhalisia huamini kuwa katika matokeo ya mambo, na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana katika mambo yaliyopo na yanayoweza kuthibitika na kuthibitishwa kwa tajiriba.

Kwa mujibu wa nadharia hii, mhalisia anapaswa kuchunguza kwa undani na kuendeleza masuala yake, na ya kijamii kama yalivyo na yanavyowahusu watu katika hali halisi za maisha ya kila siku. Mtazamo huu wa uhalisia unaiangalia jamii na mazingira yake kama kiungo thabiti katika usanifu wa kazi za kifasihi, na inapaswa kuwaweka wanajamii katika dunia yao ya kawaida na hali halisi. Hivyo, kazi ya kifasihi inatakiwa kuwa wazi bila kupiga chuku kwa kuyasawiri matukio katika fasihi kama yalivyo maisha ya kila siku. Kwa ufupi, uelewa wa maisha na mazingira ya jamii yanayotazamwa na msanii ni nyenzo sahihi kwa mhakiki wa kihalisia.

Mtafiti anayeitumia nadharia hii kuchunguza kwa kina namna msanii anavyouonesha wazi wazi uhalisia wa masuala au matukio ya kijamii kupitia kazi za kisanaa. Mtafiti

huchunguza namna uyakinifu unavyojipambanua katika harakati za msanii za kueleza hali halisi ya masuala ya kijamii katika wakati muhsusi. Kwa mujibu wa nadharia hii, msanii hana budi kusawiri mandhari, wahusika na masuala ya kijamii yanayoaminika na kukubalika katika jamii ya wakati wake, kama Sengo (2009) anavyoeleza kuwa, ili mtu aielewe fasihi fulani, sharti ajue eneo linalohusika na utamaduni wao, mila, lugha na mazingira yao.

Kwa hiyo, uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya shughuli za kijamii, mazingira na fasihi, ndiyo msingi wa nadharia ya Uhalisia. Aidha, waimbaji wa nyimbo za harusi za jamii ya Waasu walitazamwa kama sehemu kamili ya jamii yao kwa kuzingatia mazingira ya uimbaji wao. Uhusiano uliopo kati ya jamii ya Waasu na nyimbo zao za harusi ndio unaoyachukua masuala yaliyomo katika jamii na kuyaweka kama yalivyo katika nyimbo zao. Tuliitumia nadharia hii katika uchambuzi wa lengo letu la kwanza katika utafiti wetu.

Kwa hiyo, mtafiti alizitalii nyimbo za harusi za jamii ya Waasu na kuzikita katika msingi uliosaidia katika uchambuzi wa data zilizokuwa zinahitajika. Aidha, mtafiti aliwaweka Waasu katika ulimwengu wao wa kawaida, kweli na halisi ili kufanya uchambuzi wa kina. Waimbaji wa nyimbo za harusi za jamii ya Waasu walitazamwa kwa undani jinsi walivyoyachunguza masuala ya kijamii na kuyaweka kama yalivyo na yanavyoaminika na kukubalika kupitia nyimbo zao. Nyimbo za harusi za Waasu zilitazamwa kwa kuzingatia masuala halisi moja kwa moja bila chuku ili kuweza kufanya uhakiki wa kina. Kipekee, tulizisikiliza na kuzichambua nyimbo

zilizoteuliwa na kupata maana zake kwa kuzingatia historia, utamaduni na muktadha wa uimbaji wake.

### 2.7.2 Nadharia ya Simiotiki

Nadharia ya simiotiki imeasisiwa na Ferdinand de Saussure na Charles Pierce miaka ya 1970. óSimiotikiô ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara. Kimsingi nadharia hii hushughulika na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi. Charles Pierce anaihusisha nadharia ya simiotiki na kielelezo cha pembe tatu; yambwa (kitu), ishara, na kifasiri. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu kila ishara huwa na yambwa au kitendwa kinachorejelewa. Kifasiri ni kile kinachochochewa katika akili ya anayefasiri ishara hiyo (Wamitila, 2002).

Semiotiki ni nadharia inayoshughulika na ishara pamoja na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Kulingana na Cameron (1985), ishara zinazojitokeza katika fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii na binadamu ndiye mtengenezaji wa alama mbalimbali za ishara ambazo huzitumia katika mawasiliano yake ya kila siku. Semiotiki ni taaluma ya mfumo wa alama katika mawasiliano ya kutumia lugha (Eco, 1976). Hadhira inayolengwa hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama na ishara inazokutana nazo katika kazi za kifasihi inazozisikiliza au kuzisoma.

Katika taaluma ya lugha kuna vitu viwili ambavyo ndivyo husaidia mawasiliano, yaani kiashiria na kiashiriwa (De Saussure, 1966). Kiashiria ni alama, sauti au herufi zinazotumika kutaja jina la kitu fulani. Kiashiriwa ni kitu halisi kinachorejelewa na alama, sauti au herufi zinazotaja kitu hicho. Kwa mfano, neno ópaaô ni kitaja

ambacho hurejelea vitajwa mbalimbali kama vile, paa, yaani ómnyama wa porini aliyefanana na mbuziô na ósehemu ya juu inayofunika nyumbaô. Neno ópaaô linarejelea vitu viwili tofauti. Jambo hili linathibitisha kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kitaja na kitajwa. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kitajwa, isipokuwa kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake.

Senyamanza (2015) aliitumia nadharia hii katika uchunguzi wa mabadiliko ya *rara* katika jamii za mkoani Mbeya. Senyamanza alizitazama ishara kama dhana zinazorejelea matukio yaliyobainishwa katika nyimbo hizo kwa kuzingatia muktadha na utamaduni wa jamii zilizochunguzwa. Uchunguzi huo ulimpa fursa mtafiti kukitazama kila kipengele kilichotumika katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu kuwa ni ishara inayowakilisha dhana maalumu katika muktadha wa jamii hiyo. Kulingana na Hawkes (1977), matumizi ya baadhi ya mbinu za kifani na kimaudhui katika kazi za fasihi kuwa si ya kibahati nasibu bali yana maana katika kazi zinazochunguzwa.

Barthes (1994) kama alivyonukuliwa na Wamitila (2002:134) anabainisha misimbo mitano ya simiotiki inayotumika katika uchambuzi wa kazi za kifasihi kwamba ni msimbo wa; kihemenitiki, kimatukio, kiseme, ki-ishara na kirejelezi. Matumizi ya misimbo hii hutegemea lengo, mada na tanzu anayoitafitia mtafiti. Katika utafiti wetu tumetumia misimbo minne ambayo ni; Msimbo wa kiseme, ki-ishara, kihementiki na wa kiurejelezi. Hii ni kutokana na mada, utanzu na lengo letu la utafiti, kama anavyobainisha Wamitila (kesht.). Hivyo basi, msimbo wa kimatukio hatujautumia kwa sababu hauna uhusiano wa moja kwa moja na utafiti wetu.

Wamitila (2002:134) anaeleza zaidi kwamba msimbo wa kimatukio huangaza jinsi matukio yanavyoungana na kushonana kutokana na usababisho. Aidha Omary (2011) anasema matukio hujitokeza zaidi katika riwaya na tamthilia kuliko ushairi.

Msimbo wa kihemenitiki huhusishwa sana na anuani ya kifasihi. Anuani ya kifasihi inaweza kuwa ni jina au kichwa cha shairi/wimbo  ama kichwa cha habari. Hivyo basi, kwa mujibu wa maelezo haya vichwa vya habari katika nyimbo mbalimbali za harusi za jamii ya Waasu, zimebeba msimbo wa kihemenitiki, kwa mfano wimbo wa *mama chunga idafa* (mama jikaze/funga mkanda). Kutokana na vichwa hivyo msikilizaji atajiuliza maswali mengi kama vile; kwa nini? Ili iweje? Nakadhalika. Majibu ya maswali haya yanapatikana baada ya msikilizaji kusikiliza wimbo wote na kuutafakari kufuatana na muktadha. Hivyo basi, msimbo wa kihemenitiki humfikirisha msikilizaji juu ya kile anachokisikia na kukitafitia.  Katika utafiti wetu tumeongozwa na msimbo huu katika kubainisha usanaa wa lugha uliotumika katika ujenzi wa nyimbo za harusi za Waasu, kwa kuanzia na vichwa vyake vya habari na wimbo mzima kwa jumla yake.

Msimbo wa kiseme, msimbo huu kwa asili unatokana na neno sema. Wamitila (2002 :134) anasema neno sema hutumiwa kuielezea elementi nasibishi ya kisemantiki. Hii ina maana kutokana na viashiria mbalimbali tunaweza kuelewa kuwa mhusika fulani ana sifa zipi?

Kwa mfano tukirejelea wimbo wa *Hiyo Pete Yetu Naitoke* ambao ni mojawapo ya nyimbo za harusi unaoimbwa katika harusi za Waasu tunapata picha kwamba *pete* ni msichana mzuri, mrembo na anayependeza, na pia mwenye thamani. Aidha sifa zote

hizi hutokana na unasibishaji wa mtu fulani na sifa za kitu fulani. Kwa mantiki hii, msimbo wa kiseme unaweka mchango mkubwa katika kuiongoza kazi yetu. Katika utafiti wetu msimbo huu umetuongoza katika kufanya unasibishaji wa maeneo mbalimbali, kwa mfano watu, vitu na matukio.

Msimbo wa ki-ishara, msimbo huu unahusiana na jinsi ambavyo wasikilizaji au wasomaji wa kazi ya kifasihi wanavyoweza kubaini maana mbalimbali baada ya kufumbua ishara husika. Kwa mfano katika utafiti wetu wimbo *Wifi unatete mphoa* (Wifi uwe na upendo) katika wimbo huu kuna ishara mbalimbali kwa mfano *kajoto* (moto), pia wimbo wa *mama chunga idafa* (mama jikaze/jifunge mkanda). Maneno kama vile *chunga idafa* (funga mkanda) ni ya ki-ishara. Ili msikilizaji aweze kuelewa maana katika nyimbo hizi ni lazima afikirie na kuzielewa ishara husika. Msimbo huu wa simiotiki ulituongoza katika kubainisha dhana na maneno yaliyotumika ki-ishara na kuweza kuyatafsiri katika uchambuzi wetu.

Msimbo wa kiurejelezi, huu umejikita katika viashiria vya utamaduni wa jamii unaorejelewa katika kazi husika. Urejelezi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya dhana au vitu fulani vinavyoeleweka kwa hadhira ya kazi husika ya mwanafasihi kwa kuzingatia utamaduni wake (Wamitila 2002). Katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu, wimbo kama vile *Kasanga kavo kahuyuka* (kijijini kwao kumepwaya) unaposikiliza unakutana na maneno kama vile ; *makoko* (maboga) *viagho* (sangare) vitu hivi ni vya kiutamaduni katika jamii hii.

Kwa mfano *makoko* ni mojawapo ya chakula cha kiutamaduni na *viagho* ni mojawapo ya majani maarufu yaotayo katika ardhi isiyo na rutuba na huwa ni

magumu kuyalima. Maneno kama haya mara wimbo husika uimbwapo msikilizaji hujenga picha fulani kwa kuyahusianisha na utamaduni wa jamii yake. Msimbo huu tumeutumika katika utafiti wetu kwa kuzingatia kwamba, kuna maneno mengi katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu yaliyotumika kiurejelezi. Hivyo basi, kwa kuongozwa na msimbo huu tuliweza kuyafafanua kwa kuzingatia utamaduni wa jamii hii. Misimbo hii minne tumeitumia kwa ujumuifu wake katika utafiti wetu.

Kwa hiyo, nadharia za Uhalisia na Simiotiki zilitumika kama nguzo imara katika uchunguzi wa mambo yanayowazunguka waimbaji wa nyimbo za harusi za Waasu kwa kuzingatia utamaduni na muktadha wa uimbaji wao. Eneo la utafiti lilipewa uzito ili kuonesha muktadha wa kijamii ulivyofungamana na dhima za nyimbo za harusi zilizolengwa kuchunguzwa. Aidha, mazingira ya uimbaji ya kijamii yaliwekwa wazi ili kuona namna yalivyodhibiti utunzi na uimbaji wa nyimbo za harusi za jamii ya Waasu.

## 2.8 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti wetu ili kupata maoni na maarifa kutoka kwa watafiti waliotangulia. Hali hiyo, imetuongezea maarifa katika mada iliyoshughulikiwa. Baadhi ya vipengele vilivyochunguzwa katika sura hii ni dhana ya nyimbo, chimbuko la nyimbo, dhima za nyimbo, pamoja na tafiti tangulizi zilizofanywa na watafiti wengine zinazohusiana na mada yetu ya utafiti . Pia, nadharia za Simiotiki na Uhalisia zilizoongoza mjadala wa data yetu zimejadiliwa katika sura hii. Nadharia hizo zilikuwa muafaka katika kufikia malengo mahsusi ya tasinifu hii. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Mbinu za utafiti ni jumla ya taratibu zote zinazotakiwa kufuatwa katika kazi ya utafiti. Mbinu za utafiti ni hatua za msingi za mtafiti ambazo huzitumia katika kazi yake ya utafiti, na hasa namna atakavyokusanya data, kuzichambua na kuziandikia taarifa ya utafiti (Bailey, 1994). Mbinu za utafiti humsaidia mtafiti akubalike katika jamii na kupewa taarifa bila ya hofu. Baadhi ya mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni uteuzi wa eneo la utafiti, usanifu wa utafiti na sampuli ya utafiti. Pia, kuna mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data na itikeli ya utafiti. Kwa hiyo, mbinu za utafiti zilimuongoza mtafiti katika ukusanyaji wa data zinazomwezesha kufikia malengo ya utafiti wake.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti huelezwa kuwa ni mahali ambapo data za utafiti zilikusanywa na pengine zilichambuliwa (Kothari, 2008). Eneo la utafiti huteuliwa kulingana na lengo kuu la utafiti. Utafiti huu umefanyika mkoani Kilimanjaro katika wilaya ya Same, kata ya Mhezi; vijiji vya Mhezi na Mtunguja, kata ya Mshewa; kijiji cha Kwizu; na kata ya Same Mjini; mtaa wa Stesheni na mtaa wa Mjini. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa kuwa yalikuwa na mawanda ya kutosha kupata data zilizolengwa kukidhi mahitaji ya utafiti huu. Aidha tulichagua maeneo mengi ya vijijini kwa sababu ndiko hasa utamaduni wa jamii zikiwemo nyimbo za harusi za Waasu vimetamalaki zaidi. Eneo la Same mjini liliteuliwa kwa sababu kwa uzoefu wetu, sherehe za harusi katika eneo hili hufanyika mara kwa mara ukilinganisha na maeneo

ya vijijini. Hivyo tulikuwa na uhakika wa kukuta sherehe za harusi kwa ajili ya data yetu.

### 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpango mahsusi unaobainisha mtiririko wa upatikanaji wa data zinazohitajika. Kulingana na Kothari (2008), usanifu wa utafiti ni mpangilio unaoonesha sura nzima ya utafiti unavyopaswa kufanyika kuanzia katika hatua ya ukusanyaji wa data mpaka hatua za uandishi wa ripoti. Pia, hutoa picha kamili inayoonesha jinsi utafiti utakavyofanyika tangu unapoanza mpaka hatua za uandishi wa ripoti. Usanifu wa utafiti huonesha vipengele muhimu vitakavyoshughulikiwa katika utafiti unaohusika, ambavyo ndio picha kamili ya utafiti huo.

Vipengele hivyo ni kama vile; malengo ya utafiti, njia za utafiti, mbinu za utafiti na sampuli na usampulishaji. Vipengele vingine ni mbinu za uchakataji wa matokeo na matokeo ya utafiti. Katika tasinifu hii mbinu ya uchunguzi kifani imetumika. Uchunguzi kifani ni utaratibu maalumu unaomwezesha mtafiti kuteua jambo mahsusi ambalo atalishughulikia katika utafiti wake (Troachim, 2006).

Uchunguzi kifani katika tasinifu hii ni nyimbo za harusi za jamii ya Waasu, ambapo jumla ya nyimbo 30 ziliteuliwa. Mbinu hii ilimruhusu na kumpa uhuru mtafiti kuteua na kuchunguza dhima na kipengele cha usanaa wa lugha kwa undani. Pia, ilimwongoza kupata data za msingi katika nyimbo na vipengele vilivyolengwa. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data za kutosha zilizowezesha kukamilisha utafiti wake.

3.4 Aina ya Utafiti

Utafiti huu ni wa maskanini na maktabanini. Data za msingi zilikusanywa mkoani Kilimanjaro, katika wilaya ya Same. Kata ya Mhezi; vijiji vya Mhezi na Mtunguja, kata ya Mshewa; kijiji cha Kwizu; na kata ya Same Mjini; mtaa wa Stesheni na mtaa wa Mjini. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa kuwa yalikuwa na mawanda ya kutosha kupata data zilizolengwa kukidhi mahitaji ya utafiti wetu. Data za upili zilipatikana katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania iliyopo Dar es Salaam, maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta iliyopo Nairobi, Kenya na ile ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Dar es Salaam. Maktaba hizi ziliteuliwa kwa kuwa zina machapisho ya kutosha yaliyohusiana na mada ya utafiti huu.

## 3.5 Populesheni Lengwa ya Utafiti

Katika utafiti populesheni inafasiliwa kuwa ni kundi la watu lenye kufanana katika mambo kadhaa kama vile utamaduni, ambamo sampuli huchukuliwa (Kombo na Tromp, 2006). Populesheni lengwa ya utafiti inahusisha jamii nzima, makundi ya watu, au vitu vingine ambavyo kwavyo mtafiti amevihusisha kama chanzo cha data (Cooper, 1989; Vans, 1990). Hivyo katika utafiti huu populesheni ni jumla ya waimbaji wote wa nyimbo za harusi katika wilaya ya Same.

## 3.6 Sampuli na Usampulishaji

### 3.6.1 Sampuli

Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa kutoka kundi kubwa ambalo linampa mtafiti data zinazosaidia kutoa hitimisho (Kothari, 2009). Sampuli inapatikana kwa njia ya usampulishaji. Hivyo katika utafiti huu sampuli ilikuwa jumla ya wakazi 40 wa wilaya ya Same wenye umri wa miaka 25 ï 45 na 60 -75 katika vijiji/maeneo

vilivyobainishwa (taz. kipengele 3.4). Aidha tuliteua nyimbo 30 tu kati ya nyimbo 65 tulizokusanya, ambazo ndizo zilizotumika katika uchambuzi wa data yetu. Sampuli hii ilichaguliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji nasibu na usampulishaji usonasibu. Sampuli hii imeweza kuwa toshelevu kwa sababu tumechagua maeneo matano kwa kuzingatia mtawanyiko wa kimaeneo. Kila eneo tulichagua wastani wa watafitiwa 8. Aidha idadi hii ya watafitiwa haikuwa ndogo kwa sababu nyimbo nyingine tulizikusanya kwa njia ya kurikodi kupitia mbinu ya ushiriki. Hivyo data hii iliweza kukidhi haja yetu na kuwakilisha wilaya nzima.

### 3.6.2 Usampulishaji

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006) usampulishaji ni mchakato wa kuchagua sampuli au sehemu ya populesheni inayowakilisha populesheni nzima. Kwa upande mwingine usampulishaji ni mchakato wa uteuzi wa watafitiwa kutoka katika populesheni lengwa ya utafiti ili wawe sampuli ya utafiti (Kothari, 2009).

Utafiti huu umetumia wakazi wa vijiji/maeneo vilivyobainishwa na idadi yao (taz. jedwali na.1). Wakazi hao wamegawanyika katika kategoria kuu mbili. Mosi, wazee 15 wenye umri wa miaka 60 ï 75, ambapo wanawake walikuwa 10 na 5 ni wanaume. Kategoria ya pili ilikuwa kundi la vijana wenye umri wa miaka 25- 45, ambapo jumla walikuwa vijana 25; wanawake 15 na wanaume 10. Kundi la wazee sio wengi kiidadi kwa sababu wazee sio waimbaji wa nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu, ila tumeliteua ili kutupatia uzoefu wao kuhusu tamaduni za jamii hii ikiwemo nyimbo zake za harusi. Aidha kundi la vijana ni wengi kiidadi kwa sababu ndio waimbaji wa nyimbo hizi kwenye sherehe za harusi za jamii hii. Kwa upande

mwingine idadi ya wanawake kiujumla ni kubwa kwa sababu ndio hasa waimbaji wakuu wa nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu.

Utafiti huu umetumia usampulishaji nasibu na usampulishaji usonasibu. Usampulishaji usonasibu ni mbinu ambayo inamsaidia mtafiti kupata wahojiwa wale tu anaowataka ili kupata data anazozihitaji. Katika mbinu hii, watafitiwa hawawi na nafasi sawa ya kuchaguliwa bali mtafiti huchagua watafitiwa wale tu anaowataka na uteuzi wake hufanywa kwa makusudi kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa (Chava na David, 1981: 303). Mbinu hii imetumiwa kwa sababu si kila mtu angeweza kujua na kuimba nyimbo za harusi za jamii ya Waasu kikamilifu.

Aidha mbinu hii pia ilitumika kuwapata walengwa wale tu waliokuwa na ujuzi wa kusoma na kuandika. Kutengwa kwa kundi la wasiojua kusoma na kuandika hakukuweza kuathiri data yetu kwa sababu kundi hilo ni dogo mno. Aidha, mbinu ya usampulishaji nasibu ilitumika kupata nyimbo 30 kati ya 65 zilizokuwa zimekusanywa, ambazo ndizo zilizotumika katika uwasilishaji na mjadala wa data.

Nyimbo zote 65 zilipewa namba zilizokuwa zimeandikwa katika vikaratasi vidogo vidogo vilivyoviringishwa vizuri na kutupwa chini. Kisha vilikusanywa pamoja. Mtafiti alilenga kuchota vikaratasi thelathini (30) kwa kutumia mkono ili kupata sampuli yake. Mtafiti alifumba macho, kisha kuokota vikaratasi hivyo kimoja kimoja hadi vilivyofika 30. Mbinu hii ni nzuri kwani huepuka upendeleo. Nyimbo hizo ndizo zilizotumika kama sampuli na kuwasilishwa katika mjadala wa data.

Ukusanyaji wa data yetu kwa njia ya ushiriki hatukuzingatia vigezo vya umri, elimu na jinsia kwani ilikuwa vigumu kuwaainisha waimbaji wa nyimbo za harusi za Waasu katika sherehe za harusi tulizohudhuria. Hii ni kutokana na mbinu tuliyotumia ya ushiriki wa moja kwa moja bila ya kujulikana na watafitiwa. Mbinu hii nayo ilikuwa mwafaka kwa sababu ilitupatia idadi kubwa ya nyimbo za harusi zilizojumuishwa katika uchanganuzi wa data yetu.

**Jedwali Na. 3.1: Sampuli ya Utafiti**

| **Na.** | **Kundi la Watafitiwa** | **Umri (Miaka)** | **Kata ya Mhezi** | | | | **Kata ya Same Mjini** | | | | **Kata ya Mshewa** | | **Idadi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kijiji Cha Mhezi** | | **Kijiji Cha Mtunguja** | | **Mtaa Wa Mjini** | | **Mtaa Wa Stesheni** | | **Kijiji cha Kwizu** | | |
| | | | **me** | **ke** | **me** | **ke** | **me** | **ke** | **me** | **ke** | **me** | **ke** | |
| 1. | Vijana | 25-45 | 2 | 3 | 2 | 3 | 2 | 3 | 2 | 3 | 2 | 3 | 25 |
| 2. | Wazee | 60-75 | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 2 | 15 |
| | **JUMLA** | | 3 | 5 | 3 | 5 | 3 | 5 | 3 | 5 | 3 | 5 | **40** |

**Chanzo:** Mtafiti 2018

## 3.7 Vyanzo vya Data

Katika utafiti huu tumekusanya data za aina mbili. Kuna data za msingi na data za upili.

### 3.7.1 Data za Msingi

Data za msingi hurejelea data zilizokusanywa kwa mara ya kwanza kabisa katika utafiti fulani. Data za msingi ni zile ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine kwa ajili ya utafiti kama anaofanya mtafiti wakati huo (Yin, 1984). Katika tasinifu hii, data za msingi ni nyimbo za harusi za jamii ya Waasu zilizokusanywa mkoani Kilimanjaro katika wilaya ya Same. Kata ya Mhezi; vijiji vya Mhezi na

Mtunguja, kata ya Mshewa; kijiji cha Kwizu na kata ya Same Mjini, mtaa wa Stesheni na mtaa wa Mjini. Maeneo hayo yalitupatia data zilizokidhi mahitaji ya utafiti huu. Mbinu za usaili, hojaji na ushiriki zilitumika katika ukusanyaji wa data za msingi.

### 3.7.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zimekwisha kusanywa na watafiti wengine na kuwekwa katika machapisho mbalimbali (Newman, 2006). Data za upili hukusanywa kwa ajili ya kukamilisha data za msingi zilizokusanywa. Mbinu hii hujulikana kama mbinu ya kukusanya data mezani (Hakim, 2000). Hii ni kwa sababu mtafiti haendi maskanini kufanya mahojiano na watafitiwa. Katika utafiti huu data za upili zilikusanywa katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania iliyopo Dar es Salaam, maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta iliyopo Nairobi, Kenya na maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Dar es Salaam. Mbinu ya kinyaraka ilitumika kupata data za upili.

## 3.8 Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti huu data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uwandani na maktabani. Data zilikusanywa kwa mbinu za hojaji, ushuhudiaji, usaili na ile ya kinyaraka.

### 3.8.1 Mbinu ya Hojaji

Hojaji ni orodha (kwa maandishi) ya maswali yanayohitaji kujibiwa au kuelezwa na wahojiwa kwa lengo la kukusanya taarifa (Chava na David, 1981). Kwa msingi huo, hojaji ni njia ya kukusanyia data na taarifa kutoka kwa watafitiwa kimaandishi. Mtafiti alikusanya data kwa kupeleka hojaji kwa watafitiwa 25 ambao walizijaza. Hojaji zilitumika katika kundi la vijana wenye umri wa miaka 25-45. Mtafiti alitumia mbinu hii kutokana na kwamba baadhi ya vijana ilikuwa vigumu kuwapata moja kwa moja na kufanya nao majadiliano kutokana na majukumu ya kazi. Vile vile mbinu hii inatoa fursa kwa mtafitiwa kutafakari kabla hajajaza anachoulizwa. Kwa upande mwingine, mbinu hii ina usiri mkubwa kwa sababu majina ya watafitiwa hayaandikwi katika hojaji. Kutokana na hali hiyo, watafitiwa walikuwa huru kujaza hojaji hizo kulingana na uelewa na tajiriba yao kuhusu nyimbo za harusi za jamii ya Waasu.

### 3.8.2 Mbinu ya Usaili

Usaili ni majibizano ya ana kwa ana (simu au kidijitali) baina ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililobainishwa (Kombo na Tromp, 2006). Njia hii ilitumiwa na mtafiti kwa kuhojiana ana kwa ana na watafitiwa ili kukusanya data zilizohusu nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Kundi lililotumia mbinu hii ni lile la wazee kuanzia miaka 60 - 75. Hii ni kwa sababu tuliamini baadhi ya watafitiwa kutoka kundi hili walikuwa na matatizo ya uoni kutokana na uzee, hivyo mbinu hii ilikuwa mwafaka zaidi kwao. Pia tuliamini kundi hili lina uzoefu mkubwa zaidi katika masula ya utamaduni wa

jamii hii ikiwemo nyimbo za harusi, hivyo basi ilikuwa mwafaka zaidi kuhojiana nao. Aidha, usaili huo ulilenga kupata dhima zinazobebwa katika nyimbo za harusi za jamii hiyo, pamoja na kujadili usanaa unaojibainisha katika kipengele cha lugha. Mbinu ya usaili ilimsaidia mtafiti kusaili taarifa mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti.

### 3.8.3 Mbinu ya Ushiriki

Mbinu ya ushiriki katika ukusanyaji data ni ile ambayo mtafiti anaenda uwandani na kushiriki katika shughuli za wale anaowatafiti (Kombo na Tromp, 2006). Kwa kutumia mbinu hii mtafiti alienda wilayani Same katika kata ya Mhezi, vijiji vya Mhezi na Mtunguja, kata ya Mshewa, kijiji cha Kwizu na kata ya Same Mjini, mtaa wa Stesheni na mtaa wa Mjini. Katika maeneo hayo mtafiti alishiriki katika baadhi ya harusi za Waasu. Wakati wa ushiriki mtafiti alirekodi nyimbo za harusi za jamii ya Waasu kwa njia ya vinasasauti kupitia simu ya kiganjani.

Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kwa kuwa huwezesha kupata data halisi, kwa sababu watafitiwa walikuwa huru katika uimbaji wao kwa kuwa hawakujua kinachoendelea. Pia, mbinu hii ilisaidia kupata data ambazo zisingepatikana kama angetumia mbinu nyingine.

Tuliweza kuhuduria sherehe nne za harusi zilizofanyika katika eneo lililolengwa katika utafiti wetu. Kwa mfano, tulishiriki sherehe ya bwana Fredi Msuya iliyofanyika tarehe 30/08/2018 kijijini Mhezi kata ya Mhezi; Elisante Mmbaga tarehe 01/09/2018 eneo la kata ya Mshewa kijiji cha Kwizu, Bwana Bony Chediel ya tarehe 06/09/2018 iliyofanyika eneo la Same mjini na harusi ya bwana Eliakimu Mkumbwa

iliyofanyika tarehe 08/09/2018 huko Same mjini. Katika mbinu hii watafitiwa walikuwa huru kuimba kwa kadiri walivyoweza, huku mtafiti akiwa ni sehemu yao naye akishiriki kuimba nyimbo hizo pamoja na shughuli zilizoambatana nazo kama vile kucheza na kushangilia pasipo kujibainisha.

### 3.8.4 Upitiaji wa Nyaraka

Mbinu ya kinyaraka inahusu ukusanyaji wa data za upili kwa kusoma machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti (Ngechu, 2002). Data za upili ni zile ambazo tayari zimewekwa katika kumbukumbu za kimaandishi. Mbinu hii humsaidia mtafiti kushughulikia moja kwa moja kile ambacho anahitaji kukitafiti (Sharma, 2008). Mtafiti alidurusu machapisho mbalimbali ili kupata data za upili zilizotumika katika urejelezi na ufafanuzi wa data za msingi za utafiti uliofanyika. Maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania iliyopo Dar es Salaam, Chuo kikuu cha Kenyatta iliyopo Kenya na ile ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Dar es Salaam zilitumika kupata data za upili zilizokuwa zimelengwa katika utafiti huu.

## 3.9 Uchambuzi wa Data

Kulingana na Boote na Penny (2005), uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia data vizuri kwa jinsi ambavyo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Katika tasinifu hii, mtafiti alichambua data kwa kutumia mkabala wa kimaelezo ambao haukuhusisha takwimu katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za msingi. Mtafiti alizipanga data kulinga na malengo na maswali ya utafiti ili uchambuzi wa data ulandane na malengo na kujibu maswali ya utafiti. Ili kupata mtiririko mzuri wa uchanganuzi wa data kulingana na malengo na maswali ya utafiti,

data zote zilipewa msimbo wa kimaelezo. Pia, data fuatizi zilinukuliwa pale ilipobidi ili kuthibitisha uchambuzi wa data za msingi.

Sambamba na mkabala wa kimaelezo, mtafiti aliongozwa na mhimili wa nadharia za Uhalisia na Simiotiki katika uchambuzi na uwasilishaji wa data. Nadharia ya Uhalisia ilitumika kwa kuwa ina uhusiano mkubwa na hali halisi ya masuala yaliyopo katika jamii yanayojidhihirisha kupitia kazi za kisanaa. Aidha, nadharia ya Simiotiki ilitumika kwa kuwa ina uhusiano mkubwa na masuala ya lugha. Kwa kuwa mtafiti alilenga kuchunguza dhima na usanaa wa lugha katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu, nadharia hizo zilikuwa muafaka katika uchambuzi na uwasilishaji wa data zilizolengwa. Aidha uwasilishaji wa data kwa ujumla umefanyika katika sura mbili; sura ya nne na katika sura ya tano. Hii ni kutokana na urefu wa sura hizi. Sura ya nne imejikita katika lengo mahususi la kwanza na sura ya tano lengo la pili.

### 3.10 Itikeli ya Utafiti

Mligo (2012) anashauri kwamba watafiti ambao watafitiwa wao ni watu au wanyama wanapaswa kuwa na maadili wanapofanya tafiti na wachukue tahadhari kuhusu mambo ya kimaadili yanayohusiana na tafiti wanazofanya. Aidha, Fink (1998) anaeleza kwamba, kanuni za maadili ya utafiti zinahusisha mtafiti kuwa na usiri, kupata kibali cha kwenda kufanya utafiti na kupata ridhaa ya watafitiwa kushiriki kutoa data.

Kwa kuzingatia kanuni hizo, mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka kwa Mratibu wa utafiti wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Vile vile mtafiti alipata kibali cha utafiti kutoka kwa Mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya ya Same.

Pia, kila alipokuwa anakutana na watafitiwa, mtafiti alijitambulisha na kufafanua malengo na umuhimu wa utafiti huu.

Kwa kufuata utaratibu, mtafiti alikuwa anawaomba watafitiwa kushiriki katika utafiti kwa ridhaa yao na aliwahakikishia kuwa data watakazozitoa ni siri na zitatumika kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti na si vinginevyo. Hayo yalifanywa kwa maandishi mwanzoni mwa hojaji walizopewa kujaza na pia kupitia mazungumzo ya ana kwa ana wakati wa mahojiano.

## 3.11 Usahihi wa Data

Usahihi wa mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data halali na za kuaminika (Cohen na wenzake, 2000). Kuaminika kwa data za utafiti hutokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data ili kufanikisha upatikanaji wa data halali na sahihi. Ubora wa mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data humwezesha mtafiti kupata data sahihi na za kuaminika.

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa mbinu za hojaji, ushiriki, usaili na ile ya kinyaraka. Uchambuzi wa data uliongozwa na nadharia za Uhalisia na Simiotiki,

pamoja na mbinu za kimaelezo na kidhamira. Kwa kawaida, upungufu wa mbinu moja hukamilishwa na ubora wa mbinu nyingine (Dornye, 2007). Kwa msingi huo, upungufu wa mbinu moja ulikamilishwa na ubora wa mbinu nyingine. Aidha, mjadala kuhusu uhalali wa mbinu zilizotumika ulifanyika baina ya mtafiti na msimamizi wake, pamoja na wanataaluma wa fasihi katika ngazi ya uzamili katika fasihi ya Kiswahili. Kwa ujumla, usahihi wa data katika tasinifu hii umehakikiwa kwa kutumia mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data zilizotoa majibu yanayolingana.

## 3.12 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kuhusu mbinu za utafiti. Baadhi ya vipengele vilivyochunguzwa ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, jamii ya watafitiwa na vyanzo vya data. Pia, kuna walengwa wa utafiti, mbinu za ukusanyaji data, uchambuzi wa data na itikeli ya utafiti. Mbinu hizo ndizo zilizomwongoza mtafiti katika ukusanyaji wa data, uchambuzi na uandishi wa ripoti ya utafiti. Mbinu hizo zilitegemeana na kukamilishana katika ukusanyaji, uwasilishaji na mjadala wa data za utafiti uliofanyika katika sura ya nne na ya tano. Sura ya nne inayofuata inahusu uwasilishaji na mjadala wa data.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data zilizokusanywa kutoka uwandani, ikijikita katika lengo la kwanza la utafiti wetu lililohusu kuchunguza dhima ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Aidha, sehemu hii nayo imeganyika katika vipengele vingine vidogovidogo vinavyohusiana na dhima husika. Katika kila kipengele nyimbo kadhaa za harusi katika jamii ya Waasu zimerejelewa na kujadiliwa kwa kina. Baadhi ya nyimbo zimerejelewa katika dhima zaidi ya moja kutokana na upana wa kidhima uliobebwa na wimbo husika. Mjadala wa data umezingatia dhima ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Aidha nyimbo zimewasilishwa kwa utaratibu wa kupewa majina ili kurahisisha urejelezi wake katika hatua mbalimbali. Jumla ya nyimbo 30 zimetumika katika mjadala wa data yetu.

## 4.2 Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasu

Wamitila (2004) anasema, nyimbo zinazoimbwa kwenye sherehe za ndoa zinakuwa na majukumu ya kuwashauri wanaooana. Pia, huonesha masitikiko ya bibi harusi kuondoka nyumbani, kukashifiana na kuelekeza kuhusu matarajio na maisha ya unyumba. Jamii ya Waasu ni miongoni mwa jamii zenye utamaduni wa sherehe ya harusi tangu zamani. Utafiti huu umelenga kuchunguza dhima ya nyimbo za harusi za jamii hiyo.

Jamii ya Waasu ina utamaduni wa aina mbalimbali, mojawapo ya utamaduni huo ni nyimbo za harusi (Kimambo, 1967). Mtaalamu huyu anaelezea mila na tamaduni

mbalimbali za jamii ya Waasu, kwa mfano, katika sherehe za harusi lazima shughuli hii iambatane na nyimbo za harusi. Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zina majukumu mbalimbali. Dhima za nyimbo za harusi hulenga kutoa maonyo kwa maharusi, kupongeza na kuwahimiza waoanao kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mila na desturi za jamii yao. Kwa mujibu wa Wamitila (2004), nyimbo za harusi huwa na mawazo mazito, na hulenga huliwaza na kuburudisha, ndio maana takriban shughuli zote za kuoa na kuolewa katika jamii huambatana na uimbaji wa nyimbo. Kwa ujumla, nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zina dhima za aina mbalimbali.

Dhima ya nyimbo za harusi za jamii ya Waasu huweza kugawanywa katika makundi mbalimbali kulingana na tukio linalohusika. Kwa mfano, zipo nyimbo zinazoimbwa wakati wa kwenda kumchukua mwali na kuingia katika nyumba ya wakwe. Nyimbo hizo huimbwa watu wakiwa karibu na nyumba ya wakwe upande wa bibi harusi. Aidha, nyimbo hizi huendelea kuimbwa mpaka wageni walioenda kumfuata mwali wanapopokelewa na kupewa viti na baadaye kukaribishwa chakula na vinywaji.

Pia, zipo nyimbo zinazoimbwa zikiwa na ujumbe wa kuomba mwali kutoka kwa baba na mama mkwe. Kwa kawaida, katika harusi za Waasu mwali hufichwa ndani mpaka wakati maalumu wa kuagwa ukifika na hawezi kutoka mpaka ziimbwe nyimbo za kumwomba. Nyimbo hizo huimbwa mara baada ya wakwe kutoka kwa bwanaharusi kumaliza kula na kupumzika kwa muda. Baada ya mwali kutoka na kupewa zawadi, ukiwamo wasia wa aina mbalimbali wakwe huanza kuimba nyimbo za kuaga kabla ya kuondoka. Kwa ujumla nyimbo hizi huwa na ujumbe wa kushukuru, pamoja na kuaga.

Aidha, zipo nyimbo zinazoimbwa ili kumkaribisha mwali nyumbani kwao bwana harusi. Hili ni kundi la nyimbo zinazoimbwa pindi maharusi pamoja na waliokwenda kuchukua mwali wanaporejea nyumbani kwao bwanaharusi. Nyimbo hizi huwajulisha wazazi wa bwanaharusi, ndugu na jamaa waalikwa kwamba mwali anaingia katika mji wao. Nyimbo za shangwe, nderemo, vifijo na vigelegele husikika katika kaya ya wazazi wa bwanaharusi kwa kufuata miongozo na utamaduni wa jamii hii. Kwa kawaida, nyimbo hizo huimbwa kwa kufuata misingi ya mila na desturi za jamii ya Waasu.

Kwa muhtasari, kwa uzoefu wetu nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zimegawanyika katika makundi makuu manne. Makundi hayo ni nyimbo za wakati wa bwanaharusi kuingia katika nyumba ya wakwe (kwao binti), nyimbo za kuomba mwali akiwa nyumbani kwao, nyimbo za kutoa shukurani na kuaga baada ya kukabidhiwa mwali, nyimbo za mwali kuingia nyumbani kwao bwanaharusi/kumkaribisha bibi harusi ukweni. Kulingana na mapokeo ya wenyeji, nyimbo hizo huitwa nyimbo kuu kwa sababu ni lazima ziimbe kwa namna yoyote ile katika sherehe za harusi za jamii hii.

### 4.3 Uchambuzi wa Dhima za Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasu

Data zilizokusanywa katika utafiti huu ni nyimbo za harusi za jamii ya Waasu waishio katika wilaya ya Same. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti na kuongozwa na mihimili ya nadharia za Uhalisia na Semiotiki. Mbinu za kimaelezo na kidhima zilitumika katika uchambuzi wa data zilizolengwa. Baadhi ya nyimbo zilizokusanywa hazikuchambuliwa katika ujumla wake, bali zilichukuliwa katika vifungu au beti chache chache muhimu na kuzitumia

kama kiwakilishi cha wimbo mzima. Hii ni kwa sababu baadhi ya nyimbo zilikuwa ni ndefu mno.

Mtafiti aliwashirikisha watafitiwa katika hatua ya uchambuzi ili kubaini uelewa wao uliomo katika nyimbo zilizokusanywa kwa kuwauliza maswali na kufanya majadiliano. Ushirikishwaji wa watafitiwa katika kufasili data zilizokusanywa ulimsaidia mtafiti kutumia maarifa ya wazawa katika uchambuzi wake. Hali hiyo ilimwezesha mtafiti kuunganisha mawazo ya watafitiwa na tafakuri yake katika uchambuzi wa data zilizokuwa zimelengwa. Hatua hiyo ilikuwa muhimu katika kuondoa upendeleo wa kifasili, kama Pollock (2005) anavyoeleza kwamba, ni vizuri kuwashirikisha watafitiwa katika uchambuzi wa data ili kuimarisha mamlaka ya matokeo ya utafiti. Kwa msingi huo, nyimbo 30 za harusi za jamii ya Waasu zilichambuliwa kulingana na lengo mahsusi la kwanza, lililomtaka mtafiti, kuchunguza dhima ya nyimbo za harusi za jamii ya Waasu**.** Aidha, nyimbo hizo ziliandikwa kwa Chasu na baadaye tulizitafsiri kwa kiswahili. Zipo chache zilizokuwa katika lugha ya Kiswahili, hizo tulizichambua moja kwa moja. Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zimebainika kuwa na dhima mbalimbali, kama ilivyoelezwa katika sehemu inayofuata.

### 4.3.1 Kudumisha Upendo

Mulokozi (1996) anaeleza kwamba, nyimbo katika jamii yoyote ile zina dhima kubwa sana katika kuendeleza, kudumisha na kuhifadhi mila na desturi za jamii. Kudumisha upendo ni mojawapo ya dhima inayojitokeza katika nyimbo za harusi za Waasu ambayo imejitokeza katika uchambuzi wa data yetu. Huu ndio mojawapo ya msingi wa nadharia ya Uhalisia kuitazama kazi ya fasihi inavyosawiri hali za kijamii

kwa kuzingatia uyakinifu wa mazingira yanayomzunguka binadamu. Kwa msingi huo, dhima ya kudumisha upendo ilichunguzwa namna inavyosawiriwa kwa mujibu wa data yetu inavyojitokeza katika wiimbo wa ***Ambiere evava e mghosi ee*** (Baba mkwe shikamoo, shikamoo), kama waimbaji wanavyoeleza:

| | |
|---|---|
| *Ambiere evava e mghosi ee,* | Baba mkwe shikamoo, shikamoo, |
| *Ambiere evava e mghosi eee* | Baba mkwe shikamoo, shikamoo, |
| *Ne vamcheku eee eee eee x2,* | Na akina mama mkwe shikamoo ×2*,* |
| *Ghuhieni ngezia x3,* | Pokeeni salamu ×3, |
| *Jefuma noko hetu,* | Zinazotoka huko kwetu, |
| *Vazima na vadori vose vemkezia.* | Wakubwa kwa wadogo wanawasalimia. |

Wamitila (2004) anaeleza kwamba, nyimbo ni njia nzuri ya kupitisha thamani za kitamaduni katika jamii mbalimbali. Wimbo huu unaimbwa kipindi cha kwenda kumchukua mwali, ndugu na jamaa wa bwanaharusi wanapokaribia nyumbani kwao bibiharusi. Wimbo huu huonesha upendo baina ya wazazi na ndugu wa upande wa bwanaharusi na wale wa upande wa bibi harusi. Hujikita katika maamukizi ambapo ni miongoni mwa kipengele cha mila na utamaduni wa jamii wa Waasu, na kwamba upendo huanzia katika kusalimiana na kujuliana hali. Wimbo huo huonesha kwamba, upendo ni jambo la muhimu kwao baada ya familia zao kuunganishwa na vijana wao.

Aidha, upendo hudumisha na kujenga umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii (Ibarahim, 2005). Jambo hili linapewa nafasi kubwa na jamii ya Waasu kwa kuwa ni mojawapo ya vipengele muhimu vya mila na desturi vya jamii hiyo.

Katika wimbo wa ***Mwekiketa shida mnatete*** (Mkipata shida mtoe taarifa) jambo hili linajibainisha zaidi;

| | |
|---|---|
| *Mwekiketa shaida mnatume ee,* | Mkipata shida mtoe taarifa, |
| *Ambu kaka wetu si mvivi,* | Kwani kaka yetu si mtu mbaya, |
| *Mama iyele iyele iyele x2,* | Mama iyele iyele iyele ×2, |
| *Lukwi la kibare tukaote ee,* | Hutaota moto wa kuni za kuchana ee, |
| *Cho weneota ni makongoti x2.* | Moto utakaoota ni wa magunzi ×2 |

Upendo kama mojawapo ya kipengele cha mila na utamaduni wa jamii ya Waasu hutakiwa kuendelezwa hususan kwa ndugu, marafiki au watu wa karibu. Hili hujidhihirisha katika wimbo huo. Huelezea kwamba, bwanaharusi ni mtu mwenye upendo na hivyo ndugu kutoka upande wa bibiharusi wakipata shida waseme naye atawasaidia. Mulokozi (1996) anaelezea kwamba, tangu kale nyimbo zimetumika kama chombo kikuu cha kurithisha na kudumisha mila na utamaduni wa jamii. Aidha, katika jamii yoyote ile upendo ni jambo muhimu linaloleta ustawi na uhusiano imara wa watu na jamii inayohusika (Kanyama na Wenz, 2004). Hivyo kwa ujumla, kipengele hiki cha utamaduni ni vyema kidumishwe na kuendelezwa,

Katika wimbo wa ***Hoodi tuvagheni*** (Hoodi tu wageni) huelezea zaidi suala la kudumisha upendo. Hujikita katika kutoa salamu kwa wale waliopo katika sherehe na wale waliobaki nyumbani.

| | |
|---|---|
| *Hooodi tuvagheni, hooodi tuvagheni x2* | Hoodi tu wageni, hoodi tu wageni ×2, |
| *Ghuhieni ngezia jefuma noko hetu* | Pokeeni salamu zinazotoka huko kwetu, |
| *Vabaha na vadori veti vemkezia* | Wakubwa kwa wadogo wanawasalimia. |

Wimbo huu ni mojawapo wa zile zinazoimbwa wakati ndugu wa bwanaharusi wakiingia nyumbani kwa wakwe upande wa bibiharusi. Wakati huo baba na mama pamoja na ndugu wengine wa bibiharusi hutoka nje wakipiga makofi kuwakaribisha wakwe zao. Wimbo huu hutoa ujumbe wa salamu kutoka kwa ndugu wa upande wa bwanaharusi. Salamu ni kitu muhimu sana katika jamii ya Waasu; ni udhihirisho wa juu kabisa wa kuonesha upendo. Hali hii inasawiri nadharia yetu ya uhalisia, kama anavyoeleza Spurlin & Fischer (1985) kwamba uhalisia katika jamii huelezwa jinsi ulivyo katika fasihi na unaichukulia fasihi kama zao halisi la jamii.

Aidha, dhima kuu ya nadharia ya uhalisia ni kuzisawiri hali halisi za maisha ya watu katika jamii husika kupitia fasihi. Nyimbo ni chombo cha jamii kinachohakiki tabia za watu na chenye uwezo wa kutoa mwelekeo na kuirekebisha jamii juu ya maisha yao, pamoja na kuweza kuyatambua na kuyatawala kwa urahisi (Luhanga, 1988). Hivyo, wimbo huu unaonesha umuhimu wa salamu kwa jamii nzima.

### 4.2.2 Kudumisha Heshima

Heshima ni mafunzo yaliyotolewa katika jamii kupitia maeneo mbalimbali ya utamaduni wa jamii. Aidha, heshima ni mojawapo ya jambo linaloleta ustawi wa jamii, unaojenga amani na utulivu katika jamii. Nyimbo za harusi ni mojawapo ya taasisi ya mafunzo hayo kwa jamii ya Waasu. Nyimbo hutumiwa kama nyenzo muhimu ya kupitisha thamani ya kitamaduni katika jamii na kwamba nyimbo fulani huakisi vipengele mbalimbali vya utamaduni wa jamii (Wamitila, 2004). Suala hili husawiriwa katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu kwa mawanda mapana kwa kuwa hulenga kusisitiza umuhimu wa maharusi kuwaheshimu wazazi wao wa pande zote. Nyimbo ni njia anayoitumia mwanadamu kuelezea hisia zake za ndani, hisia

zinazoelezwa kwa njia hiyo huwa na athari kubwa zaidi (Silau, 2013). Hivyo, nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu ni miongoni mwa njia kuu inayosawiri hisia za ndani kuhusu masuala yanayohusiana na heshima. Wimbo wa ***Lubegho lwa mwana luwaja*** (Uchungu wa mtoto unauma) huimbwa na akina mama kuelezea uchungu wa kumzaa binti. Wimbo huu unadhihirisha dhima hii (kudumisha heshima);

| | |
|---|---|
| *Lubegho lwa mwana luwaja,* | Uchungu wa mtoto unauma, |
| *Aheee luwaja x2,* | Aheee unauma x2, |
| *Luwaja kangi ugure kikwidi,* | Unauma hadi ushike kiuno ee, |
| *Aheee luwaja,* | Aheee unauma, |
| *Luwaja kangi ugure ndeni,* | Unauma hadi ushike tumbo ee, |
| *Aheee luwaja,* | Aheee unauma, |
| *Luwaja kangi ugure mtwi,* | Unauma hadi ushike kichwa eee, |
| *Aheeee luwaja*. | Aheee unauma. |

Wimbo huu hutumia lugha ya mafumbo kuelezea jinsi mama alivyomzaa binti kwa taabu kubwa. Hivyo, wazazi kwa ujumla wanastahili heshima kubwa kutoka kwa vijana wao (maharusi), vinginevyo laana itawaangukia. Kulingana na mila na desturi za jamii ya Waasu, wimbo huu huimbwa na akina mama tu, kama sehemu ya wasia kwa maharusi. Mlambia (2017) anaeleza kwamba, nyimbo zina dhima mbalimbali kama vile kuhimiza maadili mema, kuionya jamii na kudumisha heshima miongoni mwa wanajamii.

Vilevile wimbo wa ***Mama hooho hooho*** (Mama mbembeleze) nao huelezea dhima ya kudumisha heshima, ambapo maharusi husisitizwa kuendelea kuwaheshimu wazazi wao. Huelezea jinsi maharusi wakiwa watoto wadogo walivyokuwa wanabembelezwa na wazazi wao, na sasa maharusi nao wanatakiwa

kuwabembeleza, yaani kuwaheshimu na kuwanyeyekea wazazi. Waimbaji wanapoimba ***mama hooho hoooho (***mama mbembeleze) humaanisha maharusi wanatakiwa wawabembeleze wazazi wao yaani kuwapa heshima na unyenyekevu wa hali ya juu. Hali hii inaakisi nadharia yetu ya uhalisia, yaani nyimbo hizi huonesha hali halisi iliyomo katika jamii. Sengo (2009) akishadidia nadharia ya uhalisia anasema msingi wa nadharia ya uhalisia ni ule uhusiano wa moja kwa moja uliopo kati ya shughuli za kijamii, mazingira na fasihi.

Aidha, wimbo wa ***Mama huyoo*** vilevile huingia katika kundi la nyimbo zinazobeba dhima ya kudumisha heshima;

> Maaama huyo, mama, mama huyo ee,
> Mama mama huyo mama maaama huyo mama,
> Mpe mkono, mama, maaama huyo mama,
> Alikulea, mama maaama huyo mama,
> Baaaba huyo, baba baba huyo ee,
> Baba baba huyo baba baaaba huyo baba,
> Mpe mkono, baba baaba huyo baba,
> Alikule baba baaba huyo baba ×2.

Nukuu hii inasisitiza suala la heshima kwa wazazi kutoka kwa maharusi. Huonesha jinsi wazazi walivyowalea maharusi na wanavyoendelea kuwapenda, hivyo maharusi hupewa somo kwamba nao wanatakiwa kudumisha heshima kwa wazazi. McNiff (1992) anaeleza kwamba, nyimbo ni mbinu mojawapo ya vyombo vya kueleza hisia na maono; na ni namna pekee ya kujieleza ambayo kila mtu huweza kuitumia wakati wowote bila gharama. Nyimbo hizi huelekezwa kwa wazazi zikiwa na dhima ya kuonesha heshima kwao. Huibwa kipindi wazazi wanapokwenda kutoa zawadi kwa vijana wao wakati wa kumuaga binti na wakati wa kumkaribisha kwa

upande wa bwanaharusi. Nyimbo zote hizi huonesha umuhimu wa watoto kuwaheshimu wazazi, kwamba wao ndio waliowazaa na kuwalea, hivyo wanapaswa kuwaheshimu. Kwa kawaida, nyimbo za namna hii huibua hisia kwa maharusi kwa kurudisha kumbukumbu nyuma, jinsi walivyolelewa na kuhangaikiwa na wazazi wao (Kingɛ̂i na Kisovi, 2005). Hivyo, kuchochea mioyo ya kuwapenda wazazi wao siku zote.

Katika wimbo wa ***Tuomba mwai wetu*** (Tunaomba mwali wetu), waimbaji husisitiza uumuhimu wa heshima kwa wazazi kama ilivyobainishwa hapa chini;

| | |
|---|---|
| *Tuomba mwai wetu tutonge naye uko hetu,* | Tunaomba mwali wetu twende naye kwetu, |
| *Kweri kididi vava izuva laingi he ntuvi,* | Kweli baba jua limezama. |

Wimbo huu huimbwa wakati wa kumwomba mwali, huonesha dhima ya heshima, kwamba ukitaka kitu hususan kutoka kwa mzazi ni lazima uoneshe heshima na unyenyekevu. Wimbo huo huimbwa ili kumwomba baba amruhusu mwali atoke ndani. Unapoimbwa, baba wa bibi harusi naye hutakiwa kupokea heshima aliyopewa kwa kuridhia maombi hayo. Kama wimbo huu haukuimbwa, basi mwali hawezi kutolewa ndani. Hali hii inahakiki misingi ya nadharia ya Uhalisia kwamba mojawapo ya majukumu ya kazi za kifasihi ni kuzisawiri hali halisi zilizopo kwenye jamii. Wafula na Njogu (2007) wanashadidia hoja hii kuwa uhalisia hutumiwa kama njia ya kutathmini hali halisi ya maisha ya jamii katika uyakinifu wake. Ukweli huo umejidhihirisha katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu jinsi zinavyoakisi uhalisia wa jamii hii.

### 4.2.3 Kuwapongeza na Kuwasifia Maharusi

Katika jamii yoyote ile mtu anapofanya jambo zuri hustahili kusifiwa na kupewa pongezi. Wamitila (2004) anaeleza kwamba, mojawapo ya majukumu ya nyimbo ni kusifu kwa mtu au watu kwa jambo zuri walilofanya. Mwanasaikolojia Bandru (1971) anaeleza kwamba, tabia fulani huweza kupatikana kutokana na hamasa au kuiga kutoka kwa watu wengine au jamii kutokana na matendo yao au uchunguzi wa moja kwa moja kutoka kwao. Hivyo basi, katika wimbo wa ***Dada wetu tonga*** (Dada yetu nenda) dhima yake kubwa ni kuwasifia na kuwapongeza maharusi, huku pia ukiwalenga vijana wengine ambao hawajafikia hatua hiyo ya kuoa na kuolewa, kuiga mfano wa maharusi kwa kujitunza na kufanya bidii ili nao siku moja wapate sifa na pongezi hizo (wafunge ndoa). Kwa upande wa pili ni kuwahamasisha maharusi kwamba, tabia nzuri zilizowasaidia kufikia hatua ya ndoa waziendeleze.

| | |
|---|---|
| *Dada wetu tonga,* | Dada yetu nenda, |
| *Dada wetu tonga ee x2,* | Dada yetu nenda ee ×2, |
| *Uvavonye utanda ee,* | Uwaoneshe ustaarabu ee, |
| *Verugha makoko ee veti ni mchere,* | Wanapika maboga wanasema ni ugali, |
| *Verugha viongwe weti ni vughai* | Wanapika viazi vitamu wanasema ni ugali |

Wimbo huu unamsifia bibi harusi kwamba ana tabia nzuri ndio maana ameolewa. Katika mshororo wa tatu hadi wa tano unamuelezea bibiharusi kama mwanamke anayejua kupika vizuri. Hukejeli kwamba wapo wasiojua kupika vizuri. Hivyo, hunuia kusema kwamba, bibiharusi ni mweledi wa mambo mengi ikiwa ni pamoja na kupika. Ni kawaida katika jamii yoyote mwanamke anatakiwa awe na tabia njema na kuwa mweledi wa kazi mbalimbali kama vile kupika (Abdulla, 2016 na

Mlambia, 2017). Hii ni sifa ya kumwezesha binti kupata mume katika jamii, ikiwamo jamii ya Waasu. Pia, zipo nyimbo zinazosifia uzuri (wa umbo) wa bibiharusi. Katika jamii nyingi urembo wa msichana ni jambo muhimu kwa binti kupata mchumba. Msichana hutakiwa kujipamba na kuwa mwaminifu na safi (Mahenge, 2009).

Katika data yetu tuliyoipata suala la urembo na weledi wa mambo mengi ni mojawapo ya mambo ya msingi yanayomwezesha binti kuolewa. Wimbo wa ***Hiyo pete yetu naitoke*** hutumika kusifia urembo wa bibiharusi;

> Hiyo pete yeeetu, naitoke naitoke, hiyo pete yetu naitoke.
> Tutaitunza kama kioo, kama kioo tutaitunza kama kioo.

Katika nukuu hii, bibiharusi analinganishwa na pete. Pete ni kitu chenye thamani katika jamii, kinachopendeza na ni ishara ya uzuri na urembo wa bibiharusi. Kwa msingi huo binti analinganishwa nayo kama alama ya kusifiwa na kupongezwa, hivyo basi kupokelewa kwa heshima upande wa familia ya mumewe. Pia, wimbo huu huonesha namna upande wa bwanaharusi wanavyojiapizia kwamba watamtunza mithili ya kioo. Kioo ni kitu cha thamani na kinachotakiwa kushikwa kwa uangalifu, hivyo basi upande wa bwanaharusi wanamsifia bibiharusi kama kioo na kuahidi watamtunza sana. Kimsingi jamii yoyote ile mwanamke hupewa sifa za uzuri kwa kulinganishwa na vitu vizuri na/vya thamani kama vile; maua, kioo, pete nakadhalika. Huu ndio msingi wa nadhari yetu ya uhalisia ya kwamba fasihi huakisi uhalisia wa hali halisi katika jamii. Uhalisia unaeleza namna kazi ya fasihi

inavyouwakilisha ulimwengu wa maisha ya jamii na hali halisi ilyomo (Moore, 1976).

Jambo la kusifia urembo na uzuri wa bibiharusi hujitokeza pia katika wimbo wa ***Anameremeta*** kama ulivyobainishwa hapa chini;

> Anameremeta, anameremeta Ξ2,
> Mwali wetu anameremeta, anameremeta Ξ2,
> Nguo zake zinawaka waka, zinawaka waka Ξ2.

Wimbo huu humuonesha bibiharusi kama ua linalomeremeta na kuonesha mavazi yake kama maua yanayowakawaka. Huimbwa kipindi bibiharusi anakaribia ukweni. Wimbo huu huelezea uzuri na urembo wa bibiharusi, kuanzia sura yake na mavazi halikadhalika. Samwel na wenzake (2013) anaeleza kwamba baadhi ya mambo yanayosawiriwa katika nyimbo ni kusifia kuwa na mke au mume bora/mzuri. Dhima kuu ya wimbo huu ni kumpongeza bibiharusi na kwamba kupitia pongezi hizo wasichana wengine hupata funzo, kwamba nao wajitunze na wawe na tabia nzuri ili waweze kuolewa. Kwa upande mwingine, wimbo huo hutoa wito kwa bibiharusi mwenyewe kuendelea kujitunza ili urembo wake na tabia njema ziendelee kudumu zaidi.

Suala la kusifia maharusi halijikiti kwa bibiharusi tu, bali pia kwa bwanaharusi. Hata hivyo mbali na sifa nyingine yeye hasifiwi kwa uzuri wa sura bali jinsi alivyopata mwanamke mrembo. Suala hili linajitokeza katika wimbo wa ***Kaka esaghure cheaka aka*** (kaka amechagua kinachowaka waka)

| | |
|---|---|
| *Kaka esaghure cheaka aka,* | Kaka amechagua kinacho waka waka, |

| | |
|---|---|
| *Kaka esaghure chekoma meso,*<br>*Cheaka ng᾿we ng᾿we ng᾿we,*<br>*Kikome meso x2.* | Kaka amechagua kinachoumiza macho,<br>Kinachowaka mwaa, mwaa, mwaa,<br>Kiumize macho ×2. |

Wimbo huu umebeba dhima ya kumsifia bwanaharusi kwamba amechagua mwanamke mzuri. Huibwa kipindi bibiharusi akiwa njiani kuelekea nyumbani kwa bwanaharusi au anapokaribia kwao. Kwa kawaida, huimbwa kwa kurudiwa rudiwa hata zaidi ya mara mbili kabla ya kuimbwa wimbo mwingine kutokana na tukio linalohusika. Kimsingi wanamume aliyefanikiwa katika kupata mke mzuri huonekana mtu ambaye anaenda kujenga familia bora (Mauya, 2006). Kwa hiyo, wimbo huu umejikita katika kumpongeza bwanaharusi kwa kupata mwanamke mzuri na mrembo, anayewakawaka na kumeremeta. Aidha, mwanamke kama huyo jamii humchukulia kwamba anaweza kumtuliza mumewe na kumzuia kuchepuka nje ya ndoa kwa sababu ya uzuri wake.

Katika wimbo wa ***Kaka wetu ringa ee*** (Kaka yetu ringa ee) hubainisha zaidi suala la sifa na pongezi kwa bwanaharusi na kumtaka aringe kwani tabu alizokuwa anazipata zitakoma baada ya kuoa;

| | |
|---|---|
| *Kaka wetu ringa ee x3*<br>*Wapata mwai, wekela hoteli iki tukale ee x2.* | Kaka yetu ringa ee ×3<br>Umepata mke, sasa hutakula hotelini ×2. |

Wimbo huu hujikita kwa bwanaharusi kumwelezea kwamba amepata mke. Huelezea zaidi kwamba hatatangatanga tena kwa sababu amepata mtu atakayemtuliza na kumpikia, hivyo usumbufu na gharama za kula hotelini hatazipata tena. Kwa msingi huu anatakiwa aringe. Katika jamii ya Waasu mtu anapofanikiwa kupata kitu kizuri na chenye manufaa, huchukuliwa kama mfano wa kuigwa, hivyo huringa au kujiona

fahari. Hali hii huakisi nadharia yetu, kwamba msingi wake mkuu ni kuakisi hali kama zilivyo katika jamii. Spurlin & Fischer (1985) wanafafanua zaidi juu ya dhana hii, kwamba uhalisia wa maisha katika jamii huelezwa jinsi ulivyo katika fasihi.

Naye Mhando na Balisidya (1976) wanaeleza zaidi kwamba sherehe, ikiwamo harusi katika jamii, zinaambatana na nyimbo zenye ujumbe wa aina mbalimbali kama vile kuwapongeza wari na kuwaelekeza mambo mbalimbali yatakiwayo katika unyumba na ndoa. Kimsingi wimbo wa *kaka wetu ringa ee* (kaka yetu ringa ee) una dhima ya kumpongeza bwanaharusi kwamba anastahili kuringa baada ya kupata mke. Aidha, huelezea kwamba, hatahangaika tena kula ovyo kwani ana mke ambaye atampikia. Katika jamii ya Waasu kuoa ni jambo linalojenga heshima na la kupongezwa kwa kuwa kuoa na kuolewa hutazamwa kama nyenzo mojawapo ya kuendeleza kizazi kimoja hadi kizazi kingine katika ngazi ya familia na jamii nzima ya Waasu.

Kwa ujumla, nyimbo hizi huonesha dhima ya pongezi na kuwasifia maharusi, hasa bibiharusi kwa kujitunza, urembo, usafi, ukarimu na uchapakazi kama sifa mojawapo ya kupata mwenzi. Licha ya nyimbo hizi kuwahusu zaidi maharusi, pia huonesha zinawalenga waliohudhuria katika sherehe hasa vijana ambao hawajaoa kutakiwa kuwa na sifa hizo nzuri na wanapofikia umri wa kuoa au kuolewa kutofanya kosa, kuzingatia sifa hizo.

### 4.2.4 Kusisitiza Ukarimu na Ushirikiano

Ushirikiano ni chachu ya mafanikio katika shughuli zote za kijamii. Jamii za Kitanzania hazina budi kujenga misingi imara ya kushirikiana ili kuyakabili

mazingira yao kwa kadiri zitakavyoweza (Mwipopo, 2016). Kwa kawaida, jamii inahamasishwa kujenga moyo wa kushirikiana katika shughuli mbalimbali. Dhima hii imejitokeza kwa kiasi kikubwa katika nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Dhima ya ukarimu na ushirikiano inajitokeza katika nyimbo mbalimbali, ukiwamo wimbo wa ***Wifi unatete mphoa*** (Wifi uwe na upendo) ambao unasisitiza suala la bibiharusi kuwa na upendo, ukarimu na ushirikiano na wanaomzunguka;

> *Wifi unatete mphoa hako haharwe kajoto x2,*
> *Kangi wekiteta nyaka, hako ni njia ya mivwa x2.*
> Wifi uwe na upendo ili kwako kuombwe moto ×2
> Kama utakuwa na kiburi, kwako kutakuwa njia ya miiba ×2

Wimbo huu humtaka mwali anayeolewa awe mkarimu kwa kila mtu, wakiwamo ndugu wa upande wa mumewe ili apendwe na kupewa ushirikiano. Kwa kawaida, kiburi, lugha ya maudhi na ujeuri humjengea mtu uadui, uhasama na migogoro katika ndoa yake (Bakari, 2010).

Vilevile suala hili la ukarimu na ushirikiano linasisitizwa kwa wazazi wa pande zote mbili. Kwa mfano, mama mkwe wa binti anayeolewa pindi anapofika kwake hutakiwa kuonesha ukarimu wa hali ya juu kwa mwali wwake. Jambo hili linafafanuliwa kwa kina katika wimbo ***Mama virita nkanga*** **(**Mama mfunike mwanao kanga):

| | |
|---|---|
| *Mama virita nkanga mwanao aingi,* | Mama mfunike mwanao kanga aingie, |
| *Kakicha tutegoa mwana ngwa ahunduke,* | Kama hujaridhika mtoto wa watu arudi. |

Wimbo huu huimbwa pindi maharusi wanapofika nyumbani kwao bwanaharusi ambapo mama hutakiwa kuja kwenye geti la kuingia kwenye boma lake na kuwafunika maharusi kanga. Hii ni ishara ya ukarimu na ushirikiano, kwamba mama anamkaribisha mwali wake katika boma lake na kwamba atamsaidia na kuwa mkarimu kwake na kumpa ushirikiano kama mwanae wa kumzaa. Jamii ya Waasu ni jamii inayoishi kwa misingi ya umoja, upendo na ushirikiana tangu kale. Wimbo huu ni mojawapo ya kitu kinachosawiri hali hiyo. Aidha huakisi nadharia yetu ya uhalisia iliyotuongoza katika uchambuzi wa dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu.

Suala la ukarimu na ushirikiano halimhusu mama mkwe wa bibiharusi tu au bibiharusi, bali pia husawiriwa kwa bwanaharusi. Katika wimbo wa ***Mwekiketa shida mnatume*** (Mkipata shida mtoe taarifa), bwanaharusi huelezewa kama mtu mkarimu na aliyeko tayari kutoa ukarimu huo na ushirikiano kwa wazazi na ndugu wa bibiharusi; kama ilivyooneshwa hapa chini;

| | |
|---|---|
| *Mwekiketa shida mnatume ee,* | Mkipata shida mtoe taarifa, |
| *Ambu kaka wetu si mvivi,* | Kwani kaka yetu si mtu mbaya, |
| *Mama iyele iyele iyele ee, iyele iyele iyele x2,* | Mama iyele iyele ee, iyele iyele x2, |
| *Lukwi la kibare tukaote ee,* | Kuni za kuchana hutaota moto wake, |
| *Cho weneota ni makongoti x2.* | Moto utakaoota ni wa magunzi x2. |

Katika wimbo huu msisitizo upo katika kuonesha dhima ya ushirikiano na ukarimu, ambapo bwanaharusi huelezwa kwamba ni mtu mkarimu na yuko tayari kutoa ushirikiano na ukarimu kwa ndugu na wazazi wa bibiharusi. Nyimbo hutumiwa kuwahamasisha watu watende mambo fulani na pia nyimbo huwa na dhima ya kusisitiza ushirikiano na mshikamano katika jamii (Wamitila, 2004 na Mulokozi, 1996). Hivyo, kwa ujumla wimbo huu unasawiri dhima ya ukarimu na ushirikiano katika jamii ya Waasu.

Pia, wimbo wa ***Twahavache twaighuta*** *(Ahsante tumeshiba*) unahimiza na kubaini suala la ukarimu katika jamii hii:

| | |
|---|---|
| *Twahavache twahavache, twaighuta,* | Ahsante, ahsante tumeshiba, |
| *Vila tuorirwe ee,* | Vile tulivyokaribishwa, |
| *Esiighute atete aongejwe ee x2.* | Asiyeshiba aseme aongezawe ×2. |

Wimbo huu huimbwa na ndugu na jamaa wa bwanaharusi baada ya kushiba vyakula. Huonesha ukarimu waliopewa kutoka kwa wakwe zao. Katika jamii ya Waasu ukarimu ni suala linalopewa kipaombele. Mgeni akifika nyumbani hutakiwa kukarimiwa kwa hali ya juu, hususan mgeni maalumu. Wimbo huu husisitiza suala la ukarimu kwamba hata kama hujashiba unaongezewa chakula. Bernad (2002) anasema suala la ushirikiano na ukarimu ni miongoni mwa mambo yanayohimizwa na kupewa kipaombele katika sherehe nyingi za harusi za jamii. Uchambuzi wa data yetu katika kipengele hiki imejengewa wigo na kusawiri nadharia yetu ya uhalisia. Uhalisia unaelezea namna kazi ya fasihi inavyouwakilisha ulimwengu wa maisha ya jamii na hali halisi iliyomo (Moore, 1976). Hivyo basi, dhima zinazoelezwa katika nyimbo hizi ndio hali halisi iliyopo katika jamii ya Waasu hadi leo hii.

### 4.2.5 Kurekebisha Tabia

Katika jamii yoyote ile kuna utani na vijembe vinavyolenga kurekebisha tabia isiyotakiwa na kutoa mwelekeo fulani unaotakiwa na jamii. Nyimbo huwaelekeza na kuwafundisha vijana mwenendo mzuri na maadili yafaayo (Wamitila, 2004). Katika jamii ya Waasu suala la maadili na mienendo bora ni jambo linalosisitizwa. Wale wanaopotoka hurudishwa mstarini kupitia taasisi mbalimbali zikiwemo nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Miongoni mwazo ni wimbo wa ***Dada wetu tonga*** (Dada yetu nenda):

| | |
|---|---|
| *Dada wetu tonga,* | Dada yetu nenda, |
| *Dada wetu tonga eee x2,* | Dada yetu nenda ee*x2,* |
| *Uvavonye utanda eee,* | Uwaoneshe ustaarabu, |
| *Verugha makoko ee, veti ni mkate,* | Wanapika maboga wanadai ni mkate ee, |
| *Verugha viongwe veti ni vughai x2.* | Wanapika viazi vitamu wanadai ni ugali x2. |

Wimbo huu huimbwa na ndugu wa upande wa bibiharusi kabla hajaondoka nyumbani kwao. Hupiga vijembe kwamba, kwao upande wa bwanaharusi si wajuaji wa mambo mengi, hivyo basi, kwa kuwa binti yao ni mweledi sana akalete mabadiliko huko. Kila jamii ina mgawanyo wa majukumu kati ya mwanamke na mwanamume.

Kila upande hutakiwa kutimiza majukumu yake. Mojawapo ya majukumu ya wanawake katika jamii ya Waasu ni kushughulika na malezi ya watoto, usafi wa nyumba, kupika na shughuli za uzalishaji mali na uchumi. Mbogo (2008) anashadidia kwamba, mwanamke ambaye hana weledi wa kuzimudu kazi za usafi, kupika na malezi ya watoto hudharaulika na kama ameolewa ndoa huweza kuvunjika. Kwa hiyo wimbo huu una dhima ya kuwasema wasichana wenye tabia

mbaya ili wajirekebishe. Hii ndiyo hali halisi katika jamii ya Waasu, na ni wigo wa nadharia ya uhalisia.

Aidha, wimbo wa ***Emlanga kaka wetu kivivi nalifwe*** (Anayemsema kaka yetu vibaya afe) una dhima ya kuwasema watu wenye tabia mbaya za kuwasema watu, kuwasengenya na kuwafitini na tabia kama hizo, hususan kwa maharusi, ili wajirekebishe na kuziacha;

| | |
|---|---|
| *Emlanga kaka wetu kivivi nalifwe,* | Anayemsema kaka yetu vibaya afe, |
| *Emalanga wifi wetu kivivi nalifwe,* | Anayemsema wifi yetu vibaya afe, |
| *Vava wavo mwana lukundo ni mari,* | Baba mtoto upendo ni mali, |
| *Usighoje kuvona mwenye unevona,* | Usisubiri kuona mwenyewe utaona, |
| *Chekihera tunechinja kagonji na mwana.* | Ikishindikana tutachinja kondoo na mtoto wa kondoo. |

Wimbo huu huelezea juu ya watu wenye tabia ya kusengenya, wivu, vijicho na kusema wengine, kwamba wajirekebishe na hasa dhidi ya maharusi. Pia, hulaani kuwa mwenye tabia hizo mbaya afe au apatwe na mabaya. Tabia ya wivu na hata kumsema mtu vibaya ni vitu visivyotakiwa katika tamaduni mbalimbali katika jamii (Samwel na wenzake, 2013). Hivyo, tabia hizi hupigwa vita kupitia taasisi mbalimbali za kijamii zikiwamo nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Kwa ujumla, wimbo huu una dhima ya kuwataka watu wenye tabia mbaya dhidi ya wenzao waziache na kusisitiza kutowasema au kuwasengenya maharusi, badala yake husisitiza tabia njema kama vile upendo.

Aidha wimbo wa ***Ena picha yakwe kaka ahundue*** (Aliye na picha yake kaka arudishe) huendelea kusisitiza na kuwataka watu wenye tabia mbaya zisizotakiwa katika jamii dhidi ya maharusi wajirekebishe, kama waimbaji wanavyoimba;

| | |
|---|---|
| *Ena picha yakwe kaka ahundue,* | Aliye na picha yake kaka arudishe, |
| *Ambu kaka aovoa x3,* | Kwa sababu kaka ameoa x3, |
| *Mvwi wedi tuuikaa he iziaka,* | Mshale mzuri haukai kwenye podo, |
| *Yoo chakulok , kaka apata mshorwa.* | Leo yametimia, kaka amepata mrembo. |

Kimsingi wimbo huu nao una dhima ya kurekebisha tabia. Huwasema wasichana waliokuwa na uhusiano au waliokuwa wanamtaka bwanaharusi kimapenzi waache mara moja kwa sababu amepata mke. Wimbo huu unakemea tabia hiyo kwa kuwa haitakiwi katika jamii. Naye Mlokozi (1996) anasema nyimbo zenye maadili ya kuonya ziliimbwa na makabila yote Afrika, zikikusudia kuwaasa vijana na watoto. Kimsingi, bwanaharusi na bibiharusi hawatakiwi kuhangaika na kutoka nje ya ndoa yao, badala yake waitunze na kuiheshimu kwa kadri wanavyoweza. Uaminifu katika ndoa hujenga ndoa imara na endelevu.

Katika jamii ya Waasu, ndoa ni jambo linaloheshimiwa sana kwa kuwa ni nyenzo inayoendeleza uzazi na uendelevu wa jamii yao. Kuingilia ndoa ya mtu hutazamwa kama kosa kubwa lisiloweza kusamehewa kwa urahisi (Mturo, 2011). Adhabu kali za kisheria na kimila huchukuliwa kwa yeyote anayepatikana na kosa hilo. Kwa hiyo, ndoa imara hutazamwa kama msingi wa ustawi wa familia na jamii. Mafunzo na maonyo mengi kuhusu ndoa hutolewa kupitia taasisi mbalimbali za kijamii, ikiwemo nyimbo za harusi za jamii hiyo.

### 4.2.6 Kuonesha Masikitiko na Uvumilivu

Hii ni dhima nyingine inayojitokeza katika nyimbo za harusi katika jamii za Waasu. Data yetu inaonesha kwamba, masikitiko na uvumilivu huo hulengwa kwa mama wa bibiharusi, bibiharusi, ndugu wa bibiharusi pamoja na bwanaharusi. Baadhi ya

nyimbo zilizoonesha dhima hii ni ule wa ***Mama wemanyire*** (Mama ulizoea), kama ulivyobainishwa hapa chini;

*Mama wemanyire ee, mwana ee,*
*Ja mazi ja mazi, uoje viombo,*
*Iki atonga ee mama ee, uneja mazi mwenye uoje viombo,*
*Mama wemanyire mwana ee chavanga, chavanga, uturije mhunga,*
*Iki atonga ee mama ee unechavanga mwenye, uturije muhunga.*

Mama ulizoea binti ee, kateke maji, kateke maji, uoshe vyombo,
Sasa ameenda ee, mama ee, utateka maji mwenyewe uoshe vyombo,
Mama ulizoea ee, binti ee, lima lima, uoteshe mpunga,
Sasa ameenda ee, mama ee, utalima mwenyewe, uoteshe mpunga.

Wimbo huu huelekezwa kwa mama mzazi wa bibiharusi, huonesha maskitiko yake kwa binti yake kuondoka nyumbani kwake. Kimsingi, humtaka kuwa mvumilivu kutokana na uchungu wa binti yake kuondoka nyumbani kwake na kuolewa. Huelezea zaidi kwamba alikuwa amemzoea katika majukumu na kumtuma kazi mbalimbali kama vile kuteka maji na kuosha vyombo, na hata kazi za uzalishaji mali na uchumi. Wamitila (2004) anaeleza kwamba nyimbo za harusi huandamana na sherehe za ndoa, na kwamba zipo jamii zinazotumia nyimbo hizi kuonesha maskitiko ya kuhama nyumba moja kwenda nyingine.

Kimsingi, maskitiko haya huyamhusu bibiharusi peke yake, bali mama yake mzazi na hata ndugu zake waliokuwa wamemzoea. Nadharia ya uhalisia inaeleza kwamba kazi ya kifasihi lazima isawiri hali halisi zilizopo katika jamii (Moore, 1976). Hivyo basi, nadharia hii imeweza kuweka mwigo mzuri wa kitaaluma katika wimbo huu na kazi yetu kwa ujumla.

Kwa namna nyingine, pia wimbo wa ***Mama chunga idafa*** (Mama jikaze/funga mkanda) nao unaelezea dhima ya uvumilivu kwa mama mzazi wa binti anayeolewa. Kama ilivyobainishwa hapa;

| | |
|---|---|
| *Chunga idafa, mama wavo (jina la binti),* | Jikaze, jikaze, mama (jina la bibi harusi), |
| *Chunga idafa mwana etetonga x3.* | Jikaze mtoto anaekwenda x3. |

Wimbo huu humlenga mama mzazi wa bibiharusi, kuelezea maskitiko yake, ukimwomba kuwa na uvumilivu kwa sababu binti yake anaolewa. Kwa hiyo utapata upweke na msaada aliokuwa anaupata kutoka kwake kama vile kumsaidia kuchota maji, kuosha vyombo na kulima hataupata tena. Maneno ñ*Chunga idafa*ò humaanisha mama mzazi kutakiwa ajifunge mkanda (jani la mgomba) yaani kujikaza na kuwa mvumilivu kwani binti yake anaenda kwa mumewe. Kwa ujumla, nyimbo hizi hulenga kumuomba mama mzazi wa bibiharusi kuwa mvumilivu na kuanza kuzoea maisha mapya.

Katika nyimbo za harusi za Waasu, suala la maskitiko na uvumlivu halimlengi mama mzazi wa bibiharusi tu, bali hata bibiharusi mwenyewe. Hii ni kutokana na kuolewa hivyo kutengana na familia yake. Suala hili hujibainisha katika wimbo wa ***Aiyaiya kuolewa;***

Aiya iya kuolewa utarudi nyumbani kutembea,
Kwa heri mama na baba kuonana majaliwa,
Aiya iya kuolewa utarudi nyumbani kutembea (korasi),
Kwa heri kaka na dada kuoanana majaliwa.

Wimbo huu una dhima ya kumtaka bibiharusi kuwa na uvumilivu, kwamba anaondoka nyumbani kwao na kuachana na wazazi wake na nduguze. Husisitiza kwamba anatakiwa azoee na kwamba kurudi nyumbani kwao itakuwa ni kwa madhumuni maalumu au kusalimia tu. Wimbo huu huelezea na kuonesha masikitiko hayo kwa binti anayeolewa. Kwa kawaida, nyimbo hulenga kumwandaa bibiharusi kisaikolojia namna ya kuyamudu mazingira na maisha mapya ya kindoa (Mohamed, 2004). Aidha, wimbo wa ***Mshigheni atonge ee*** (Mwacheni aende ee) humtaka bibiharusi kuwa mvumilivu katika maisha ya ndoa:

| | |
|---|---|
| *Mshigheni atonge ee,mshigheni atongeee,* | Mwacheni aende ee, mwacheni aendeee, |
| *Mshigheni atonge, arevona vwasi vya ijumba x2,* | Mwacheni aende, akaone taabu za unyumba ×2, |
| *Ijumba telijinkwa, mavwasi gumirija x2,* | Unyumba haukimbiwi taabu zivumilie ×2. |

Wimbo huu huimbwa pindi bibiharusi anapokuwa njiani kuelekea kwa bwanaharusi. Huwa na dhima ya kumtaka kuwa mvumilivu kwani ndoa ina changamoto na wakati mwingine shida nyingi. Kwa upande mwingine humwandaa kisaikolojia bibiharusi kukabiliana na changamoto na shida za ndoa na kuzivumulia kwa kadiri atakavyoweza. Ndoa si jambo jepesi, huhitaji kukabiliana na harakati zake za kila siku katika jamii (Uta na Roland, 2006). Kwa msingi huo, ndoa si ya kuikimbilia kabla ya kukomaa kikamilifu kimwili na kiuchumi. Aidha, si kuikimbia ndoa baada ya kupata changamoto kadhaa, bali hutakiwa uvumilivu. Kwa hiyo, wanandoa hawana budi kuvumiliana pindi matatizo au changamoto zinapotokea. .

### 4.2.7 Kuonya

Jamii yoyote ile inapoona kuna tabia, mienendo au mambo yanayoonekana kuelekea kuleta matatizo katika ustawi wa jamii, jambo la kwanza ni kutoa maonyo kwa wahusika. Katika utafiti huu, pia kuna nyimbo zinazolenga hutoa maonyo mbalimbali kwa walimwengu. Nyimbo hizo husisitiza suala la uaminifu na kuheshimu ndoa zao na watu wengine katika jamii. Kwa upande mwingine, nyimbo hizi huwa na dhima ya kutoa onyo kwa wale wote wanaowatazama maharusi kwa kuwamezea mate. Tabia ya kuingilia ndoa ya maharusi hukemewa kwa nguvu zote katika jamii nyingi hapa nchini (Meena, 1995). Vilevile nyimbo hizi hubeba dhima kwa maharusi kuachana na wapenzi wa zamani kama walikuwa nao. Jambo hili linaelezwa kwa kina katika wimbo wa ***Ena picha yakwe kaka ahundue*** (Aliye na picha yake kaka arudishe).

| | |
|---|---|
| *Ena picha yakwe kaka (jina la bwana harusi) ahundue* | Aliye na picha ya kaka (jina la bwanaharusi) arudishe, |
| *Ambu kaka aovoa x3.* | Kwa sababu kaka ameoa ×3. |

Wimbo huu huwa na dhima ya kutoa maonyo dhidi ya binti yeyote aliyekuwa anamfuatafuata bwanaharusi ili amwache kwa kuwa bwanaharusi amepata mke. ***Picha ya kaka*** hutumika kama lugha ya kiishara ikiwa na maana mwenye mawasiliano na bwanaharusi, hasa yaliyokuwa yanalenga mahusiano ya kimapenzi akome mara moja. Kwa upande wake Pembe (2013) anaeleza kwamba, nyimbo zina dhima nyingi zinazolenga kuiadili, kuionya na kutahadharisha jamii ili ifuate maadili yafaayo.

Pia, katika wimbo wa ***Emlanga kaka wetu kivivi*** (Anayemsema kaka yetu vibaya), suala la kusengenya, kuheshimu na kutoingilia ndoa linaelezwa:

| | |
|---|---|
| *Emlanga kaka wetu kivivi nalifwe,* | Anayemsema kaka yetu vibaya na afe, |
| *Emalanga wifi wetu kivivi nalifwe,* | Anayemsema wifi yetu vibaya na afe, |
| *Vava wavo mwana lukundo mari,* | Baba yake kijana upendo ni mali, |
| *Usighoje kuvona mwenye unevona,* | Usisubiri kuona utaona mwenyewe, |
| *Chekihera tunechinja kagonji na mwana.* | Ikishindikana tutachinja kondoo na mtoto wake. |

Wimbo huu hutoa maonyo kwa walimwengu wote wenye nia mbaya na maharusi; bibiharusi na bwanaharusi na hutoa laana kwao. Dhima hii ni muhimu kwani kwa kawaida vijana wanapooana maadui wengi hujitokeza wakinuia kuwakwamisha kwa njia ya kuwasema, kuwasengenya, pamoja na kuzua umbea unaolenga kuwafarakanisha. Mojawapo ya dhima ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu ni kuutangazia umma na kuutahadharisha kwamba bibi na bwanaharusi wameoana. Aidha, kufanyika kwa harusi kunatazamawa kama muhuri unaohalalisha uhusiano na maisha ya kindoa miongoni mwa wanaooana. Huu ndio msingi wa nadharia ya Uhalisia inayoelezea namna kazi za kifasihi zinavyouwakilisha ulimwengu wa maisha na hali halisi iliyomo katika jamii (Moore, 1976). Hivyo, jamii inatakiwa kuwasaidia maharusi na anayelenga kuwakwamisha hupewa maonyo na hupigwa vita na jamii nzima. Kinyume chake jamii husisitiza umuhimu wa umoja, upendo na ushirikiano kwa maharusi na jamii kwa ujumla.

Dhima ya maonyo haiwalengi walimwengu tu, bali pia hata maharusi. Huonywa juu ya kushikamana, kwamba bwanaharusi anatakiwa amshike mkewe vizuri, vivyo hivyo kwa upande wa bibiharusi. Wimbo wa ***Kaka mgure mkono kidinde*** (Kaka mshike mkono kisawasawa) hujihirisha hoja hii;

| | |
|---|---|
| *Kaka mgure mkono kidinde* | Kaka mshike mkono kisawasawa |
| *Kaka ee mgure mkono kidinde* | Kaka ee mshike mkono kisawasawa |
| *Uo niye wako wa maisha x2* | Huyo ni wako wa maisha×2 |

Wimbo huu huwataka maharusi kushikamana ili kusaidia kuziba mianya ya maadui wa ndoa. Hivyo, huonywa na kuhimizwa ili washikamane kila wakati, hususan mwanume kuwa karibu na mkewe wakati wote. Wimbo huu humweleza bwanaharusi kumshika mkewe mkono imara, ikiwa na maana kuwa karibu naye wakati wote, ili mafisadi wasiweze kumnyemelea na kumrubuni kimapenzi. Pia, humwonya kutotoka nje ya ndoa. Kwa namna nyingine, wimbo huu humsisitiza bwanaharusi kushikamana na mkewe maisha yake yote ya ndoa. Hivyo kwa ujumla wimbo huu huhusika na dhima ya maonyo kwa maharusi (bwanaharusi)

Kimsingi suala la mshikamano wa wanandoa ni jambo muhimu katika kudumisha na kustawisha ndoa. Jambo hili husistizwa sana katika mila na utamaduni wa Waasu. Kwa upande mwingine wimbo wa ***Vaisanga vena ngoro mbivi*** (Walimwengu wana roho mbaya) hujikita katika kutoa onyo kwa watu walio na tabia za kukwamisha mambo ya watu (ndoa/uchumba);

| | |
|---|---|
| *Vaisanga vena ngoro mbivi, vekitie kinehera ee x2,* | Walimwengu wana roho mbaya walidhani itashindikana ×2, |
| *Vaisanga vena ngoro mbivi ee, vekitie kinehera,* | Walimwengu wana roho mbaya ee, walidhani itashindikana, |
| *Vapate cha kuteta, mira iki chakuloka,* | Wapate cha kusema, lakini sasa imetimia, |
| *Cha kuteta chasoveka* | La kusema limekosekana. |

Wimbo huu hutoa maonyo kwa walimwengu juu ya kuharibu uchumba wa watu. Huonesha kwamba katika mchakato wa kuoa na kuoelewa wahusika hukumbana na

changamoto nyingi zenye nia ya kuwakwamisha. Wimbo huu huimbwa kuwaonya wote wenye roho mbaya kama hizi waziache. Huelezea kwamba walikuwa wanataka ishindikane ili wafurahi na wapate la kusema lakini wameshindwa, hawana la kusema au la kufanya tena. Hivyo basi, katika jamii ya Waasu tabia hii ya kukwamisha mambo ya watu huchukiwa na haifumbiwi macho. Hali hii inasawiri nadharia yetu ya uhalisia kama ilivyoelezewa na waalamu kama vile; Moore, (1976), Wafula na Njogu (2007) na Spurlin & Fischer (1985); ambayo hujikita katika kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uhalisia wa maisha. Aidha, uhalisia humaanisha uwakilishi wa hali na uhalisi wa mambo ya kijamii yanavyojidhihirisha katika fasihi.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii tumeshughulikia lengo letu la kwanza lililolenga kufafanua dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Baadhi yake zinahusu kusisitiza masuala ya upendo, heshima na pongezi kwa maharusi. Dhima nyingine zinazojitokeza zaidi katika nyimbo za harusi za Waasu ni; kuonesha ukarimu na ushirikiano, kurekebisha tabia na kuonesha maskitiko na uvumilivu pamoja na kuonya. Hali hiyo huipa jamii uelewa mpana wa kuyatambua na kuyatawala kikamilifu maisha ya kindoa katika mazingira yao. Sura inayofuata inahusu usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu.

# SURA YA TANO

# USANAA WA LUGHA KATIKA KUJENGA DHIMA ZA NYIMBO ZA HARUSI ZA JAMII YA WAASU

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii ya tano tumefafanua data zilizolenga kukamilisha lengo mahsusi la pili. Lengo hilo lilikusudia kuchunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi za Waasu. Kazi ya kifasihi hujengwa kwa kutumia vipengele mbalimbali vya kifani - vya lugha. Kulingana na Kingꞌei (2002), matumizi bora ya vipengele vya lugha hujenga mvuto wa kisanaa unaomfanya msomaji au msikilizaji awe makini na kuweza kuifuatilia kazi inayohusika. Aidha, sura hii nayo imegawanywa katika vipengele vidogovidogo vya usanaa husika wa lugha. Kila kipengele kimefungamanishwa na nyimbo kinazozisawiri. Vipengele hivyo vya usanaa wa lugha vimepewa majina ili kusaidia pale urejelezi ulipohitajika iwe rahisi.

## 5.2 Usanaa wa Lugha katika Kujenga Dhima za Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasu

Lugha ni kipengele muhimu sana kinachotofautisha sanaa ya fasihi na sanaa nyingine. Fasihi ya Kiswahili ina utajiri mkubwa uliojilimbikiza katika vipengele vya lugha (Armitt, 2005). Lugha ndicho chombo cha mawasiliano ambayo huhitilafiana kulingana na mazingira pamoja na utamaduni wa jamii inayohusika. Mawasiliano hufanywa kisanaa katika kazi za kifasihi kwa kuzingatia muktadha mahsusi wa jamii (Kiganza, 2011). Kulingana na Wamitila (2004), usanaa ni ufundi anaoutumia msanii kuiumba kazi ya kifasihi na kuifanya ivutie na kuwa na athari kwa msomaji, msikilizaji au mtazamaji. Maelezo haya yanatoa mwelekeo maalumu unaousukuma

mbele utafiti huu (katika kipengele hiki) uliolenga kuchunguza usanaa wa lugha katika kujenga dhima katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu.

Katika kipengele cha matumizi ya lugha tumechunguza usanaa uliojibainisha katika tamathali za semi kwa kuziweka katika muktadha mpana wa jamii iliyochunguzwa. Kimsingi, tamathali za semi huburudisha na kuzindua akili ya msomaji au msikilizaji na kuacha athari ya kudumu katika hisi na mawazo yake (Ngure, 2010). Vile vile mbinu nyingine za usanaa wa lugha kama vile methali tumeziangalia. Mjadala ulilenga kubaini usanaa wa lugha unavyosaidia kujenga dhima katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Baadhi ya vipengele vya lugha vilivyojadiliwa katika sehemu hii ni jazanda, taswira na ishara, chuku, takiriri, tashibiha, methali na dhihaka.

### 5.2.1 Jazanda

Ntarangwi (2004:104) anasema jazanda ni mafumbo ambamo maana ya kitu imefichika. Anaeleza kwamba, wakati mwingine mwandishi huwa anawapatia wasomaji wake kazi ya kutafuta na kungĀmua maana ya kitendo au hali fulani au kisa kwa kutumia fumbo au kwa kutumia jambo ambalo laelekea kuwa la kawaida lakini kumbe pana ujumbe uliofichika. Anaendelea kusema kwamba kwenye jazanda unaweza kutumia maneno au visa ambavyo kwa msingi ni vya kawaida kumbe visa vinatoa ujumbe mwingine, ambao umefumbwa kama jazanda. Kwa hiyo, jazanda ni matumizi ya lugha ya mafumbo. Kwa upande wake Senyamanza *(?)* anaelezea jazanda kwamba ni mbinu ya matumizi ya lugha kwa njia ya kufumba ujumbe. Huendelea kueleza zaidi kwamba mbinu hii hulenga kumfikirisha msomaji

au msikilizaji ambapo ugunduzi wa ujumbe huo huufanya ujumbe kupatikana kwa nguvu zaidi.

Baadhi ya wataalamu wengine wameshindwa kuitofautisha vyema jazanda na sitiari, huzielezea kama kitu kimoja (Senyamanza (kesht.). Wataalamu wengine kama vile Wamitila (2004, 2016) huelezea jazanda na taswira/picha kama kitu kimoja. Kimsingi, taswira ni matumizi ya lugha inayojenga picha fulani katika akili ya msomaji/msikilizaji. Kwa upande wake sitiari ni uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine tofauti, wakati jazanda ni lugha ya mafumbo. Ntarangwa (kesht.) anasema dhana ya jazanda mara nyingi huchukuliwa kama taswira, ukweli ni kwamba, taswira ni picha zinazoundwa kichwani mwa msomaji au msikilizaji kutokana na maelezo ya mtunzi.

Wamitila (2004) anaeleza kwamba, mafumbo ni lugha ya kificho inayotumiwa kwa lengo la kuelezea kauli fulani ambapo ili maana ipatikane huhitajia hadhira au mlengwa kufikiria kwa kina. Fikira hizi za kina husaidia kuleta athari chanya na kubwa kwa walengwa. Mafumbo hutumiwa kuelezea kauli ambazo huficha maana fulani, huwa na jambo ambalo limefumbwa ambalo msikilizaji anahitajika kufumbua (Msokile, 1992).

Mojawapo ya nyimbo za harusi zilizotumia mbinu hii ni ***Ena picha yakwe kaka ahundue*** (Aliye na picha yake kaka arudishe) kama ilivyobainisha hapa chini;

| | |
|---|---|
| *Ena picha yakwe kaka (jina la bwana harusi) ahundue,* | Aliye na picha ya kaka (jina la bwanaharusi) arudishe, |
| *Ambu kaka wetu aovoa x3.* | Kwa sababu kaka yetu ameoa. |

Wimbo huu humaanisha wale wote waliokuwa na uhusiano wa kimapenzi au waliokuwa wanamtaka kimapenzi bwanaharusi wakome mara moja kwa kuwa amepata mke. Neno ñpichaò ni fumbo ambalo linamaanisha *uhusiano wa kimapenzi*. Kimsingi, ufundi huu wa lugha huibua fikira ambayo huleta athari chanya kwa walengwa, na kusaidia kuwatahadharisha walimwengu kutowataka tena maharusi kimapenzi. Kwa hiyo, wimbo huu umesaidia katika kujenga na kutia nguvu dhima ya kuonya katika nyimbo za harusi za Waasu.

Aidha, wimbo wa ***Chunga idafa*** (funga mkanda) ambao unasisitiza hali ya kujenga uvumilivu kwa mama wa bibiharusi, bibiharusi mwenyewe na nduguze kama inavyoelezwa unatummia jazanda ambayo ni ñidafaò:

| | |
|---|---|
| *Chunga idafa, mama wavo mwana (jina la binti),* | Funga mkanda (jani la mgomba), mama, wa mtoto (jina la binti), |
| *Chunga idafa* | Funga mkanda (jani la mgomba), |
| *Mwana etetonga x2* | Mtoto anakwenda Ξ2. |

Maneno ***chunga idafa*** kama ilivyotafsiriwa kwa Kiswahili hapo juu ni lugha ya mafumbo, ambayo humaanisha kuwa mama mzazi wa binti hana budi kujifunga mkanda kiunoni, yaani kuvumilia hali ya maisha ya baada ya bintiye kuolewa na kumuacha. Usanaa wa lugha uliotumika hapa umechangia pakubwa kujenga na kushadidia suala la uvumilivu.

Maneno ñchunga idafaò yaani kujifunga mkanda (jani la mgomba) ni jazanda; humanisha uvumilivu. Hali hii husawiri nadharia yetu ya simiotiki, inayoelezea dhana ya kiashiria na kiashiriwa; kwamba kila kiashiriwa huwa na kiashiria chake.

Aidha huelezea zaidi kwamba mtunzi wa kazi za kifasihi huunda alama hizi kufuatana na utamaduni wa jamii yake, na kwamba alama hizi hueleweka kwa wanajamii hao na kuzitumia katika mawasiliano yao ya siku hadi siku. Cameroon (1985) anasema ishara zinazojitokeza katika fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii. Jamii ya Waasu ni wakulima ikiwemo kilimo cha migomba, kwa hiyo, migomba na kila kitu chake ni sehemu ya utamaduni wao. Hivyo alama hizi hutengenezwa na wanajamii hii kwa kuzingatia utamaduni na muktadha wao.

Aidha wimbo wa ***Lubegho lwa mwana luwaja*** (uchungu wa mtoto unauma) umejengeka kwa kutumia mbinu za kisanaa za jazanda kwa kiasi kikubwa katika kusaidia ujenzi wa dhima yake ya kusisitiza heshima kwa wazazi;

| | |
|---|---|
| *Lubegho lwa mwana luwaja,* | Uchungu wa mtoto unauma |
| *Aheee luwaja x2,* | Aheee unauma ×2, |
| *Luwaja kangi ugure kikwidi i,* | Unauma mpaka ushike kiuno ee, |
| *Aheee luwaja,* | Aheee unauma, |
| *Luwaja kangi ugure ndeni i,* | Unauma mpaka ushike tumbo ee, |
| *Aheee luwaja*, | Ahee unauma, |
| *Luwaja kangi ugure mtwi i*, | Unauma tena ushike kichwa ee, |
| *Aheeee luwaja* . | Ahee unauma. |

Wimbo huu umetumia jazanda kwa kiasi kikubwa. Maneno haya *Lubegho lwa Mwana Luwaja* (uchungu wa mtoto unauma) humaanisha wajibu wa watoto kuwaheshimu wazazi, kutokana na kulelewa kwa shida na uchungu mwingi. Wimbo huu umesaidia kujenga dhima ya kuheshimu wazazi na kumtunza binti anayeolewa kwani amezaliwa na kulelelwa kwa taabu na shida. Ntarangwi (2004) anasema msanii anaweza kutumia maneno au visa vya kawaida, kumbe vina maana nyingine ambayo imefumbatwa kwenye jazanda. Naye, Senyamanza (?) anasema jazanda

huwa na maana mbili, maana ya juu na ya ndani. Hueleza zaidi kwamba maana ya ndani ndiyo inayokuwa na nguvu zaidi. Kimsingi jazanda hunuia kuchochea na kuibua fikra kwa msomaji au msikilizaji. Mbinu hii huibua fikira nzito kwa walengwa (maharusi) zinazowajenga na kuwaimarisha kindoa kwa kuzingatia heshima.

Kwa upande mwingine, usanaa wa lugha (jazanda) unajidhihirisha katika wimbo wa ***Wifi unatete mphoa*** (wifi uwe na upendo) ambao unasisitiza suala la umuhimu wa upendo na adabu kwa ndugu na jamaa katika jamii. Pia, humaanisha mwali anatakiwa kuongea vizuri na watu na kuwa mkarimu ili apate marafiki na kupewa ushirikiano. Kwa upande wa pili, maneno *"kangi wekiteta nyaka hako ni njia ya mivwa"* humaanisha kama mwali atajiona na kujivuna basi nyumbani kwake hakuna atakayefika, atakosa marafiki. Maneno *Nzia ya mivwa* (njia ya miiba) ni jazanda inayomaanisha sehemu mbaya inayokwepwa na watu kuipitia; watu huiogopa kwa sababu miiba hiyo huweza kuwachoma na kuwaumiza. Maana yake ni mtu mbaya na mchoyo ambaye kila mtu humkwepa na kumkataa. Pia maneno *"haharwe kajoto"*(kuombwe moto) humaanisha ukarimu na ushirikiano. Kwa ujumla, matumizi ya lugha ya mafumbo, ambayo humhitajia mtu kufikiri ili kuweza kupata maana iliyokusudiwa na mtunzi yamesaidia pakubwa katika kujenga dhima ya ukarimu na ushirikiano ambayo ndiyo dhima kuu iliyobebwa na nyimbo hizi.

Kwa mujibu wa data yetu ya utafiti jazanda zilizotumika hueleweka kwa jamii ya Waasu kwa kuhusisha utamaduni, uchumi, falsafa na mazingira yao. Kulingana na Cameron (1985), alama zinazojitokeza katika fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii; na binadamu ndiye mtengenezaji wa alama

mbalimbali za ishara ambazo huzitumia katika mawasiliano yake ya kila siku. Hali hii inasawiri ndharia yetu ya simiotiki inayosisitiza suala la ishara na uashiriaji, kwamba katika kazi za fasihi mtunzi huuunda ishara mbalimbali kufuatana na muktadha na utamaduni wa jamii. Kimsingi ishara hizo hutafsirika na hueleweka kwa wanajamii hao.

### 5.2.2 Ishara

Ishara ni neno linalotokana na kuashiria; yaani kitu kimoja kuashiria au kuwakilisha kitu kingine. Kavuna na wenzake (2003:23) wanaeleza kwamba ishara ni picha ambazo zinaweza kujengwa na fanani katika kutoa ujumbe wake. Picha hizo hutokana na uteuzi wa maneno ya mwandishi katika kukifananisha kitu anachozungumzia na ukweli wa maisha. Kimsingi, ishara nyingi hufungamana na utamaduni wa jamii na mazingira yake. Kwa ujumla ishara ni kitu kinachosimama kuwakilisha sifa ya kitu kinachohusika au kusimama kuwakilisha kitu kingine.

Naye Samwel na wenzake (2013) anaelezea lugha ya ishara kuwa ni lugha inayobeba dhana zinazotumika kuwakilisha kitu/maana nyingine. Hueleza zaidi kwamba, ishara moja huweza kuwa na maana hii katika jamii moja na ishara hiyo hiyo kuwa na maana nyingine katika jamii nyingine. Anachomaanisha mtaalmu huyu ni kwamba ishara hujikita katika utamaduni wa jamii husika. Jamii ya Waasu ina ishara mbalimbali zinazosawiriwa kupitia lugha yake. Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zimejengwa katika ishara mbalimbali.

Katika wimbo ***Kasanga kahavo kahuyuka*** (kijijini kwao kumepwaya), maneno *viagho* (sangare) na *mabange* (mimea inayofanana kama bangi) kwa mujibu wa

jamii ya Waasu, ni majani yasiyo na thamani. Maneno hayo huashiria kijiji anachotoka bibiharusi kuwa ni sawa na kitu kisicho na thamani tena baada ya bibiharusi kuchukuliwa. Hii ina maana bibiharusi huyo ndiye aliyekuwa analeta thamani hapo kijijini na nyumbani kwao kwa ujumla. Hivyo, maneno hayo yanaashiria thamani ya bibiharusi. Kwa upande wa pili, maneno *majighu* (ndizi mshale) na iliki haya ni mazao yenye thamani miongoni kwa jamii ya Waasu. Maneno haya huashiria kwamba, anakokwenda mwali kumekuwa na thamani, yaani amepafanya kuwa na thamani.

Hivyo, maneno haya huashiria uzuri wa kitu, hali au jambo na hujennga picha fulani katika vichwa vya wasikilizaji, ambao hupata maana kutokana na uakisi wa mazingira yao, mila na utamaduni na uchumi wa jamii ya Waasu. Hali hii inasawari nadharia yetu ya simiotiki, kwamba kila jamii huunda ishara kufuatana na utamaduni wake, na ishara hizo huwa na maana kwao. Aidha Eco (1976) hufafanua zaidi kwamba simiotiki ni mfumo wa alama (ishara) katika mawasiliano ya kutumia lugha. Usanaa wa lugha uliotumika hapa umesaidia kujenga dhima ya kuwasifu na kuwapongeza maharusi.

Katika wimbo ***Hiyo pete yetu naitoke*** maneno ñpeteò na ñkiooò ni lugha ya ishara. Pete na kioo huashiria kitu cha thamani na kinachotakiwa kushikiliwa kwa uangalifu na kutunzwa. Wimbo huo umesaidia katika kujenga na kuwezesha dhima ya kuwasifia maharusi (kumsifia bibiharusi). Kwa upande mwingine, maneno haya huleta taswira Fulani zinazoibua fikra nzito na kuwa na athari chanya kwao. Matumizi ya lugha ya ishara husaidia katika kuleta athari chanya na nzito katika

nyimbo, hivyo upokezi wa dhima za nyimbo hizo kuwezekana kwa kiasi kikubwa (Perpetua, 2011).

Katika wimbo wa ***Mama chunga idafa (***mama jikaze/funga mkanda) kuna matumizi ya lugha ya ishara. Maneno haya huelezea uvumilivu kwa mama, kwamba anatakiwa avumilie na aanze kuzoea maisha mapya nje ya bintiye kwa kuwa anaolewa. Maneno ñchunga idafaò humaanisha kujifunga mkanda, yaani kuashiria kujikaza na kuvumilia. Maneno hayo kwa upande mwingine, hujenga taswira fulani akilini mwa wasikilizaji, na kuibua fikira zinazosaidia kueleza uvumilivu. Kimsingi, uibukaji wa fikira hizo huwahusu wazazi na ndugu wa bibiharusi, hususan mama mzazi kwamba wazoee maisha mapya, na kwamba katika maisha kuna mambo yanatokea wanatakiwa kuyavumilia.

Hivyo basi, lugha ya ishara iliyotumika katika wimbo huu imesaidia sana katika kujenga dhima ya uvumilivu inayobebwa na wimbo huu, na kuufanya kuwa na athari chanya kwa walengwa wake. Kimsingi, usanaa wa lugha ndio unaozifanya nyimbo kuwa na ufasihi unaosaidia katika kujenga dhima inayokusudiwa katika kazi za kifasihi kama ilivyojidhihirisha katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Naye Maganga (1996), anaeleza kwamba matumizi ya usanaa wa lugha kama vile lugha ya ishara ndio unaozifanya nyimbo kuwa na ufasihi na athari chanya kutokana na dhima iliyokusudiwa.

### 5.2.3 Takriri

Takriri pia huitwa *inadi* au *uradidi* (Samwel na wenzake, 2013). Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema kuwa takriri ni urudiaji wa sauti, neno, kirai, kishazi au

hata sentensi katika kazi ya fasihi. Wanaeleza kwamba kuna aina mbalimbali za takriri kama vile; takriri irabu, konsonanti, vina, takriri neno na takriri mstari. Ama kuhusu dhima ya takriri ni kusisitiza dhamira, ujumbe au jambo liongelewalo na kuifanya hadhira imakinike nalo. Mbinu hii imetumika katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano, katika wimbo wa ***Twahavache twaighuta*** (ahsante tumeshiba) unaeleza na kusisitiza kuhusu umuhimu wa shukrani. Kwa mfano:

*Twahavache twahavache, twaighta vila tweorirwe ee*
Ahsante asante, tumeshiba vile tulivyokaribishwa

Katika wimbo huu maneno *"twahavache twahavache"* (ahsante ahsante) ni takiriri, neno limerudiwa. Mbinu hii imesaidia katika kujenga dhima ya wimbo huu ambayo ni ukarimu. Usanaa huu wa lugha kwa mujibu wa data yetu umesaidia pakubwa katika kujenga dhima hii na kuonesha jinsi suala la ukarimu na shukrani linavyopewa umuhimu katika jamii ya Waasu. Aidha ukarimu huendana na shukrani, ukikarimiwa huna budi kushukuru, hivyo takriri hii inaonesha matokeo ya ukarimu na msisitizo wake. Hawkes (1977) akishadidia nadharia ya simiotki anasema matumizi ya baadhi ya mbinu za kifani na kimaudhui katika kazi za fasihi si ya kibahati nasibu bali yana maana katika kazi zinazochunguzwa. Aidha takiriri ni mojawapo ya mbinu za kifani katika kazi za kifasihi, hivyo yana maana, ambayo ni kusisitiza maudhui lengwa.

Kwa upande mwingine takriri imejitokeza katika wimbo wa ***Anameremeta*** ikiwa na dhima ya kusisitiza sifa kwa maharusi (bibiharusi);

Anameremeta, anameremeta ᅲ2
Mwali wetu anameremeta, anameremeta ᅲ2
Nguo zake zinawaka waka, zinawaka waka ᅲ2
Zinawaka waka, zinawaka waka ᅲ2

Katika wimbo huu kuna takiriri neno ambapo neno ***anameremeta*** limerudiwa rudiwa katika mshororo wa kwanza na wa pili. Pia neno ***zinawakawaka*** limerudiwa katika mshororo wa tatu na wa nne. Takriri hii husisisitiza dhima ya kuwapongeza maharusi (uzuri wa bibiharusi), humwelezea kwamba anameremeta yaani ni mzuri sana. Kwa upande wa nguo zake huelezea kwamba zinawakawaka; kumeremeta na kuwakawaka kwa ujumla husisitiza suala la uzuri na urembo wa bibiharusi. Kimsingi katika jamii ya Waasu ili uolewe unatakiwa uwe na sifa nyingi; mojawapo ni urembo. Msichana asiye mrembo na asiyejipenda kimsingi anapungukiwa na sifa za kupata mchumba/mume na mwenye nia ya dhati ya kutaka kumuoa (Howe na Bryceson, 2000).

Katika wimbo wa ***Mama hoo ho hoo ho*** (mama mbembeleze) kuna matumizi ya takriri sentensi. ñMama mbembelezeò na ñbaba mbembeleze. Sentensi hizi zinajirudiarudia kuanzia mwanzo wa wimbo mpaka mwisho; yaani wimbo huu hujengwa na kujirudiarudia kwa sentensi hizi. Kujirudiarudia huku husisitiza dhima ya kuheshimu wazazi; mama na baba.

Mulokozi na Kahigi (1979) wanabainisha aina mbalimbali za takiriri, mojawapo ya hizo ni takiriri sentensi. Wanaeleza kwamba msanii hutumia aina fulani ya takiriri kutegemea lengo lake. Wimbo huu umetumia takiriri sentensi, ambapo katika mshororo wa kwanza kuna sentensi ñmama hoo ho, hoo hoò, sentensi hii imerudiwa katika mshororo wa pili. Halikadhalika katika mshororo wa tatu sentensi ñbaba hoo

ho, hoo hoò kama ilivyotafsiriwa kulia kwake umerudiwa katika mshororo wa nne. Katika jamii ya Waasu mzazi ni mtu anayehitaji heshima kubwa sana. Hivyo basi, takriri hii husisitiza jambo hilo.

Usanaa wa lugha katika kipengele cha takriri vilevile umejitokeza katika wimbo wa ***Vaisanga vena ngoro mbivi*** (walimwengu wana roho mbaya) ukiwa na lengo la kusisitiza dhima ya kuonya;

> *Vaisanga vena ngoro mbivi ee, vekitie kinehera eeee x2,*
> *Vaisanga vena ngoro mbivi ee, vekitie kinehera eeee x2,*
> *Vapate cha kuteta, mira iki chakuloka,*
> *Cha kuteta chasoveka.*
>
> Walimwengu wana roho mbaya ee, walidhani itashindikana ×2,
> Walimwengu wana roho mbaya ee, walidhani itashindikana ×2,
> Wapate cha kusema, lakini sasa imetimia,
> La kusema limekosekana.

Takiriri inayojitokeza hapa ni takiriri sentensi ambapo mstari wa kwanza umerudiwa katika mstari wa pili. Hii husisitiza suala la kuwaepuka walimwengu, kuwa si watu wazuri kwa hiyo kila mtu anatakiwa kuwa na tahadhari nao. Kwa upande mwingine hutoa maonyo kwa walimwengu kuwa fitina zao haziwezi kufanikiwa katika kukwamisha mipango ya watu. Hivyo waache, la sivyo watabakia fedheha.

Kimsingi takriri hutumiwa kusisitiza jambo au dhana husika, na kwa kawaida jambo linalosisitizwa huwa ni lile lenye umuhimu. Katika mila na utamaduni wa Waasu yapo mambo ambayo hupewa umuhimu zaidi, miongoni mwake ni; kuheshimu wazazi, ni kwamba kwa jamii ya Waasu wazazi huchukuliwa kuwa ni Mungu wa pili, hivyo kuwashimu ni kitu kinachomlazimu kila mtoto. Lingine ni kusifia

maharusi, jamii ya Waasu huchukulia kuwa uimara wa ndoa ni msingi wa ustawi wa jamii, hivyo maharusi hutakiwa kuwa na sifa nzuri na kuziendeleza. Pia suala la kuwa makini na walimwengu huchukuliwa kwa umakini mkubwa, kila mtu hutakiwa kuwa na tahadhari na watu wabaya, na watu hao hupewa maonyo na kusemwa ili wajirekebishe. Hivyo basi, dhima hizi ni muhimu kwa ustawi wa jamii. Hii ndio sababu husisitizwa zaidi kwa kutumia mbinu ya takiriri. Izack (2007) anaeleza kwamba, aghalabu, mbinu ya takiriri hutumiwa ili kutilia uzito wa maneno au mafungu yanayorudiwa.

### 5.2.4 Tashibiha

Tashibiha ni ulinganishaji wa moja kwa moja kwa kutumia maneno kama vile; mithili ya, kama nakadhalika ambao hudhamiria kusisitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini (Wamitila 2010; Senkoro 1988; Steen, 1994; Mulokozi na Kahigi 1979). Kwa mujibu wa data yetu inaonesha kuna baadhi ya nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu hutumia mbinu ya usanaa ya tashibiha. Baadhi ya nyimbo hizo ni kama vile wimbo wa ***Emlanga kaka wetu kivivi*** *(anayemsema kaka yetu vibaya);*

| | |
|---|---|
| *Emlanga kaka wetu kivivi nalifwe,* | Anayemsema kaka yetu vibaya afe, |
| *Emalanga wifi wetu kivivi nalifwe,* | Anayemsema wifi yetu vibaya afe, |
| *Avo vena ngoro mbivi sa vasavi.* | Hao wana roho mbaya kama wachawi. |

Fungu la wimbo huu katika mshororo wa tatu kuna tashibiha; hulinganisha tabia ya watu wenye roho mbaya, wasengenyaji, wanaowasema watu sawa na wachawi kwa kutumia kiunganishi *kama.* Mchawi katika jamii ni mtu anayechukiwa, kuogopwa na kukwepwa, hivyo ulinganishwaji wa watu hawa na wachawi huibua hisia nzito zinazolenga kubadilisha tabia zao. Kimsingi usanaa huu wa lugha umesaidia katika

kujenga dhamira ya maonyo, kama ilivyofafanuliwa katika kipengele cha 4.2.7. Perpetua (2011) anaeleza kwamba matumizi ya tamathali za semi ikiwamo tashibiha yana mchango mkubwa katika kujenga mwitikio wa maudhui ya nyimbo husika kwa watu au jamii lengwa. Hivyo, kwa ujumla tashibiha kama mojawapo ya kipengele cha tamathali za semi kina mchango mkubwa katika kujenga na kushadidia dhima za nyimbo katika jamii ya Waasu na kuibua hisia na fikira zinazosaidia dhima hizo kuwa na athari chanya kwa walengwa wake.

Aidha, matumizi ya tashibiha hujitokeza vilevile katika wimbo wa hiyo ***Pete yetu*** ikishadidia dhima ya kusifia maharusi;

> Hiyo pete yeeetu naitoke naitoke,
> Hiyo pete yeeeetu naitoke,
> Baba na mama wanaingoja, wanaingoja,
> Baba na maaama wanaingoja ×2,
> Tutaitunza kama kioo kama kioo, tutaitunza kama kioo.

Katika wimbo huu mshororo wa mwisho kuna matumizi ya tashibiha; utunzaji wa pete (bibi harusi) unafananishwa na utunzaji wa kioo. "Tutaitunza ***kama*** kioo, ***kama*** kioo, tutaitunza ***kama*** kioo" Kimsingi kioo ni kitu kinachotakiwa kushikiliwa kwa umakini kwani ukikidondosha chini huvunjika kwa urahisi. Hivyo basi, tashibiha hii inasisitiza sifa ya bibiharusi kwamba ni mrembo na mzuri sana, hivyo anatakiwa atunzwe mithili ya kioo. Tashibiha hii imerudiwarudiwa, hii huonesha umuhimu wa bibiharusi kutunzwa. Ujumbe huu kwa ujumla humlenga hasa bwanaharusi juu ya kumtunza mkewe. Wamitila (2006) anasema ulinganishaji huu, yaani tashibiha unadhamiria kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani

kichwani. Kimsingi katika wimbo huu sifa iliyojengwa na tashibiha hii ni urembo na uzuri wa bibi harusi na utunzaji wake, sawa na wa kioo.

Vilevile katika wimbo wa ***Vaisanga vena ngoro mbivi*** (walimwengu wana roho mbaya) matumizi ya tashibiha hujitokeza katika kushadidia dhima ya kuonya;

*Vaisanga vena ngoro mbivi ee, vekitie kinehera ee x2,*
*Vapate cha kuteta aa, miomo sa njugha ee,*
*Mira iki chakuloka aa, cha kuteta chasoveka ee.*

Walimwengu wana roho mbaya ee, walidhani itashindikana ee ×2,
Wapate la kusema ee, midomo kama njuga ee,
Lakini sasa yametimia, la kusema limekosekana.

Tashibiha inajitokeza katika mshororo wa pili, ambapo wasengenyaji wanaonuia kuharibu mipango ya watu (uchumba wa maharusi), midomo yao hufananishwa na njuga. Kimsingi njuga ni kifaa kinachovaliwa shingoni na wanyama kama vile mbwa, ngĀombe au mbuzi, kila wakati hupiga kelele mnyama husika anapotembea. Hivyo wambea, wasengenyaji, wenye majungu ambao midomo yao haitulii kuchukua neno hapa na kulipeleka kule kwa lengo la kufarakanisha watu. Hawa midomo yao kwa mujibu wa data yetu hufananishwa na njuga. Madumulla (2009) anasema tashibiha hutumiwa kulinganisha vitu viwili, kimoja hutumiwa kuelezea kingine. Aghalabu kimoja huwa kinafahamika na hutumiwa kuangazia hichi kingine.

Jamii ya Waasu ni wafugaji kama ilivyobainishwa katika kipengele cha 1.2, hivyo dhana ya njuga pamoja na sifa zake hueleweka kwao. Hivyo basi, makelele ya njuga hufananishwa na wasengenyaji na wambea. Mbinu hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kujenga na kushadidia dhima mbalimbali katika nyimbo za harusi za Waasu, kama

vile dhima ya maonyo dhidi ya watu wenye majungu, wasengenyaji na wambea wanaonuia kukwamisha mambo ya wenzao, kwamba waache. Matumizi ya ishara ya *njuga* katika kuelezea watu wenye tabia za umbea, majungu na fitina, husawiri nadharia yetu ya simiotiki ambayo huelezea kwamba katika fasihi kuna ishara zinazoundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha na utamaduni wa jamii yake. (Cameroon, 1985, Eco, 1976). Kwa ujumla, ishara hizi hueleweka kwa wanajamii husika kulingana na utamaduni wao, uchumi, falsafa, imani na historia ya jamii hiyo.

### 5.2.5 Chuku

Msokile (1992) na Wamitila (2001) wanafafanua chuku kwamba ni tamathali ya semi inayotumika kukuza kitu kupita kiasi. Ambapo kukuzwa huko huweza kuwa kwa ukubwa au udogo, nia ya mbinu hii ya usanaa wa lugha ni kulifanya jambo fulani litokeleze kwa uwazi zaidi, kuikuza sifa fulani na vilevile hutumika kwa lengo la kumfikirisha msomaji ili kuona uzito uliopo katika usemi husika. Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zinazotumia mbinu hii miongoni mwazo ni; ***Kaka esaghure chekoma meso*** (kaka amechagua kinachoumiza macho);

| | |
|---|---|
| *Kaka esaghure chekoma meso,* | Kaka amechagua kinachoumiza macho, |
| *Cheaka ngʾwe ngʾwe ngʾwe,* | Kinachowaka ngĀwe ngĀwe ngĀwe, |
| *Kikome meso x2,* | Kiue/kiumize macho. |

Wimbo huu una matumizi makubwa ya chuku ambapo anayepigwa chuku ni bibiharusi. Wamitila (2006) anasema chuku huweza kutumika kulikuza jambo kupita kiasi kwa upande wa pili huweza kutumika kulidogosha jambo. Katika wimbo huu chuku iliyotumika ni ya kulikuza jambo, ambapo bibiharusi hupewa sifa zilizopitiliza kwamba ana sura nzuri sana inayowaka waka hadi kuua macho. Kwa

kawaida mtu hawezi kuwa na sura nzuri inayongĀaa mpaka iue/kuumiza macho kwa mngĀao wake. Chuku hii imesaidia katika kujenga dhima ya kuwasifu maharusi. Katika mila na tamaduni za Waasu mtu mwenye sifa na tabia nzuri ndiye anakuwa kimbilio la kuozwa au kuozeshwa (kuoa au kuolewa) na kwa wanawake uzuri wa sura na urembo ni kigezo cha ziada. Mbinu hii huibua fikira kwa vijana ambao hawajaolewa na kuoa jinsi ya kujitunza na kujipamba ili nao siku moja waoe/waolewe na kusifiwa.

Halikadhalika chuku imejitokeza katika wimbo wa ***Dada wetu tonga ee (***dada yetu nenda ee), kama inavyojibainisha;

| | |
|---|---|
| *Dada wetu tonga* | Dada yetu nenda |
| *Dada wetu tonga eee x2* | Dada yetu nenda ee Ȥ2 |
| *Uvavonye utanda ee* | Uwaoneshe ustaarabu ee |
| *Verugha makoko ee, veti ni mchere* | Wanapika maboga wanasema ni wali |
| *Verugha viongwe weti ni vughai x2* | Wanapika viazi vitamu wanasema ni ugali |

Chuku iliyotumika katika wimbo huu ni ya kudogosha. Wamitila (2006) na Hassan (2010) wanaeleza kwamba chuku ni semi inayotumika kukuza jambo kupita kiasi, ambapo kukuzwa huko huweza kuwa kwa ukubwa au udogo. Katika wimbo huu chuku hujitokeza katika mshororo wa tatu na wa nne ambapo ndugu wa bwanaharusi wamedogoshwa kwamba hawawezi kupika; wanapika maboga wanasema ni wali na viazi vitamu wanadai ni ugali. Kimsingi hakuna mtu timamu anayeweza kufanya mambo haya; kupika kwa mfano maboga akasema ni wali. Chuku hutumika ili kuikuza sifa fulani na vile vile kumfikirisha msomaji au msikilizaji ili aone uzito wa jambo husika.

Katika wimbo huu chuku imetumika kumsifu bibiharusi, yaani weledi wake katika mambo kwa mfano kupika; kwamba ni wa hali ya juu kilinganisha na wengine. Mbinu hii imesaidia kwa kiasi kikubwa katika kujenga dhima ya kusifu maharusi (bibi harusi) na kurekebisha tabia kwa watu wasio weledi katika majukumu yao (kutojua kupika vizuri).

Katika jamii ya Waasu tumebaini kwamba tabia nyingi zisizotakiwa huelezwa kwa kupitia nyimbo za harusi kwa kutumia mbinu kadhaa, ikiwemo chuku. Aidha chuku zote mbili; yaani ya ukuzaji na udogoshaji hutumika. Chuku ya ukuzaji wa jambo pia imejitokeza katika wimbo wa ***Mshigheni atonge ee*** (Mwacheni aende ee)

| | |
|---|---|
| *Mshigheni atonge eee x3* | Mwacheni aende eee ×3 |
| *Arevona vwasi vwa ijumba* | Akaone taabu za unyumba |
| *Kaa ni mlima ee wesina mhaka* | Ndoa ni mlima ee usio na mwisho |

Chuku inayojitokeza katika wimbo huu ni  ñndoa ni mlima wesina mhakaò (ndoa ni mlima usio na mwisho). Hii ni chuku, yaani matatizo na changamoto za ndoa zimekuzwa kupita kiasi. Kimsingi hakuna mlima usio na mwisho, na hakuna ndoa iliyo na matatizo tu! Chuku hii imetumiwa ili kusisitiza umakinifu na zaidi sana uvumilivu wa ndoa unaotakiwa kwa maharusi. Hunuia kuwaonesha uzito wa ndoa uliopo mbele yao, hivyo kuibua fikira nzito juu ya dhima iliyokusudiwa. Mbinu hii ya usanaa wa lugha imesaidia pakubwa katika kujenga na kutia nguvu dhima mbalimbali katika nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu, kama vile uvumulivu.

Wamitila (2004) anasema chuku hutumika ili kumfikirisha msomaji au msikilizaji na kuona uzito wa jambo lililopo. Aidha Senyamanza (2015) naye alitumia nadharia

ya simiotiki katika kuchunguza nyimbo za *rara* katika jamii za mkoani Mbeya. Halikadhalika Omary (2011) alitumia nadharia hii katika kuchunguza siasa katika ushairi wa Kezilahabi katika diwani ya Dhifa (2008) na Karibu Ndani (1988). Hii huonesha uimara wa nadharia hii katika uchunguzi wa kazi mbalimbali za kifashihi ikiwemo nyimbo.

Kwa ujumla kazi yoyote ya kifasihi iliyo na matumizi bora ya lugha yaliyosheheni mbinu mbalimbali, huibua fikira nzito na kuwa na athari chanya kulingana na dhima na ujumbe uliokusudiwa. Ishara ya ñmlima usio na kikomoò katika wimbo wa mshigheni atonge (mwacheni aende) hapo juu kutumika kuashiria matatizo na changamoto za ndoa. Hapa mlima usio na kikomo ni kiashiriwa na matatizo na changamoto za ndoa ni kiashiria. Ishara hii husawiri nadharia yetu ya simiotiki. Kiashiria ni alama, sauti au herufi zinazotumika kutaja jina la kitu fulani. Kiashiriwa ni kitu halisi kinachorejelewa na alama, sauti au herufi zinazotaja kitu hicho (De Saussure, 1966).

### 5.2.6 Dhihaka

Dhihaka ni tamatahali inayohusiana na kinaya kwa karibu. Katika dhihaka msemaji au mwandishi hutumia usemi unaoficha hisia zake kuhusu mtu au kuihusu hali fulani. Sababu kuu ya kutumia dhihaka ni kumcheka au kumkera mtu (Khatibu, 2009). Dhihaka hunuia kumsema mtu kwa njia isiyo ya moja kwa moja, kwa lengo la kumsababisha akereke ili ajirekebishe dhidi ya tabia fulani isiyofaa au asiyoitaka msemaji.

Wamitila (2016) kwa upande wake anaongezea kwamba dhihaka ni tamathali ya usemi ambapo msanii hutoa kauli kwa nia ya kubeza au kukereketa. Anasema

dhihaka hutumiwa sana pale msanii au msemaji anapotaka kufichua uozo fulani. Maelezo ya wataalamu hawa yamesaidia pakubwa katika kujazilia data yetu ya msingi kwani kimsingi yanayosemwa katika nyimbo za harusi za Waasu kupitia mbinu ya dhihaka ni uozo (tabia isiyotakiwa) unaohitaji kurekebishwa, na wasemwaji hukereketwa wasemwapo.

Kwa mujibu ya data yetu mbinu hii hutumiwa kuwasema watu wenye tabia zisizotakiwa kama wasengenyaji, wafitini na wambea. Nyimbo zilizobeba dhihaka ni kama vile; ***Dada wetu tonga ee*** (dada yetu nenda);

| | |
|---|---|
| *Dada wetu tonga,* | Dada yetu nenda, |
| *Dada wetu tonga eee x2,* | Dada yetu nenda ee ×2, |
| *Uvavonye utanda eee,* | Uwaoneshe ustaarabu, |
| *Verugha makoko ee veti ni mchere,* | Wanapika maboga wanasema ni ugali |
| *Verugha viongwe weti ni vughai x2* | Wanapika viazi vitamu wanasema ni ugali ×2. |

Ubeti huu umejengwa na mbinu ya dhihaka, katika mshororo wa tatu na nne kuna dhihaka. Dhihaka hii imetumika kuwasema watu hasa wasichana wasiokuwa na weledi katika mapishi, lengo lake ni ili wakereke na wajirekebishe. Wimbo huu unawasema watu kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mhando na Balisidya (1976) wanaeleza kwamba katika shrehe za harusi katika jamii, zipo nyimbo zilizoimbwa kuwasema wasichana waliokuwa na tabia mbaya ili wakereke na wajirekebishe. Hivyo basi, wimbo huu husaidia pakubwa kujenga dhima ya kurekebisha tabia kwa watu (wasichana/wanawake) wenye tabia zisizofaa.

Jamii nyingi ikiwemo Waasu watu wasio na weledi katika majukumu yao huchukiwa na kudharaulika. Hivyo, husemwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja ili

wakereke na kujirekebisha. Mbinu hii huibua fikra kubwa kwa wasemwaji hivyo kuwa na mwitikio chanya, vilevile huepusha ugomvi ambao ungetokea kama wahusika wangesemwa kwa njia ya moja kwa moja (kavu kavu). Maneno kama vile *verugha makoko veti ni mchere* (wanapika maboga wanasema ni wali) yametumika ki-ishara kudhihaki watu wenye tabia za kutokuwa weledi katika mapishi au shughuli zao kwa ujumla. Huu ndio msingi wa nadharia ya simiotiki kwamba fasihi hutumia lugha ya ishara za aina mbalimbali, na kwamba jamii husika hutengeneza tafsiri za ishara hizo kwa kuzingatia utamaduni wao na muktadha husika. (Cameroon, 1985, Eco, 1976).

Kwa mujibu wa data yetu dhihaka vilevile hujitokeza katika wimbo wa ***Ena picha yakwe kaka ahundue*** (aliye na picha ya kaka arudishe). Katika mshororo wa tatu wa wimbo huu unaelezea juu ya mtu anayenuka jasho kwamba atazeeka. *"enuka kiruke enekua"* (anayenuka jasho atazeeka). Hii ni dhihaka dhidi ya wasichana wachafu kwamba hawatapata wachumba, watabakia kuzeeka bila kuolewa. Dhihaka hii hunuia kuwasema wasichana wote wachafu ili wakereke, waichukie hali hiyo na kujirekebisha, wakijua kwamba kama hawatabadilika basi itakuwa vigumu kwao kuolewa. Katika jamii ya Waasu kama ilivyo jamii nyingine, suala la usafi hasa kwa msichana ni sifa mojawapo inayompatia mchumba/mume. Uchafu ni kikwazo cha binti kuolewa. Hivyo, dhihaka hii imesaidia kujenga dhima ya kurekebisha tabia na maonyo. Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema matumizi bora ya lugha husaidia kuleta hisia nzito na athari chanya kwa walengwa. Hivyo basi, matumizi ya mbinu hii ni dhahiri hujenga hisia nzito kwa walengwa katika jamii ya watafitiwa.

Kwa mujibu wa nadharia ya simiotiki hufafanua kwamba kila kiashiria huwa na kiashiriwa chake. Katika wimbo huu ñkunuka jashoò ni kiashiriwa yaani kitu/dhana halisi, ambapo kiashiria chake ni ñmtu mchafuò (msichana mchafu), ambaye katika jamii ya Waasu hapendwi. Aidha kwa mujibu wa simiotiki kiashiria lazima kitafsrike katika jamii husika. Hali hii hukamilisha upembe tatu wa nadharia ya semiotiki, kama anavyoeleza Barthes (1994). Hivyo basi, uchambuzi wa data yetu katika kipengele hiki umejengeka vema katika wigo wa nadharia ya simiotiki, hali hii imechangia kwa kiasi kikubwa kuaminika kwa matokeo ya utafti wetu.

Kwa mujibu wa nadharia ya simiotiki kiashiriwa huweza kuwa kitu au dhana halisi. Zipo nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu ambazo katika kipengele hiki cha dhihaka zimetumia kiashiriwa kitu. Wimbo wa ***Ena picha yakwe kaka ahundue*** (aliye na picha ya kaka arudishe) katika mstari wa tatu kuna dhihaka ya kitu halisi (mvwi wedi). Kama inavyobainishwa;

| | |
|---|---|
| *...Mvwi wedi tuuikaa he iziaka* | Mshale mzuri haukai kwenye podo |
| *Yoo chakuloka , kaka apata mshorwa x3* | Leo yametimia, kaka amepata mrembo×3 |

Mshororo wa tatu katika wimbo huu umebeba dhihaka. Dhihaka hiyo huelekezwa kwa wasichana walio na tabia mbaya kwamba wao wataishia kutoolewa, kinyume chake wenye tabia nzuri wanaolewa. Maneno *mshale mzuri* humaanisha msichana mwenye tabia nzuri. Maneno *haukai kwenye podo* humaanisha msichana mwenye tabia nzuri haachi kupata mchumba/mume. Hapa wasichana wenye tabia mbaya husemwa kwa kulinganishwa na wasichana wenye tabia nzuri.

Dhihaka hii hunuia kuwakeresha wasichana wenye tabia mbaya wajirekebishe kama wanataka kuolewa ili nao wawe ñmshale mzuri wasikae kwenye podoò Yaani wasije kuzeekea nyumbai kwao. Dihaka hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kujenga na kutia msisitizo dhima ya maonyo na kurekebisha tabia hususan kwa wasichana dhidi ya sifa ya kuolewa.

Aidha maelezo katika kipengele hiki hujengeka katika wigo wa nadharia ya simiotki ambayo helezea juu ya ishara na uashiriaji, hivyo basi maneno ñmvwi wediò ni ishara na huashiria ñmtu (msichana) mwenye tabia nzuriò na ñteuikaa he iziakaò huashiria msichana mwenye tabia nzuri haachi kupata mchumba/mume. Kimsingi ishara hizi na maana zake hueleweka vizuri kwa jamii ya Waasu kulingana na utamaduni wao na muktadha husika.

### 5.2.7 Methali

Wamitila (2004) anasema methahi ni msemo wa kimapokeo ambao una muundo fulani mahususi, unaokumbukika na unaokusudia kuelekeza, kuadibu, kusuta, kulaumu na kushauri Methali ina sifa kubwa ya utegemezi, huweza kupatikana katika tanzu nyingine za fasihi simulizi na fasihi andishi kama vile nyimbo. Kipera hiki kinapotumika kiwe kimesimama chenyewe au kimechomekwa ndani ya tanzu nyingine dhima yake kubwa ni pamoja na kutoa funzo na maadili, kuongeza urembo katika mazungumzo au kazi husika na kuakisi mtazamo na utamaduni wa jamii. Methali hutumika sana katika fasihi kutokana na ule uwezo wake wa kuyafupisha maelezo (Khatib, 1986).

Katika nyimbo tulizochunguza baadhi ya nyimbo zinazotumia usanaa huo wa lugha ni ***Lubegho lwa mwana luwaja*** (Uchungu wa mtoto unauma);

| | |
|---|---|
| *Lubegho lwa mwana luwaja* | Uchungu wa mtoto unauma, |
| *Aheee luwaja x2* | Aheee unauma ×2. |

Fungu hili katika wimbo wa ñLubegho lwa mwana luwajaò (uchungu wa mtoto unauma) kama ulivyoelezwa kwa kirefu katika kipengele cha 4.2.2 limebeba methali. Methali iliyotumika hapa ni ñlubegho lwa mwana luwajaò (uchungu wa mtoto unauma). Methali hii ni sawa na ile ya kiswahili isemayo *uchungu wa mtoto aujuaye mzazi*. Uchopekaji wa methali hii husaidia kujenga dhima ya kuwaheshimu wazazi. Methali hii hutumika kutoa mafunzo ya maonyo kwa vijana juu ya wazazi wao, ikionesha umuhimu wa heshima kwa wazazi. Kimsingi, katika methali hii huelezea umuhimu wa watoto kuwaheshimu wazazi wao kwani wamewazaa kwa uchungu, kuwalea kwa taabu na shida. Methali zinapotumika katika kazi za kifasihi, au hata zikiwa zenyewe huibua fikira kwa wasikilizaji ambazo husaidia dhima husika kuwaingia wasomaji au wasikilizaji na kujenga mwitikio chanya kwa ujumla.

Aidha, methali nyingine katika data yetu hujidhihirisha katika wimbo wa ***Ena picha yakwe kaka ahundue*** (Aliye na picha ya kaka arudishe);

| | |
|---|---|
| *…Mvwi wedi teuikaa he iziaka,* | Mshale mzuri haukai kwenye podo, |
| *Yoo chakuloka kaka apata mshorwa,* | Leo yametimia kaka yetu amepata mrembo. |

Beti hili katika wimbo huu una metahali ya *"mvwi wedi teuikaa he iziaka"* yaani mshale mzuri haukai kwenye podo. Methali hii ni sawa na ile ya Kiswahili isemayo

*kizuri chajiuza*. Methali hii ina maana kwamba kitu kizuri hakikai bila kutumika, humaanisha msichana mzuri au mvulana mzuri wa tabia hawezi kukosa mke/mume. Methali hii imesaidia katika ujenzi wa dhima ya wimbo huu ambao ni kuonya; kuwaasa wasichanana hata wavulana wenye tabia mbaya wajirekebishe wafanane na wale wenye tabia nzuri ili nao waweze kupata sifa ya kuolewa au kuoa. Wamitila, (2004) anasema kazi kubwa ya methali ni kuibua hisia za wanajamii, hii ni kutokana na sanaa iliyomo katika methali yenyewe, hii husaidia kukamilisha ujumbe kikamilifu. Hivyo basi, methali hii imesaidia kuibua hisia nzito ya dhima ya maonyo kwa vijana wenye tabia mbaya wajirekebisha wafanane na wale wenye tabia nzuri ili waweze kupata wachumba. Kwa upande mwingine, methali hii vile vile imetumika kujenga dhima ya kuwapongeza maharusi kwamba kila mmoja ni mzuri ndio maana amepata mwezi.

Wimbo wa ***Kaka ee kaya ni migayo*** (Kaka ee unyumba/ndoa ni mazungumzo) nao kwa upande wake umebeba methali iliyotumika kusisitiza dhima ya uvumilivu;

| | |
|---|---|
| *Kaka ee kaya ni migayo* | Kaka ee unyumba ni mazungumzo |
| *Dada (binti) ee, kaa ni migayo* | Dada ee (jina la binti) unyumba ni mazungumzo |
| *Kaka (kijana) ee kaka ni migayo* | Kaka ee (jina la bwana harusi) unyumba ni mazungumzo |

Wimbo huu umebeba methali ya ñkaa ni migayoò yaani *ndoa ni mazungumzo.* Methali hii pia imetumika kama takiriri; imerudiwa kuanzia mshororo wa kwanza hadi wa tatu kwa kubadilishana kutaja majina ya maharusi (kaka na dada). Kimsingi methali ina dhima kubwa katika; kuonya, kuadibu na hata kushauri. Methali katika wimbo huu imetumika kwa lengo la kuwashauri maharusi juu ya maisha ya ndoa, kuwa wanahitaji kusuluhisha mambo kwa mazungumzo. Hivyo methali katika

wimbo huu umesaidia kujenga kwa dhati na kusisitiza dhima ya kuvumiliana kwa maharusi katika maisha yao ya ndoa siku zote. Kimsingi methali hutumia lugha ya kiishara na tafsiri yake hujikita katika utamaduni wa jamii husika. Hivyo kipengele hiki vilevile kimeakisi nadharia yetu ya simotiki.

## 5.3 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili uhusiano uliopo kati ya dhima na usanaa wa lugha katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Mjadala umeonesha namna usanaa wa lugha ulivyo na nafasi kubwa na ya pekee katika kujenga dhima katika nyimbo zilizochunguzwa. Aidha, usanaa wa lugha umejengeka katika utamaduni, itikadi, uchumi, falsafa na historia ya jamii iliyochunguzwa, na umesaidia kujenga dhima zilizomo katika nyimbo zilizochunguzwa. Kwa ujumla, usanaa wa lugha na dhima vinategemeana na kukamilishana. Sura inayofuata inahusu muhtasari wa matokeo, mapendekezo na hitimisho.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho inahusu muhtasari wa tasinifu nzima. Matokeo ya utafiti yameelezwa katika sura hii. Vipengele vilivyomo katika sura hii ni muhtasari wa tasinifu, utoshelevu wa nadharia zilizotumika katika mjadala wa data, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, pamoja na mapendekezo ya utafiti. Pia, kuna hitimisho la utafiti.

## 6.2 Muhtasari wa Tasinifu

Tasinifu hii imejengwa na sura sita. Sura ya kwanza imeweka msingi wa tasinifu kwa kueleza utangulizi wa jumla, usuli wa tatizo la utafiti na tatizo la utafiti. Malengo mahsusi ya utafiti yameelezwa, umuhimu wa utafiti na mawanda ya utafiti. Pia, kuna mpangilio wa tasinifu nzima. Sura ya pili inahusu mapitio ya machapisho na nadharia zilizotumika katika mjadala wa data za utafiti. Sura hii imesaidia kujenga hoja ya kufanyika kwa utafiti huu. Sura ya tatu imeeleza mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data. Sura ya nne na ya tano zilihusu uwasilishaji na mjadala wa data uliongozwa na nadharia za Uhalisia na Simiotiki.

Katika sura hii, dhima mbalimbali zimeelezwa, pamoja na kufafanuliwa kwa usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi zilizochunguzwa. Sura ya sita inahusu muhtasari wa tasinifu, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

## 6.3 Utoshelevu wa Nadharia Zilizotumika

Nadharia za Uhalisia na Simiotiki ndizo zilizotumika katika mjadala wa data. Nadharia ya Uhalisia ilimwongoza mtafiti kuwaweka waimbaji wa nyimbo za harusi za jamii ya Waasu katika ulimwengu wao halisi katika uchambuzi wa data zilizowasilishwa katika utafiti huu. Pia, walitazamwa kwa undani jinsi walivyoyachunguza masuala ya kijamii na kuyaweka kama yalivyo na kukubalika kupitia nyimbo zao. Kwa hiyo, nyimbo za harusi za jamii iliyochunguzwa zilitazamwa moja kwa moja bila chuku ili kufanya uchambuzi wa kina kwa kuzingatia historia yao, uchumi wao, falsafa yao, mila na desturi zao. Aidha, nadharia ya Semiotiki ilimruhusu mtafiti kuchunguza ushikamani uliopo kati ya vipengele vilivyochunguzwa katika data zilizowasilishwa. Matumizi sahihi ya nadharia hizo yalitokana na misingi ya kutegemeana na kukamilishana ili kukidhi malengo mahsusi ya utafiti huu.

## 6.4 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhima na usanaa wa nyimbo za harusi za jamii ya Waasu. Uchunguzi uliongozwa na malengo mahsusi mawili kama yalivyobainishwa katika sura ya kwanza. Mjadala wa data uliongozwa na nadharia za Uhalisia na Simiotiki. Matokeo ya mjadala wa data za utafiti yalikuwa kama ifuatavyo;

### 6.4.1 Lengo la Kwanza

Lengo letu mahususi la kwanza lilikuwa kubainisha dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Matokeo yanaonesha kwamba nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zina dhima mbalimbali. Dhima hizo ni nguzo muhimu katika ustawi wa jamii hii kupitia taasisi ya nyimbo za sherehe za harusi. Baadhi ya dhima zinahusu

kuonesha heshima, kuonesha ukarimu, kuvumilia, kuonesha ushirikiano, kurekebisha tabia, kuonya na kutoa pongezi kwa maharusi. Dhima hizo huakisi mitindo ya maisha ya kila siku ya jamii iliyochunguzwa. Kipekee, nyimbo hizo hutazamwa kama kiungo thabiti cha kijamii kinachojenga misingi ya kuifunza jamii kuhusu mila na desturi za jamii yao. Jambo hili linazipa dhima nyimbo za harusi za jamii ya Waasu kama chombo imara kinachoichunguza jamii hiyo kwa kuzingatia misingi ya utamaduni na mazingira yake.

### 6.4.2 Lengo la Pili

Lengo letu mahususi la pili katika utafiti wetu lilikuwa kujadili usanaa wa lugha katika kujenga dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Baadhi ya vipengele vilivyounda kisanaa nyimbo zilizolengwa ni ishara, jazanda, dhihaka, methali na chuku. Vipengele vingine ni tashibiha na takriri. Usanaa uliomo katika vipengele hivyo umetumika kama nguzo imara iliyotumika kuwasilisha dhima zilizochunguzwa katika nyimbo za harusi za jamii ya Waasu katika utafiti huu. Vipengele hivyo, vina nafasi kubwa ya kuishawishi hadhira kuongeza nguvu na umakini wa ushiriki wao wakati wa uimbaji ili kungʼamua dhima zilizomo katika nyimbo zilizolengwa na kuchunguzwa.

Aidha, usanaa wa lugha katika data iliyochunguzwa hujenga utamu wa nyimbo hizo na kuleta msisimko masikioni mwa wasikilizaji. Hali hii huwavutia wasikilizaji kuhamasika kusikiliza nyimbo hizi kwa makini, hali hii husaidia kuleta athari chanya kwao, hivyo kusaidia dhima kusudiwa kwa walengwa. Matokeo ya utafiti wetu vilevile yanabainisha kwamba, vipengele vya lugha vinavyotumika katika ujenzi wa dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu, husawiri mazingira, utamaduni,

falsafa, uchumi na itikadi mbalimbali za jamii iliyotafitiwa. Kimsingi nyimbo hizo hueleweka kwa wanajamii hao kutokana na uzoefu wa jamii yao katika mambo mbalimbali.

## 6.5 Mchango wa Utafiti

Tasinifu hii imebaini kwamba nyimbo za harusi za jamii ya Waasu hutumiwa kama nyenzo maalumu inayosaidia kuibua, kufafanua na kuifunza jamii masuala ya mila na desturi za jamii kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Hii ni kwa sababu nyimbo za harusi zilizochunguzwa ni kama mtaala maalumu uliosheheni mienendo yao kulingana na maadili ya jamii hiyo. Misingi ya mila, desturi, falsafa, historia na maendeleo yao yanarejelewa katika vipengele vingi vya maisha yao ya jadi. Aidha, usanaa katika vipengele vya lugha una mchango mkubwa katika kuvuta makini ya utulivu na kupata udhati wa mambo yanayolengwa katika nyimbo zinazohusika.

## 6.6 Mapendekezo

Mapendekezo kutokana na matokeo ya utafiti huu juu ya maoni ya mtafiti kwa ujumla ni kwa watafiti wajao, kwa viongozi wa serikali, wasomaji, wazazi au walezi katika jamii na taifa kwa ujumla.

### 6.6.1 Mapendekezo ya Kitaaluma

Utafiti huu umefanyikia katika jamii ya Waasu katika wilaya ya Same. Ulidhamiria, moja; kubainisha dhima za nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu. Pili, utafiti huu ulinuia kujadili usanaa wa lugha unaotumika katika ujenzi wa dhima za nyimbo hizi. Hivyo, mtafiti anapendekeza watafiti wengine wajao wafanye utafiti katika nyimbo za jamii za Waasu kama zile za Jando na Unyago na za vilabuni (katika baa za

pombe) hasa katika vipengele vya muundo, mtindo na dhima zake katika kipindi hiki cha utandawazi. Aidha watafiti wengine pia wanaweza kufanya utafiti kama huu nje ya kabila la Waasu.

### 6.6.2 Mapendekezo kwa Serikali

Mtafiti anapendekeza kuwa Serikali ifanye tafiti nyingi kama hizi kupitia taasisi zake au iwawezeshe watafiti kifedha kufanya tafiti kuhusu tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, ambayo kwa hakika tanzu zake nyingi hazijatafitiwa vya kutosha bado. Aidha ihakikishe tafiti hizo zinawasilishwa kwa jamii kwa njia mbalimbali kama vile za semina au warsha ili jamii ipate uelewa wa amali mbalimbali za kijamii na kuweza kuzithamini, kuzidumisha na kuziendeleza. Kwa upande mwingine serikali inashauriwa kutumia utafiti huu na zingine kama hizi katika utengezaji au uboreshaji wa sera zake kuhusu utamaduni wa Mtanzania.

### 6.6.3 Mapendekezo kwa Jamii

Mtafiti anapendekeza wanajamii wawe na utamaduni wa kusoma au kusikiliza kazi za kifasihi hasa nyimbo na kutafakari ujumbe wake. Aidha, mtafiti anashauri jamii ikiwemo ya Waasu kuthamini nyimbo za harusi na kuzichukulia kwa umakini mkubwa, kwani ni mtaala tosha wa maadili na ustawi kwa jamii. Vile vile mtafiti anapendekza jamii iwe na tabia ya kumakinika na dhima katika ka zi mbalimbali za kifasihi kama vile ushairi, kwani katika kazi hizi kumejaa; maadili, mafunzo na mbinu mbalimbali kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya jamii.

## MARELEJEO

Abdulla, M. (2016). *Athari za Kiitikadi Katika Nyimbo za Harusi za Zanzibar***.** Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamil (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Alembi, E. B. (2000). *Understanding Poetry.* Nairobi: Acacia Publishers.

Armitt, L. (2005). *Fantasy Fiction: An Introduction.* New York: Continuum.

Bailey, K. D. (1994*). Methods of Social Reaserch.* Chicago: Maxwell Macmillan International.

Bandura, A. (1971). *Social Learning Theory. New York:* General Learning Press.

Bakari, H. (2010). Nafasi ya Maneno ya Kanga katika Kuhifadhi na Kuendeleza Utamaduni wa Waswahili. Morogoro: Tasinifu ya (M.A), Chuo Kikuu cha Kiislamu (Haijachapishwa).

Barthes, P. (1994). *The Semiotic Challenges*. Berkely: University of Colombia Press

Bernard, B. (2002). *Maudhui na Fani katika Misemo ya Wachaga*. (Tasnifu ya B.A), Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es salaam.

Boote, D. N. and Penny, B. (2005). óScholars Before Researchers: On the Centrality of the Dissertation Literature Review in Research Preparationô. Educational Research, 34. 6, 3 - 15.

Cameron, D. (1985). *Feminism and Linguistic Theory.* London: Macmillan.

Chava, N., and N. David. *(1981). Reasearch Methods in Social Sciences*. London: St.Martinös Press.

Cohen, L. (2000). *Research Methods in Eduation.* London: Routledge Falmer.

Cooper, H. M. (1989). *Person Management and Practice*. Easlang Hampshire:

Publishing House.

De Saussure, F. (1966). *A Course in General Linguistics (W. Baskin, Trans).* New York, NY.: McGra - Hill.

Dornye, Z. (2007). *Research Methodology and Methods.* Magdalen Road Ox4 IRE: Oxford University Press.

Eco, U. (1976). *A Theory Semiotics.* Bloomington: Indiana University Press.

Fink, A. (1998). *Conducting Research Literature Review.* Thousands Oaks, CA: Sage.

Finnegan, R. (1977). *Oral Poetry: Its Nature, Significance, and Social Context.* Nairobi: Oxford University Press.

Freuchen, P. (1962). *Books of the Eskimo*. London: Arthur Burker.

Fried, M. (1987). *Realism, Writing, Disfiguration: On Thomas Eakins and Stephen Crane.* Chicago: The University of Chicago Press.

Jann, J. (1961). *Muntu, The New African Culture: A History of Black Writing.* New York: Grove Press.

Hassan, N. (2010). *Mitindo na Matumizi ya Lugha: Utafiti katika Semi za Bajaji.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Hakim, C. (2000). *Research Design.* London: Routledge.

Hawkes, T. (1977). *Structuralism and Semiotics.* London: Methuen.

Howe, J., na Bryceson, D. (2000). *Poverty and Urbarn Transport in East Africa: Review of Research and Dutch Donor Experience.* World Bank.

Ibrahim, A. (2005). *Kanuni za Ndoa na Maadili ya Familia.* Dar es Salaam: Al-trah Foundation.

Izack, Z. (2007). *Towards Defining Folklore: The Significance of the Messages Found on Daladala Tickets and Bumpers.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Kanyama, A., na Wenz. (2004). ñImages of Everyday Life in the Future Sustainable Cityò: Experience of Back-casting with Stakeholders in five European cities. Fms report no 182. Stockholm.

Kavuna, S. M., na wenzake (2003). *Nuru ya Ushairi kwa Shule Mwongozo na Uchambuzi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kauti, J. (2013). *Mabadiliko ya Dhamira katika Nyimbo za Mwanamke wa Kiyao.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Khatibu, S. M. (1986). ñTamathali za Semi za Kiswahili;ò katika Temu, W.C. na Mbogo, E. (Wah) (1986), Mulika na 18, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Kur. 1-15.

Khatibu, S. M. (2009). ñTamathali za Semi za Kiswahili;ò katika Masabo T. na Mdee, J. S. (Wah) (1999). Mulika na 25, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Kur. 76-91.

Kiganza, P. M. (2011). Ujumi Katika Ushairi wa Mnyampala. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kimambo, I. N. *(1967). The History of Pare to 1900.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kingĉei, K. (2002). *'Suala la Uana katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti Kutoka Kenya katika Utafiti wa Kiswahili'*. Eldoret: Moi University Press.

Kingĉei, K., na Kisovu, C. N. M. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kombo, D. K., and Tromp, D. L. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: New Age International Publishing.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology Methods and Techniques. 2nd Edition.* New Delhi: New Age International Limited Publishers.

Kumar, R. (2010). *A Step - by - Step Guide for Beginners.* Australia: SAGE

Luhanga, A. (1988). The Role of Songs amongst Zigua. A Research Report of the Requirement for the Degree of Bachelor (Unpublished). Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Madumulla, J. S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili, Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd

Maganga, C. M. (1996). *Historia ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mahenge, E. (2009). ñUchambuzi wa Fani na Maudhui katika Semi zilizo kwenye tiketi za Daladalaò katika F. E. M. K. Senkoro na K. K. Kahigi (wah.) Kioo cha Lugha, Juzuu Na. 7. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Idara ya Kiswahili.

Mauya, B. (2006). *Semi: Maana na Matumizi.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu.

Mbonde, P. (2005). ñMethali za Kitandawaziò katika Makala ya Kongamano la Jubilee ya miaka 75 ya TUKI , Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

McGilhrist, I. (1982). *Against Criticism.* London: Faber and Faber Limited.

McNiff, J. (1992). *Art as a Medicine.* London: Jessca Kingsiley Publisher.

Meena, E. (1975). *Misemo A-E.* Nairobi: Transafrica Publishers

Mlambi, A. M. (2017). *Kuchunguza Nyimbo za Asili za Watoto za Wahehe.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mlacha, S. A. na A. Hurskainen. (1995) (Wah.). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti Yenye Mantiki.* Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

Mhando, P na N., Balisidya (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho.* Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

Mohamed, S. A. (2004). *Misemo, Milio na Tashbihi.* Nairobi: Longman Publishers (K) Ltd

Moore, H. T. (1976*). Realism and Naturalism.* London: Donald Pizzer

Mmbogo, N. (2008). *Mabadiliko ya Kimaudhui Kiwakati katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waembu.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Mreta, A. (2008). *Kamusi ya Chasu – Kiingereza – Kiswahili. Language of Tanzania (LOT) Project.* University of Dar es Salaam. LOT Publication: Lexion No. 12.

Mturo, N. (2011). Dhima ya Semi Zilizoandikwa katika Daladala. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha.* Dar es Salaam: Education Publishers and Distributor, Ltd.

Mulokozi, M. M. (1989). ó Tanzu za Fasihi Simuliziô Mulika Na. 21. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI, uk. 1 - 24.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. na K. K. Kahigi. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Dar es Salam, Tanzania Publishing House.

Mulokozi, M. M. (2011). *Fasihi Simulizi: Nyimbo za Kumbi.* Dar es Salaam: TATAKI.

Mutembei A. K. (2012). *Korasi Katika Fasihi.* Chuo Kikuu Dar es Salaam: TATAKI.

Mwipopo, A. (2016). Nafasi ya Muktadha katika Fasihi Simulizi. Mifano Kutoka Katika Nyimbo za Jamii ya Wahehe. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Kwanza (Haijachapishwa). Mbeya: Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Ndungo, C. W., na W. Mwai. (1996). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili.* Nairobi: University of Nairobi.

Ndungo, C. W., na R. M. Wafula. (1993). *Nadharia ya Fasihi Simulizi.* Nairobi: University of Nairobi.

Newman, W. L. (2006). *Social Research.* Boston: Pearson.

Njogu, K., na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ngechu, M. (2002). *Understanding Research Process and Methods.* Nairobi: Nairobi University Press.

Ngure, A. (2010). *Fasihi Simulizi katika Shule na Sekondari.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Nkwera, F. V. (1978). *Kiswahili Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Nkwera, F. V. (2002). *Fasihi Simulizi, Tamrini za Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Busness Printers Limited.

Ntaragwa, M. (2004). *Uhakiki wa Fasihi.* Rock Island IL 61207: Augustana College.

Omari, S. (2006). ñMitindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzaniaò katika Masamba, D.P.B. (Mhariri). Dar es Salaam: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Juz. na. 69, uk. 73-91.

Omary, M. (2011). *Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi*. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Okpewho, I. (1979). *The Epic in Africa.* New York: Colombia University Press.

Okpewho, I. (1990). *The Oral Performance in Africa.* Ibadan: Spectrum Books.

Pembe, J. (2013). Mabadiliko ya Maudhui kutoka Nyimbo za Ngoma ya Msewe kutoka Zanzibar. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam, Tanzania.

Perpetua, A. (2011). *Matumizi ya Lugha ya Picha katika Nyimbo za Kinyankole Zihusuzo UKIMWI.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Pollock, D. (2005). *Remembering: Oral History Performance.* New York: Palgrave Macmillan Press.

Ranger, T. (1996). *The Changing Context of African Music Performance in Zimbabwe.* Washington DC: Caleb Dube.

Samara, E. M. A. (1992). *The Social Function of Luo Burial and General Songs*. A Research Report Submmited in Apartial Fulfilment of the Requirement for the Award of Bacholer Degree (Unpublished). Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

Samwel, M., na wenzake, (2013). *Ushairi wa Kiswahili Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya MEA.* Dar es Salaam: Meveli Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Sengo. T. S. Y. (1973). *Fasihi Simulizi ya Mtanzania na Hadithi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: The Registered Trustee of Al-Amin Education and Research Academy.

Senyamanza, C. A. (2015). *Tathmini ya Mabadiliko ya Rara Mintarafu Maendeleo ya Jamii: Uchunguzi katika Mkoa wa Songwe.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Senyamanza, C. A. ( ?) *Misingi ya Kazi za Kubuni, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Kazi Bunilizi.* Dar es Salaam: Karlijamer Print Technology.

Sharma, R. N. (2008). *Methodology of Eduational Research.* New Delhi: Surjeet Publiations.

Silau, G. (2013). *Kuchunguza Dhima ya Nyimbo Katika Kukuza na Kuimarisha Malezi, Mfano wa Kabila la Wakaguru.* Tasinifu Iliyowasilishwa kwa ajili Masharti ya Kutunukiwa Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Snow, C. P. (1968). *The Realists: Portraits of Eight Novelists.* Macmillan: London.

Spurlin, W., and M. I Fischer. (1985). *The New Criticism and Contemporary Literatury Theory*. New York: Garland Publishing.

Steen, G. (1994). *Understanding Metaphor in Literature: An Emprical Approach*. London: Longman.

Troachim, W. M. K. (2006). *'Social Research Methods' katika* www.socialresearch methods.net(18. 10. 2018).

Uta, R., na K. Roland. (2006). *Lugha ya Mitaani Tanzania.* Germany: Gutenberg University.

Vans, V. (1990). *Introduction to Social Research.* Mcgraw Hill: Unwin Hyman.

Wafula, R. M., na K. Njogu. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Sai Industries Limited.

Wamitila, K. W. (2001). *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers LTD.

Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: English Press.

Wamitila, K. W. (2006). *Kamusi ya Misemo na Nahau.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, S. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide Muwa Publishres Limited.

Wamitila, K. W. (2016*). Kichocheo cha Ushairi.* Nairobi: Vide Muwa.

Yin, R. K. (1984). *Case Study Research: Design and Methods (1st ed).* Beverly Hills, CA: Sage Publishing.

## VIAMBATANISHO

## A: NYIMBO ZA HARUSI ZA WAASU ZILIZOKUSANYWA

| | |
|---|---|
| ***1. Ambiere evava e mghosi ee*** | ***Baba mkwe shikamoo*** |
| *Ambiere evava e mghosi eee x 2* | Baba mkwe shikamoo, shikamoo x2 |
| *Ne Vamcheku eee eee eee x2* | Na akina mama mkwe shikamo x2 |
| *Ghuhieni ngezia x3* | Pokeeni salamu x3 |
| *Jefuma noko hetu* | Zinazotoka huko kwetu |
| *Vazima na Vadori vose vemkezia* | Wakubwa kwa wadogo wanawasalimia |

| | |
|---|---|
| ***2. Ena picha yakwe kaka ahundue*** | **Mwenye picha yake kaka arudishe** |
| *Ena picha yakwe kaka ahundue* | Aliye na picha yake kakaarudishe |
| *Ambu kaka aovoa x3* | Kwa sababu kaka ameoa x3 |
| *Mvwi wedi tuuikaa he iziaka* | Mshale mzuri haukai kwenye podo |
| *Yoo chakuloka , kaka apata mshorwa* | Leo yametimia, kaka amepata mrembo |

| | |
|---|---|
| ***3. Kasanga kavo kahuyuka*** | **Kijijini kwao kumepwaya** |
| *Kasanga kahavo kahuyuka eee* | Kijijini kwao kumepwaya |
| *Kameja mabange na viagho* | Kumeota sangare na ñmabangeò |
| *Mama, iyele iyele iyele ee* | Mama iyele, iyele, iyele ee |
| *Iyele iyele iyele* | Iyele iyele iyele |
| *Kasanga kahavo katindima* | Kijijini kwao kumependeza |
| *Kasanga katindima ee* | Kumeota iliki na migomba |
| *Kameja iliki na majighu* | |

| | |
|---|---|
| ***4. Mwekiketa shida mnatume ee*** | **Mkipata shida mtoe taarifa** |
| *Mwekiketa shaida mnatume ee* | Mkipata shide mtoe taarifa |
| *Ambu kaka wetu si mvivi* | Kwa sababu kaka yetu si mbaya |
| *Mama iyele iyele iyele ee, iyele* | Mama iyele iyele iyele ee, iyele |
| *Iyele iyele* | iyele iyele |
| *Lukwi lwa kibare tukaote ee* | Kuni za kuchana hutaota moto wake |
| *Cho weneota ni makongoti* | Atakachoota ni moto wa magunzi |

| | |
|---|---|
| ***5. Lubegho lwa mwana luwaja*** | **Uchungu wa mtoto unauma** |
| *Lubegho lwa mwana luwaja* | Uchungu wa mtoto unauma |
| *Aheee luwaja x2* | Ahee unauma |
| *Luwaja kangi ugure kikwidi* | Unauma hadi ushike kiuno |
| *Aheee luwaja* | Ahee unauma |
| *Luwaja kangi ugure ndeni* | Unauma hadi ushike tumbo |
| *Aheee luwaja* | Ahee unauma |
| *Luwaja kangi ugure mtwi* | Unauma hadiushike kichwa |
| *Aheeee luwaja* | Ahee unauma |

**6. Chunga idafa**

Chunga idafa, mama wavo (jina la binti), chunga idafa
Mwana etetonga ×2

**Funga Mkanda**

*Funga mkanda mama yake (jina la binti), funga mkanda*
*Mtoto anakwenda x2*

***7. Kaka mgure mkono kidinde***

*Kaka mgure mkono kidinde x2*
*Kaka ee mgure mkono kidinde*
*Uo niye wako wa maisha*

**Kaka mshike mkono kisawasawa**

Kaka mshike mkono kisawasawa×2
Kaka ee mshike mkono kisawasawa
Huyo ni wako wa maisha

***8. Mama virita nkanga***

*Mama virita nkanga mwanao aingie*
*Kakicha tutegoa mwana ngwa ahunduke*
*Angia, angia ra (mara nyingi)*

**Mama mfunike kanga**

Mama mfunike mwanao kanga aingie
Kama hujaridhika mtoto wa watu arudi
Ameingia, ameingia sasa (mara nyingi)

***9.* Mama gusha kaghemba**

*Mama gusha kaghembe*
*Mwanao aingie, kakicha tutegoa*
*Mwana ngwa ahunduke x2*

**Mama weka kijembe**

Mama weka kijembe
Mwanao aingie, kama hujaridhika
Mtoto wa watu arudi ×2

***10.* Anameremeta**

Anameremeta, anameremeta ×2
Mwali wetu anameremeta, anameremeta ×2
Nguo zake zinawaka waka, zinawaka waka ×2
Zinawaka waka, zinawaka waka ×2

***11. Kaka esaghure chekoma meso***

*Kaka esaghure chekoma meso*
*Cheaka ng'we ng'we ng'we*
*Kikome meso x2*

**Kakam amechagua kinachoumiza macho**

Kaka amechagua kinachoumiza macho
Kinachowaka mwaa, mwaa, mwaa
Kiumize macho ×2

***12.* Aiya iya kuolewa**

Aiya iya kuolewa utarudi nyumbani kutembea (korasi)
Kwa heri mama na baba, kuonana majaliwa
Kwa heri kaka na dada, kuonana majaliwa

***13.* Hiyo pete yetu**

Hiyo pete yeeetu naitoke naitoke
Hiyo pete yetu naitoke
Baba na mama wanaingoja, wanaingoja
Baba na mama wanaingoja ×2
Tutaitunza kama kioo kama kioo, tutaitunza kama kioo.

*14.* **Kaka ee**

*Kaka ee kaya ni migayo*
*Dada (binti) eee, kaa ni migayo*
*Kaka (kijana) ee kaka ni migayo*

**Kaka ee**

Kaka ee ndoa ni mazungumzo
Dada ee (jina la binti) ee ndoa ni mazungumzo
Kaka ee (jina la bwana harusi) ndoa ni mazungumzo

***15. Dada wetu tonga ee***

*Dada wetu tonga*
*Dada wetu tonga eee x2*
*Uvavonye utanda eee*
*Verugha makoko veti ni mchere*
*Verugha viongwe weti ni vughai x2*

***Dada yetu nenda ee***

Dada yetu nenda
Dada yetu nenda ee x2
Uwaoneshe ustaarabu
Wanapika maboga wanasema ni wali
Wanapika viazi vitamu wanasema ni Ugali

***16. Wifi unatete mphoa***

*Wifi unatete mphoa hako haharwe kajoto x2*
*Kangi wekiteta nyaka, hako ni njia ya mivwa x2*

**Wifi uwe na upendo**

Wifi uwe na upendo,kwako kuombwe moto
Ukijivuna kwako kutakuwa njia yenye miiba

***17. Twekitie hache***

*Twekitie hache x3*
*Mira tuaghanya tutonga x2*

**Tulitamani tubaki hadi asubuhi**

Tulitamani tubaki hadi asubuhi
Lakini tunaaga tunaondoka

*18.* **Hodi tuvagheni**

*Hooodi tuvagheni, hooodi tuvagheni x2*
*Ghuhieni ngezia jefuma noko hetu*
*Vabaha na vadori veti vemkezia*
*Ambiere evava e mghosi ee*
*Ne va mcheku yeee yeeee yeee*
*Na vana vetu yeee yeeee yeeex2*

**Hodi tu wageni**

Hoodi tu wageni, hoodi tu wageni x2
Pokeeni salamu zinazotoka huko kwetu
Wakubwa kwa wadogo wote wanawasalimia
Baba mkwe shikamoo, shikamoo
Na akina mama mkwe shikamooni
Na watoto wetu marahaba, marahaba x2

***19. Kaka esaghure***

*Kaka esaghure cheve kuvonya*
*Kaka esaghure chekoma meso*
*Cheaka ng'we ng'we ng'we*
*kikoma meso*
*Kaka esaghure chemeremeta x2*

**Kaka amechagua**

Kaka amechagua kinachofaa kuonesha
Kaka amechagua kinachoumiza macho
Kinachowaka mwaa,mwaa, mwaa
kiue/kiumize macho
Tena amechagua kinachomeremeta x2

*20.* **Mshigheni atonge ee**

*Mshigheni atone ee x3*
*Arevona vwasi vya ijumba*
*Kaa ni mlima wesina mhaka*

**Mwacheni aendee**

Mwacheni aende ee x3
Akaone taabu za unyumba
Ndoa ni mlima ee usio na mwisho

***21. Mama wemanyire***

*Mama wemanyire ee mwana ee (bibi harusi) ja mazi, ja mazi uoje viombo x2*
*Iki atonga ee mama ee uneja mazi mwenye uoje viombo*
*Mama wemanyire ee (jina la bibiharusi) chavanga, chavanga uturije mhunga*
*Iki atonga ee mama ee unechavanga mwenye uturije mhunga*

**Mama umezoea**

Mama ulizoea binti ee (jina la bibi harusi) kateke maji,kateke maji uoshe vyombo ×2
Sasa ameenda ee, mama ee, utateka maji mwenyewe uoshe vyombo
Mama ulizoea ee, binti ee (bibi harusi) lima, lima uoteshe mpunga
Sasa ameenda ee, mama ee, utalima mwenyewe uoteshe mpunga

***22. Dada wetu tonga ee***

*Dada wetu tonga eex3*
*Uvavonshe utanda ee*
*Vedika makoko ee, x3*
*Veti ni mkate eee*
*Vedika viogwe x3*
*Veti ni vughai*

**Dada yetu nenda ee**

Dada yetu nenda ee ×3
Uwaoneshe ustaarabu
Wanapika maboga ee ×3
Wanadai ni mkate
Wanapika viazi vitamu
Wanadai ni ugali

***23. Emlanga kaka wetu***

*Emlanga kaka wetu kivivi nalifwe*
*Emalanga wifi wetu kivivi nalifwe*
*Vava wavo mwana lukundo mari*
*Usighoje kuvona mwenye unevona*
*Chekihera tunechinja kagonji na mwana*

**Anayemsema kaka yetu**

Anayemsema kaka yetu vibaya afe
Anayemsema wifi yetu vibaya afe
Baba mtoto upendo ni mali
Usisubiri kuona mwenyewe utaona
Ikishindikana tutachinja kondoo na mtoto

*24.* **Mama huyo**

Maaama huyo mama, mama huyoooo mama
Maaama huyo, mama maama huyo mama
Mpe mkono mama maama huyo mama
Alikule mama maama huyo mama

***25. Twahavache twaighuta***

*Twahavache twahavache, twaighuta,*
*Vila tuorirwe ee*
*Esiighute atete aongejwe ee*

***Tunashukuru tumeshiba***

Ahsanteni, ahsanteni, tumeshiba
Vile tulivyokaribishwa ee
Asiyeshiba aseme aongezwe

***26. Mama hoo ho***

*Mama hoo ho, hoo ho*
*Mama hoo ho hoo ho*
*Baba hoo ho hoo*
*Baba hoo ho hooho*

**Mbembeleze mama**

Mama mbembeleze, mbembeleze
Mama mbembeleze mbembeleze
Baba mbembeleze mbembeleze
Baba mbembeleze mbembeleze

*27.* **Kaka tulikuambia uende**

Kaka ee tulikuambia uende
Kaka ee tulikuambia uende
N a leo ee inama uokote × 3

***28. Kaka wetu ringa ee***

*Kaka wetu ringa ee* ⊐3
*Wapata mwai wekela hoteli iki tukale ee x2*

**Kaka yetu ringa ee**

Kaka yetu ringa ee ⊐3
Umepata mke, sasa hutakula hotelini ⊐2

***29.* Mama Huyo**

*Maaama huyo, mama, mama huyo ee*
*Mama mama huyo mama maaama huyo mama*
*Mpe mkono, mama, maaama huyo mama*
*Alikulea, mama maaama huyo mama*
*Baaaba huyo, baba baba huyo ee x*
*Baba baba huyo baba baaaba huyo baba*
*Mpe mkono, baba baaba huyo baba*
*Alikule baba baaba huyo baba x2*

***30.* Vaisanga vena ngoro mbivi**

*Vaisanga vena ngoro mbivi, vekitie kinehera ee x2*
*Vapate cha kuteta, miomo sa njughamira*
*Mira iki chakuloka, cha kuteta chasoveka*

**Walimwengu wana roho mbaya**

Walimwengu wana roho mbaya ee walidhani itashindikana ⊐2
Wapate la kusema, mdomo kama njuga
Lakini sasa yametimia, la kusema limekosekana

## B: MASWALI YA HOJAJI KWAVIJANA (Miaka 25-45)

**KIJIJI/MTAA**________________________________

**UMRI**________________________________

**JINSIA**_______________________________

**Utangulizi**

Mimi ni Elihaki Yonazi, ni Mwanachuo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ninafanya Shahada ya Uzamili ya Sanaa katika Kiswahili (MA ï Kiswahili). Nipo katika utafiti wa ñKuchunguza Dhima na Usanaa wa Lugha Katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasuò Wewe kama mdau unaombwa kutoa mchango wako wa mawazo na uzoefu katika nyimbo hizo. Aidha nakuhakikishia kwamba taarifa zako zote zitatumika kwa ajili utafiti tu na sio kwa nia nyingine yoyote ile.

**Maswali;**

**Weka alama ya tiki katika jibu unalofikiri ni sahihi**

**1.** Katika sherehe za harusi katika jamii ya Waasu kuna nyimbo zozote zinazoimbwa. NDIYO/HAPANA

2. Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu huimbwa kwa lugha ipi; (a) chasu tu (b) chasu na kiswahili (c) kiswahili tu (d) lugha nyingine

3. Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zina umuhimu gani? (a) kuburudisha tu (b) hazina umuhimu wowote (c) kuwafahamisha watu kwamba eneo husika lina sherehe (d) kuwapa maonyo  wanaooana (e) kuonesha kwamba watu wameshiba na kulewa

**Jibu maswali yafuatayo kwa kifupi**

4. Taja nyimbo walau tatu anazozifahamu zinaimbwa kwa lugha ya Chasu katika harusi za Waasu

   (i)é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

   (ii)é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

   (iii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

5. Nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zinatumia vipengele vipi vya usanaa wa lugha?

   (i)é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

   (ii)é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

   (iii) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

   (iv) é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é é

6. Nitajie walengwa wakuu wa nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu____________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

**C. MASWALI YA USAILI KWA WAZEE (Miaka 60-75)**

**KIJIJI/MTAA**________________________________

**UMRI**________________________________

**JINSIA**_______________________________

Mimi ni Elihaki Yonazi, ni Mwanachuo wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, ninafanya Shahada ya Uzamili ya Sanaa katika Kiswahili (MA ï Kiswahili). Nipo katika utafiti wa ñKuchunguza Dhima na Usanaa wa Lugha Katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waasuò Wewe kama mdau unaombwa kutoa mchango wako wa mawazo na uzoefu katika nyimbo hizo. Aidha nakuhakikishia kwamba taarifa zako zote zitatumika kwa ajili utafiti tu na sio kwa nia nyingine yoyote ile.

**Maswali;**

1. Wimbo wa*“ambiere evava e mghosi ee ne vamcheku…(baba mkwe shikamoo na mama mkwe pia…)”* huibwa na watu wa kabila gani?...........,huimbwa katika tukio gani?.............

2. Je, wimbo wa*“ambiere evava e mghosie eee”* ilikuwepo tangu zamani?.................. Kama ndio unafikiri ni kwa nini haujabadilika?..............................................................................

3. Je, nyimbo za harusi katika jamii ya Waasu zina mvuto wowote? Kama ndio unafikiri ni mambo gani yanayozipa mvuto huo?é é é é é é é é é , é é é é é é é é é é é , é é é é é é é é é é é é , é é é é é é é é é é é é é é ., é é é é é é é .

4. Je, nyimbo za harusi za Waasu zina mafunzo yoyote?.................Kama ndiyo yatajeé é é é é .., é é é é é é é é .., é é é é é é é é ., é é é é é é é é é .

5. Nitajie vipengele vya utamaduni wa Waasu vinavyojitokeza katika nyimbo za harusi za Waasu;

é é é é é é é .., é

**D: MWONGOZO WA MBINU YA USHIRIKI**

(a) Ushiriki wa mtafiti kuimba nyimbo za harusi katika sherehe zilizobainishwa pasipo kufahamika kwa watafitiwa

(b) Mtafiti kushiriki shughuli nyingine zinazoambatana na sherehe hizo kama vile kucheza ili kutotiliwa shaka na watafitiwa

(c) Mtafiti kutumia kinasasauti kurekodi nyimbo za harusi za Waasu katika sherehe zilizobainishwa pasipo kugundulika (kukificha mfukoni)